# Al-Madiinatu Al-Munawwarah

## Fadhila zake,
## Msikiti wa Mtume,
## Chumba cha Mtume



Utangulizi wa Mheshimiwa Sheikh

Abdur-Rahman ibnu Abdul-aziz as-Sudais

Raisi mkuu wa usimamizi wa mambo ya Msikiti Mtakatifu na Msikiti wa Mtume,
Imamu na Hatibu wa Msikiti Mtakatifu.

Utunzi wa

Sheikh Dkt. Abdul-Muhsin ibnu Muhammad Al-Qaasim
Imamu na Hatibu wa Msikiti Mtukufu wa Mtume

# Al-Madiinatu Al-Munawwarah

## Fadhila zake, Msikiti wa Mtume, Chumba cha Mtume

Pangusa kodi ifuatayo uweze kuteremsha vitabu kutoka tovuti

# Al-Madiinatu Al-Munawwarah

## Fadhila zake, Msikiti wa Mtume, Chumba cha Mtume

**Utangulizi wa Mheshimiwa Sheikh**
**Abdur-Rahman ibnu Abdul-aziz as-Sudais**

**Utunzi wa**
**Sheikh Dkt. Abdul-Muhsin ibnu Muhammad Al-Qaasim**
**Imamu na Hatibu wa Msikiti Mtukufu wa Mtume**

Amesema Sheikhul Islaam Ibnu Taymiyyah -Allah amrehemu-: **«Ikiwa mnajua kitabu chochote kuhusu Madina kilichokusanya habari zake; kama kulivyotungwa kuhusu habari za Makkah; labda mtujuze nacho».**

**al-Fataawaa, 6/373**

# Utangulizi wa Mheshimiwa Sheikh Abdur-Rahman ibnu Abdul-aziz as-Sudais

Sifa njema zote ni za Allah aliyetakasika, sifa anazostahiki yeye pekee, tunamtakasa kwa sifa na utukufu wake, na tunamuomba atupe hali njema na matokeo mazuri, Pia tunamswalia nabii wetu, bwana wetu na kipenzi chetu Muhammad ibnu Abdullah aliyechaguliwa kwa sifa bora kabisa na cheo kitukufu. Swala za Allah ziwe juu yake, watu wake na masahaba zake ambao walimfuata kwa daraja ya juu kabisa, na tabiina (waliokuja baada ya masahaba) na wale waliowafuata kwa wema maadamu usiku na mchana zaendelea kupishana, na awateremshie salamu nyingi.

Ama baada ya himdi hii

Hakika Allah ana hekima kubwa katika anachoumba na kukichagua, Allah aliyetukuka amesema:

﴿وَرَبُّكَ يَخۡلُقُ مَا يَشَآءُ وَيَخۡتَارُۗ﴾

«Na Mola wako Mlezi huumba na huteuwa atakavyo» [Al-Qaswas: 68].

Na hakika Allah aliyetukuka alichagua katika miji ile ilio bora kabisa, na miongoni mwa sehemu zile tukufu mno; akaziwekea fadhila mahususi , akazipa utukufu na akaadhimisha ujira ndani yake: Miongoni mwazo ni: Allah -aliyetukuka- kuichagua al-Madiina al-Munawwarah pawe pahala pa kuhamia Mtume wake swala na salamu za Allah zimshukie, Mtume swala na salamu za Allah zimshukie akajenga ndani yake msikiti wake mtukufu. Allah akampendekezea Mtume (mji huu), akamsahihishia na akaubarikia.

Vilevile Allah akatoa makemeo kupitia kinywa cha Mtume wake, swala na salamu za Allah zimshukie kwa yeyote atakayewakusudia watu wake kwa uovu, na akaifanya sehemu ambayo Imani itajikusanya na kurejea (pindi miji mingine

itakapoharibika zama za mwisho), kwa hivyo ni ardhi yenye thamani na nchi yenye uzuri.

Na anayempenda Mtume swala na salamu za Allah zimshukie na mji wake, basi hushikamana na Sunnah yake iliyonyooka, hutetea maadili na mipaka yake, na huishi kwa kiwiliwili na moyo wake katika mabustani yake, na hunywa kutoka kwenye maji yake safi kwa kupitia fahamu nzuri, mbali na njia za ubaguzi na ukabila.

*Mnao Madina kaburi la Mtume na sehemu ziliong'ara, japo athari hufifia na kupotea (lakini hizi hazipotei),*

*Wala hazifutiki alama katika mji mtukufu.*

*Mnao ndani yake mimbari ya Mtume aliokua akiipanda.*

*Mnao alama na athari zilizobaki, (zinazoonyesha wazi makazi yake Mtume), na nyumba yake ilio na mahala pa kuswalia na pia kuna msikiti.*

*Mnao ndani yake vijumba ambazo nuru ilikuwa ikishuka kutoka kwa Allah na kuangaza.*

*Athari ambazo hazikumalizika kwa kupitiwa na wakati mrefu.*

Wanachuoni kwa hakika wameendelea kuupa umuhimu mji wa Mtume Al-Madiinatu al-Munawwarah tangu nyakati na karne ziliopita; kukaandikwa vitabu kuihusu Madina katika nyanja mbalimbali, katika historia yake, fadhila zake, adabu na hukumu zake. Kwa kweli, ni katika mambo yanayoleta furaha na bashasha, kuona kitabu hiki chenye kunufaisha kinachoitwa na: «**Al-Madiinatu al-Munawwarah: fadhwaailuhaa, al-Masjidun-Nabawi, al-Hujratun-Nabawiyyah**» (Al-Madiinatu al-Munawwarah, Fadhila zake, Msikiti wa Mtume na Chumba cha Mtume), kilichoandikwa na ndugu yetu wa heshima, na mwenzetu mpendwa, mwenye fadhila Sheikh Dkt. Abdul-Muhsin ibnu Muhammad Al-Qaasim - Imamu na hatibu wa msikiti mtukufu wa Mtume-. Akakusanya hukumu kadhaa zinazohusiana na mji wa Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie, na fadhila zilizopokewa kuhusu mji huo, pamoja na kuzingatia kwa kina

mapokezi sahihi na maandiko yalio wazi na sentensi nyepesi fasihi.

Na hakika Allah amemtunuku kwa kumfanya imamu wa msikiti wa Madina, kuhutubu juu ya mimbari yake na kufunza ndani yake kipindi kinachofikia robo karne. Kwa hivyo, yeye ndiye anayefaa zaidi kuandika kuhusu hukumu zake, cheo na fadhila zake.

Na katika zama hizi angavu, al-Madiinatu al-Munawwarah ilipata uangalizi mzuri wa viongozi wa nchi hii iliyobarikiwa – Mamlaka ya Kiarabu ya Saudia - kwa kusimamia kwao na kupatia kipaumbele kila jambo ambalo linauhudumikia Uislamu na Waislamu, pamoja na kuyatukuza maeneo yao matakatifu. Jambo ambalo limefanya wanaotembelea na wenye kufanya Hija na Umra kuona athari yake. Na Sisi katika uongozi mkuu wa mambo ya msikiti mtakatifu (wa Makkah) na msikiti wa Mtume tunashughulikia kila jambo linalodhihirisha cheo cha Misikiti Miwili Mitukufu, na kuwaelimisha wageni wanaoyatembelea, wenye kufanya Umra na mahujaji kuhusu adabu na hukumu za Msikiti mtakatifu na Msikiti wa Mtume, kupitia mwanga wa Qurani na Sunnah kwa njia itakayopelekea kufikia matarajio ya uongozi wa busara.

Na hakika sheikh alinidhania vyema na kunipa fursa ya kuandika baadhi ya mistari mwanzo wa kitabu chake, basi natarajia Allah atawanufaisha watu na mtunzi na kitabu chake, na atuzidishie ujira mimi, yeye na wasomaji watukufu, na atuhifadhie itikadi yetu, uongozi wetu, nchi yetu na neema zetu, amani, usalama na utulivu wetu; kwani Yeye ndiye mbora anayeombwa na kutarajiwa.

***Ameandika, anayewapenda na anayewaombea -***

***Abdur-Rahman ibnu Abdul-aziz as-Sudais -***

***Raisi mkuu wa usimamizi wa mambo ya Msikiti Mtakatifu na Msikiti wa Mtume,***

***Imamu na Hatibu wa Msikiti Mtakatifu.***

بسم الله الرحمن الرحيم

# Utangulizi

**Sifa zote njema anastahiki Allah, Mola Mlezi wa walimwengu wote, na swala na salamu za Allah zimshukie Mtume wetu Muhammad, na jamaa zake na masahaba zake wote, na baada yake.**

**Ama baada ya himdi hii:**

Hakika Allah ameutukuza mji wa Mtume wake swala na salamu za Allah zimshukie kwa fadhila kadhaa, akautilia baraka, na akazifanya roho za Waislamu zitamani kwenda kuswali katika msikiti wa Mtume wa Allah -swala na salamu za Allah zimshukie. Na Wanachuoni wakubwa walitamani kujua kitabu kilichokusanya habari za Madina. Amesema Sheikhul Islaam Ibnu Taymiyyah Allah amrehemu: «Ikiwa mnajua kitabu chochote kuhusu Madina kilichokusanya habari zake; kama kulivyotungwa kuhusu habari za Makkah; labda mtujuze nacho»[1].

Na kitabu hiki kinatumiwa na mwenye kuzuru Madina na wengineo, ili waweze kufikia malengo yao kwa kupata kuujua mji wa Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie na msikiti wake. na nimekipa jina: «**Al-Madiinatu al-Munawwarah[2]: fadhwaailuhaa, al-Masjidun-Nabawi, al-Hujratun-Nabawiyyah**».

Namuomba Allah anufaishe kwa kitabu hiki, na akijaaliye ni kwa ajili yake pekee.

**Na swala na salamu za Allah ziwe juu ya Mtume wetu**

1 Fataawaa Sheikhul Islaam, 2/373.

2 Al-Munawwarah: yenye nuru kwa ajili ya kuteremka wahyi ndani yake.

**Muhammad, na juu ya watu wake na masahaba zake wote.**

***Dkt. Abdul-Muhsin ibnu Muhammad Al-Qaasim***
*Imamu na Hatibu wa Msikiti Mtukufu wa Mtume.*

# Safari ya Kuelekea al-Madiinatu al-Munawwarah

# Kuitakasa Nia

Allah alituumba ili tumuabudu Yeye, amesema Allah -aliyetakasika-:

﴿وَمَا خَلَقۡتُ ٱلۡجِنَّ وَٱلۡإِنسَ إِلَّا لِيَعۡبُدُونِ﴾

«Na sikuwaumba majini na binadamu ila waniabudu mimi» [Adh-Dhariyat: 56].

Allah akaamrisha atakasiwe ibada yeye pekee, akamwambia nabii wake:

﴿قُلۡ إِنِّيٓ أُمِرۡتُ أَنۡ أَعۡبُدَ ٱللَّهَ مُخۡلِصٗا لَّهُ ٱلدِّينَ﴾

«Sema: Hakika mimi nimeamrishwa nimuabudu Allah kwa kumtakasia Dini Yeye tu» [Az-Zumar: 11].

Na aliamrisha umma zilizopita jambo hilo (la kumtakasia Ibada), akasema Allah -aliyetukuka-:

﴿وَمَآ أُمِرُوٓاْ إِلَّا لِيَعۡبُدُواْ ٱللَّهَ مُخۡلِصِينَ لَهُ ٱلدِّينَ حُنَفَآءَ وَيُقِيمُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَيُؤۡتُواْ ٱلزَّكَوٰةَۚ وَذَٰلِكَ دِينُ ٱلۡقَيِّمَةِ﴾

«Na hawakuamrishwa ila wamuabudu Allah (peke yake) kwa kumtakasia Dini, waepuke ushirikina na waelekee kwenye imani, na washike Swala, na watoe Zaka. Na hiyo ndiyo Dini iliyonyooka» [Al-Bayyinah: 5].

Umma huu pia uliamrishwa kumpelekea ibada Yeye pekee. Amesema Allah -aliyetakasika-:

﴿فَمَن كَانَ يَرۡجُواْ لِقَآءَ رَبِّهِۦ فَلۡيَعۡمَلۡ عَمَلٗا صَٰلِحٗا وَلَا يُشۡرِكۡ بِعِبَادَةِ رَبِّهِۦٓ أَحَدَۢا﴾

«Basi yeyote anayetaraji kukutana na Mola wake Mlezi basi na atende matendo mema, wala asimshirikishe yoyote pamoja na Yeye katika ibada» [Al-Kahf: 110].

Na kutakasika amali kutokamana na ushirikina na riyaa ni sharti la kukubaliwa amali hiyo na Allah.

Amesema Mtume swala na salamu za Allah zimshukie «**Hakika Allah hakubali matendo isipokuwa yale aliyotakasiwa Yeye peke, na akatakwa kwayo uso wake na radhi zake**». Imepokewa na An-Nasaai. Kwa hivyo, ni wajibu kwa muislamu kuzifanya amali zake zote ni kwa ajili ya Allah, zikiwemo Hija, Umra na kuzuru msikiti wa Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie, hatafuti kwa ibada hizo kujionesha, kusifiwa wala kujigamba.

Na pamoja na ikhlasi, ni wajibu pia amali iafikiane na muongozo wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie. Amesema (Mtume) swala na salamu za Allah zimshukie: «**Yeyote atakayefanya amali ambayo si katika dini yetu; basi atarudishiwa**». Imepokewa na Muslim

Na mwenye kumtakasia Allah amali kulingana na kitabu cha Allah na sunnah ya mtume wake swala na salamu za Allah zimshukie, basi Allah humpa furaha duniani na akhera, na kumfanya miongoni mwa watu wa peponi, Amesema Allah -aliyetukuka-:

﴿مَنْ عَمِلَ صَٰلِحًا مِّن ذَكَرٍ أَوْ أُنثَىٰ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَنُحْيِيَنَّهُۥ حَيَوٰةً طَيِّبَةً ۖ وَلَنَجْزِيَنَّهُمْ أَجْرَهُم بِأَحْسَنِ مَا كَانُوا۟ يَعْمَلُونَ﴾

«Yeyote atakayetenda mema, akiwa ni mwanamume au mwanamke, hali ya kuwa ni Muumini, basi tutampa maisha mema (duniani); na tutawalipa ujira wao (huko Akhera) kwa uzuri zaidi ya walivyofanya (duniani)» [An-Nahl: 97].

# Hatari ya Riya

Riya: ni mtu afanye amali njema, akaipamba na kuirembesha ili watu wapate kumsifu kwa amali hio. Pia inaingia katika Riya: Mtu kuificha amali yake kwa ajili ya Allah kisha awaelezee watu (alichofanya); Na Riya haingii isipokuwa kwa mtu wa ibada. Nayo ni hatari zaidi kwa umma huu kuliko Masihi dajali. Kumepokewa kutoka kwa Abu Saiid Al-Khudri amesema: Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amesema: «**Nisiwajulisheni ninalowaogopea zaidi kuliko Masihi dajali?**». Akasema [mpokez]: [Masahaba] Wakasema: Kwani [yaani: tujulishe], [Mtume] akasema: «**Ni ushirikina uliofichika: (Nayo ni) asimame mtu kuswali, aipambe swala yake kwa ajili ya kuona kuna mtu anamuangalia**». Imepokewa na ibnu Maajah.

Na Hija na Umra ni miongoni mwa amali bora mbele ya Allah, na Shetani anaenda mbio kuziharibu (amali hizi) kwa Riya, akampambia mja awaambie watu: Nilihiji Nyumba tukufu ya Allah; Ili wapate kumsifu, au wamuite "al-Haajj" katika nchi yake, na mfano wa hayo.

Na mwenye kujionyesha hapati thawabu ya amali yake, amesema Mtume swala na salamu za Allah zimshukie: «**Amesema Allah aliyetukuka: "Mimi ndiye mkwasi zaidi na ushirikina. Yeyote atakayefanya amali akanishirikisha nayo mimi na mwingine, basi nitamuacha yeye na shirki yake"**». imepokewa na Muslim. Mwenye shirki yake amepewa makemeo ya moto. Amesema Allah -aliyetakasika-:

﴿مَن كَانَ يُرِيدُ ٱلۡحَيَوٰةَ ٱلدُّنۡيَا وَزِينَتَهَا نُوَفِّ إِلَيۡهِمۡ أَعۡمَٰلَهُمۡ فِيهَا وَهُمۡ
فِيهَا لَا يُبۡخَسُونَ ۝ أُوْلَٰٓئِكَ ٱلَّذِينَ لَيۡسَ لَهُمۡ فِي ٱلۡأٓخِرَةِ إِلَّا ٱلنَّارُۖ
وَحَبِطَ مَا صَنَعُواْ فِيهَا وَبَٰطِلٞ مَّا كَانُواْ يَعۡمَلُونَ﴾

«Yeyote atakaye (kwa matendo yake) maisha ya kilimwengu

na starehe zake, tutawalipa humo matendo yao yakiwa kamili bila ya kupunguzwa. Hao ndio ambao hawana huko Akhera isipokuwa Moto, na waliyo yafanya yatapomoka (na watakosa manufaa yake), na matendo yao yatabatilika (kwa kuwa hayakukusudiwa Allah)». [Huud: 15-16].

Na dawa ya Riya: ni kuomba kwa ikhlasi, ukumbuke utukufu wa Allah na udhaifu wa viumbe, na kwamba watu hawatokunufaisha isipokuwa kwa kile ulichoandikiwa na Allah, na pia ufiche matendo yako mema, uyahifadhi kwa ajili ya Mola Mlezi wa viumbe wote.

## Ananuwia nini anayetaka kuzuru Al-Madiinatu Al-Munawwarah?

Anuwie mwenye kuzuru: kuuzuru Msikiti wa Mtume pekee, nalo ndilo lengo la kuzuru na kusafiri kwenda Madina. Wala asinuwie wakati yuko katika nchi yake kusafiri kwa ajili ya kuzuru kaburi au kitu kingine; Kwa sababu kusafiri kwa ajili ya sehemu mahususi haijuzu isipokuwa kuenda misikiti mitatu; Kwa kauli ya Mtume swala na salamu za Allah zimshukie: «**Hazifungwi safari [za kiibada] isipokuwa kuelekea Misikiti mitatu: Msikiti wangu huu, Al-Masjid Al-Haraam [Makkah], na Msikiti wa Al-Aqsa**». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea. Amesema Ibnu Hajar Allah amrehemu: “Neno: «*Laa tushaddu ar-Rihaal*» mwanzo wake ni Dhwamma, tamko hili ni la kukanusha, na makusudio yake ni kukataza kusafiri kwenda kwengine kusiokuwa huko”[1].

Amesema Abu Muhammad al- Juwayni Allah amrehemu: “Ni haramu kufunga safari kwenda sehemu nyingine, kwa mujibu wa maana ya dhahiri ya Hadithi hii”[2].

Mtu anapofika Madina, azuru kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie na masahaba zake wawili, Msikiti wa Qubaa, eneo la makaburi ya Al-Baqi’i na makaburi ya mashahidi wa Uhud.

Na ziara ya maeneo hayo, iwe ni kufuatia pamoja na ziara ya Msikiti wa Mtume, sio peke yake - yaani, asinuwie kufunga safari kwa ajili yake. Amesema Sheikhul Islaam Ibnu Taymiyyah Allah amrehemu: “Iwapo atasafiri kwenda Qubaa kutoka nyumbani kwake, haitajuzu. Lakini akisafiri kwenda msikiti wa Mtume kisha akaenda Qubaa kutoka huko, basi hili linapendekezwa, kama vile

1 Fat-hul Baarii, 3/64.

2 Fat-hul Baarii, 3/65.

kunapendekezwa kuzuru makaburi ya watu wa Al-Baqi'i na mashahidi wa Uhud"[1].

Ama kusafiri kwa ajili ya kufanya biashara, kutafuta elimu, au kuunga kizazi, basi inajuzu; Kwa sababu haijakusudiwa pahala au sehemu kwa ajili ya fadhila yake, lakini si mengine msafiri anakusudia kwa kuenda huko kupata matakwa yake, popote yalipo, Kama biashara iko upande wa mashariki angeiendea. Na lau iko upande wa maghribi pia angeiendea. Kwa hivyo, yeye hajakusudia katika mambo haya sehemu kwa dhati yake [kwa ajili ya sehemu yenyewe].

Amesema Sheikhul Islaam Ibnu Taymiyyah Allah amrehemu: "Kauli yake Mtume: «**Hakusafiriwi isipokuwa kuenda kwenye misikiti mitatu**», inaingia ndani yake makatazo ya kusafiri kwenda kila sehemu inayokusudiwa, tofauti na ikiwa safari ni kwa ajili ya biashara, kutafuta elimu na kadhalika. Kwani kusafiri kwa ajili ya kutafuta mahitaji hayo ni popote yalipo. Vivyo hivyo, kusafiri kwenda kumtembelea ndugu katika imani, kwani yeye ndiye anayekusudiwa popote alipo"[2].

1 Fataawaa Sheikhul Islaam, 27/22

2 Fataawaa Sheikhul Islaam, 27/21.

## Kusafiri Mwanawake bila Mahram

Allah alinyanyua cheo cha mwanawake na akamlinda, na katika utukufu wa mwanamke ni kwamba hasafiri isipokuwa pamoja na Mahram wake[1], anayemlinda na kumtunza, na kumkinga na watu wa waovu. Na ili kuonyesha umuhimu wa Mahram, Allah alimuondoshea mwanamke Hija na Umra iwapo haijakuwa na wepesi kwake [kusafiri na Mahram]. Amesema Mtume swala na salamu za Allah zimshukie: «**Sio halali kwa mwanamke anayemuamini Allah na Siku ya Mwisho kusafiri umbali wa siku moja, isipokuwa pamoja na Mahram**». Imepokewa na Muslim. Amesema Ibnu Hajar Allah amrehemu: “Na kauli yake: «**Mwanamke asisafiri isipokuwa pamoja na Mahram**», inaenea kila safari; kwa hivyo inaingia pia Hija"[2].

Na kusafiri kwa mwanamke pamoja na wanawake wengine waaminifu hakumtoshi na (uwepo wa) Mahram. Na endapo mwanamke atanuwia Hija na Umra na akakosa Mahram, basi Allah kwa fadhila yake humuandika ujira wake hata kama hakufanya Hija au Umra.

1 Mahram wa mwanamke ni: mume wake, au yeyote ambaye ni haramu kwake kumuoa milele - kama vile mwanae na nduguye - Ama binamu, ndugu yake mume, na mume wa dadake; basi wote hao sio Mahram.

2 Fat-hul-Bari 4/77.

## Hukumu ya kusema: “Nifikishie salamu zangu kwa Mtume swala na salamu zimshukie”

Baadhi ya watu wanapomwona mtu anaenda Madina wanamwambia: “Ukifika kwenye kaburi la Mtume, basi nifikishie salamu zangu kwa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie; na jambo hili halifai. Kwa sababu halikuja katika Sunnah.

Na Allah alimkirimu Nabii wake kwa (kumwekea) Malaika wanaomfikishia salamu kutoka kwa umma wake sehemu zote walipo, basi ukisema nawe uko mahali popote: “Ewe Allah, mfikishie swala na salamu Mtume wetu Muhammad"; basi malaika wanamfikishia Mtume swala na salamu za Allah zimshukie salamu zako. Amesema Nabii swala na salamu za Allah zimshukie: «**Hakika Allah ana Malaika wanaozunguka ardhini wakinifikishia salamu kutoka kwa umma wangu**». Imepokewa na An-Nasaai.

Na atakayekuambia: “Nifikishie salamu zangu kwa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie", basi na wewe mwambie: Sema: “Ewe Allah, mfikishie swala na salamu Mtume wetu Muhammad" hapo ulipo, na malaika watafikisha salamu zako kwa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

Na hii inaonyesha wepesi wa sheria, kwani Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alipokataza kulifanya kaburi lake kuwa sehemu ya idi (yenye kutembelewa kila mara); aliwaelekeza wamswalie na kumsalimia popote walipo, na akasema kuwa salamu hizo zinamfikia, na wala hakuwawekea uzito umma wake (kwa kuwalazimisha) kufika kwenye kaburi lake kwa ajili ya kumsalimia.

❖❖❖

# Kuwasili Al-Madiinatu al-Munawwarah

## Neema ya kufika Al-Madiinatu al-Munawwarah

Madina ni mji uliobarikiwa, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie aliuombea baraka ndani yake na katika chakula chake, na ni mji unaopendwa na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie, na ni haki kwa kila Muislamu kupenda kile alichokipenda Mtume swala na salamu za Allah zimshukie-; Kwa hivyo, mshukuru Allah kwa kufika kwako katika mji huu uliobarikiwa, Kwani ni Waislamu wangapi waliokufa kabla ya kutimia matakwa yao kwa kuizuru Madina. Na itumie vizuri neema ya kuwasili kwako Madina, utoke humo ukiwa katika hali bora; kuwa na msimamo katika imani, tabia njema, na kukaa na watu vizuri.

# Madina Kabla ya Uislamu

Watu wa kwanza waliojulikana kuishi Madina walikuwa “Al-'Amaaliqah”, ambao walikuwa miongoni mwa Waarabu. Kisha wakaja Mayahudi walipopata shida na madhara katika mji wa Shaam na ilipoharibiwa Baitul-Maqdis, wakauchagua mji wa Madina wakati wanachuoni wao walipoona katika Taurati maelezo ya (kuja kwa) mtume ambaye Madina itakua mahamio yake:

﴿وَكَانُوا۟ مِن قَبْلُ يَسْتَفْتِحُونَ عَلَى ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ فَلَمَّا جَآءَهُم مَّا عَرَفُوا۟ كَفَرُوا۟ بِهِۦ﴾

«Walikuwa wakitafutia ushindi kuwashinda makafiri, (lakini) yalipowajia yale waliyo kuwa wakiyajua waliyakanusha». [Al-Baqarah: 89].

Na miongoni mwa Mayahudi mashuhuri waliokaa Madina ni: Banuu Quraydhwah, Banuu an-Nadhwiir, na Banuu Qaynuqaa’. Hivyo, Mayahudi wakabaki kuwa wengi mpaka walipokuja Al-Aws na Al-Khazraj. Basi walipokaa wakawekeana mkataba wa amani na ujirani pamoja na Mayahudi. Wakawa na mali na silaha, Mayahudi walipoona hali yao, wakawaogopa na wakavunja ahadi nao. Lakini hali ikaendelea kubadilika na kuwawezesha al-Aws na al-Khazraj kupata nguvu katika Madina.

Kulikuwa na upendo na udugu kati ya [kabila la] Aws na Khazraj mwanzoni. Kisha kukatokea utengano na uhasama kati yao. Kukazuka vita vikubwa baina yao, vilivyo mashuhuri zaidi na vya mwisho vilikuwa ni vita vya Siku ya Bu'ath. Aisha Allah amridhie alisema: Siku ya Bu'ath ilikuwa siku ambayo ni heri Allah alimletea na kumtangulizia Mtume wake swala na salamu za Allah zimshukie, basi Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie akaja (Madina) wakati tayari umoja wao umetawanyika na viongozi wao wameuawa na kujeruhiwa. Allah akamtangulizia Mtume wake swala na salamu za Allah zimshukie [heri hii] katika

kuingia kwao katika Uislamu[1]. Imepokewa na Al-Bukhari.

Kisha Mtume swala na salamu za Allah zimshukie akafika Madina, na Allah akaziunganisha nyoyo zao. Amesema Allah aliyetakasika:

﴿وَٱذۡكُرُواْ نِعۡمَتَ ٱللَّهِ عَلَيۡكُمۡ إِذۡ كُنتُمۡ أَعۡدَآءٗ فَأَلَّفَ بَيۡنَ قُلُوبِكُمۡ فَأَصۡبَحۡتُم بِنِعۡمَتِهِۦٓ إِخۡوَٰنٗا﴾

«Na kumbukeni neema ya Allah juu yenu, wakati mlikuwa maadui (nyinyi kwa nyinyi, Allah) akaweka maridhiano kati ya nyoyo zenu, basi kwa neema yake mkawa ndugu» [Aali-Imraan: 103]. Kisha Uislamu ulienea kutoka hapo [2].

---

1 Kwa maana siku hii ilikuwa ni heri kwa Mtume na kwa Waisilamu; kwa sababu watu wa Madina miongoni mwa Aws na Khazraj walihisi kuuhitajia kwao Uisilamu; ili kuzuia damu zao kumwagika, na kwa sababu lau viongozi wao wangekuwa hai wangelifanya kiburi kumfuata Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, na kupenda kwao uongozi kungewazuia kukubali kuingiliwa na kiongozi mwengine, basi vita hivyo vikawa ni utangulizi wa heri.

2 Tafsir ibnu Jariir 5/650, ad-Durratu ath-Thamiinah uk 57, Wafaau al-Wafaa 1/156.

# Majina ya Madina

Nabii swala na salamu za Allah zimshukie aligura kwenda Madina. Na kutokea Madina Allah aliifungua Makkah na miji mingine, na kutokea Madina Uislamu ulienea sehemu nyingine ulimwenguni. Kwa sababu ya utukufu wa Madina, majina yake yamekuwa mengi. Amesema an-Nawawi Allah amrehemu: «Hatujui mji wowote wenye majina mengi kuliko Makkah na Madina; kwa sababu ndio sehemu bora zaidi kwenye ardhi»[1].

Miongoni mwa majina yake:

**1) Madina;** Na jina hili ndilo maarufu zaidi katika majina yake, na ndilo jina linaloitiwa nalo, Amesema Nabii swala na salamu za Allah zimshukie: «**Niliamrishwa (kugura) kwenda kijiji kinachoshinda vijiji vingine, wanaiita: Yathrib, nayo ni Madina**». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea. Katika Qur-ani limekuja jina hili katika aya nne, amesema Ibnu Hajar Allah amrehemu: «[Jina Madina] limetajwa huru bila kikwazo, inakuja haraka akilini kwamba ndio (mji wa Madina) unaokusudiwa, na unapokusudiwa mji mwingine kwa tamko la Madina, basi hapana budi kuwe na kikwazo [cha kubainisha makusudio]»[2].

**2) Twayba**; Amesema Fatwima binti Qays Allah amridhie: «Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alisema akiwa anagonga mimbari kwa fimbo yake: «**Hii ni Twayba, hii ni Twayba, hii ni Twayba**». Imepokewa na Muslim.

**3) Twaaba**; Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Hakika Allah aliyetukuka aliita Madina "Twaaba"**». imepokewa na Muslim, na alisema Jabir ibnu Samurah Allah amridhie: «Nilimsikia Mtume swala na salamu za Allah zimshukie

1 Tahdhiib al-Asmaa wal-Lughaat, 4/157.

2 Fat-hul Baari, 4/81.

akiita Madina “Twaaba”» imepokewa na Ahmad. An-Nawawi Allah amrehemu alisema: «Na uliitwa “Twayba” na “Twaaba” kwa sababu ya uzuri wa matamshi hayo, na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie anapenda jina zuri na anachukia jina baya»[1].

1 Sharhu Swahiih Muslim, 9/154.

# Jina ambalo Mtume swala na salamu zimshukie alichukia iitwe kwalo Madina

Kabla ya Mtume swala na salamu za Allah zimshukie kuja Madina, ilikuwa ikiitwa “Yathrib”. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alipofika, hakupenda kuuita (mji huo) kwa jina hilo; akasema: «**…Wanasema: Yathrib, nao ni Madina**». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea. Na Sababu ya kulichukia jina hili ni kwamba limetokana na neno “Tharab” linalomaanisha uharibifu, au kutokana na neno “Tathriib”, ambayo ni kukemea na kulaumu. Na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akipenda majina mazuri, na akibadilisha jina baya na kulipatia jina zuri.

Na kuitwa Madina katika Qur-ani kwa jina la “Yathrib”; ilikuwa ni kuhadithia tu kuhusu kauli ya wanafiki na wale ambao nyoyo zao zina ugonjwa, kama ilivyokuja katika kauli yake Allah aliyetukuka:

﴿وَإِذْ قَالَت طَّآئِفَةٌ مِّنْهُمْ يَٰٓأَهْلَ يَثْرِبَ لَا مُقَامَ لَكُمْ فَٱرْجِعُوا۟﴾

«Na wakati kundi lao liliposema: “Enyi watu wa Yathrib! Hakuna mahali pa kukaa; kwa hivyo rudini!”» [Al-Ahzaab: 13].

Na kauli ya Mtume swala na salamu za Allah zimshukie kuhusu Madina: «**Akili yangu ikaenda kufikiria kuwa ni Al-Yamamah au Hajar, kumbe ikawa ni mji wa Yathrib**» Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea, na kauli yake: «**Siidhanii isipokuwa ni Yathrib**» Imepokewa na Muslim, Kwa hivyo, hii ilikuwa kabla ya makatazo ya kuuita mji huo “Yathrib”.

## Kwa nini Mtume swala na salamu zimshukie aliondoka Makkah na kuhamia Madina?

Makkah Tukufu ni mji wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, na mji wa mababa zake tangu baba yake Ibrahim kipenzi cha Allah salamu zimshukie. Alizaliwa huko, na wahyi wa kwanza ulikuja kwake akiwa huko, na alipowaita watu wake katika Tauhidi, walimuudhii na kumkejeli, na wakamzingira katika bonde, na wakaazimia kumuua, kama Allah Mtukufu alivyosema:

﴿وَإِذۡ يَمۡكُرُ بِكَ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ لِيُثۡبِتُوكَ أَوۡ يَقۡتُلُوكَ أَوۡ يُخۡرِجُوكَۚ وَيَمۡكُرُونَ
وَيَمۡكُرُ ٱللَّهُۖ وَٱللَّهُ خَيۡرُ ٱلۡمَٰكِرِينَ﴾

«Na (kumbuka) pindi walipokufanyia njama waliokufuru wakufunge au wakuue au wakutoe, na walipanga na Allah alipanga, na Allah ndiye Mbora wa wapangaji» [Al-Anfaal: 30].

Lakini alipozidi kuudhiwa, na wakamzuia kufikisha ujumbe wa Mola wake, Allah akamruhusu kuhamia Madina ili kueneza dini katika maeneo mbalimbali, watu wapate kuingia katika Uislamu.

## Je kuna dua maalumu ya kuingia Madina?

Hapana, hakuna dua maalumu ya kuingia Madina. Hata hivyo, kuna dua ya jumla ya kuingia mji wowote, sawa iwe ni Madina au kwengine. Amesema Suhaib Allah amridhie: «Mtume swala na salamu za Allah zimshukie hakuwa akiona kijiji chochote anachotaka kuingia, isipokuwa akisema wakati anapokiona: **"*Allahumma Rabbas-samaawaatis- sab'i wa maa adhlalna, Wa Rabbal-aradhwiinas- sab'i wa maa aqlalna, wa Rabbash-shayaatwiini wa maa adhwlalna, wa Rabbar-riyaaḥi wa maa dharayna. As-aluka khayra haadhihil-qaryah, wa khayra ahlihaa, wa khayra maafiihaa, wa a`uudhu bika min sharrihaa, wa sharri ahlihaa, wa sharri maa fiihaa.* /Ewe Allah, Mola wa mbingu saba na kile kilichochini ya kivuli chake, na Mola wa ardhi saba na kile kilichobebwa juu yake, na Mola wa mashetani na kile wanachopotosha, na Mola wa upepo na kile kinachotawanya, basi hakika tunakuomba kheri ya kijiji hiki na kheri ya watu wake, na tunajikinga kwako na shari yake na shari ya watu wake na shari iliyomo ndani yake/"**». Imepokewa na An-Nasaai.

Na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amesema: «**Yeyote atakayeshukia mahali, kisha akasema: "*A'uudhu bikalimaatil-laahi at-taammaati min sharri maa Khalaq* /Najikinga kwa maneno ya Allah yaliyokamilika kutokana na shari ya kile alichokiumba/", - hakuna kitu kitakachomdhuru mpaka atakapoondoka kwenye makazi yake hayo**». Imepokewa na Muslim.

## Adabu za mwenye kuzuru Madina

Allah amemfadhili mwenye kuzuru Madina kwa kumwezesha kuzuru mji uliobarikiwa, na mwenye kuzuru mji huu analazimika kufuata adabu kadhaa, miongoni mwazo:

1) Kukumbuka kwamba Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alikuja (kuamrisha watu) na Tauhidi (kumpwekesha Allah) na kumwomba Yeye peke yake. Kwa hivyo, ni wajibu kwake (aliyekuja ziara) kufuata mwito wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, wala asimwombe yeyote isipokuwa Allah na afikishe mahitaji yake kwake yeye peke yake, Allah mtukufu amesema:

﴿وَإِن يَمْسَسْكَ ٱللَّهُ بِضُرٍّ فَلَا كَاشِفَ لَهُۥٓ إِلَّا هُوَ﴾

«Na ikiwa Allah atakufikishia madhara, basi hakuna wa kukuondolea (madhara hayo) ila Yeye» [Yunus: 107].

2) Akumbuke kwamba Madina ni mji ulio bora, hivyo basi atumie vizuri muda wake wote ndani ya Madina katika mambo ya utiifu (kwa Allah), kama vile kuswali katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, kusoma Qur-ani, kumtaja Allah, na mengineo.

3) Aepuke kuingia katika uzushi na maasia. Hakika, yule anayeasi katika mahali patukufu ni mbaya zaidi kuliko yule anayeasi katika sehemu zingine.

4) Akae na watu wa Madina kwa tabia njema na adabu nzuri. Hakika, maandiko yamekuja na onyo kwa yule anayewadhuru watu wake. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Yeyote anayekusudia kuwadhuru watu wake, Allah atamyeyusha kama chumvi inavyoyeyuka ndani ya maji**». Imepokewa na Muslim.

# Ratiba ya Aliyezuru Madina

**Kabla ya Alfajiri:**

Unaamka saa moja kabla ya alfajiri kwa ajili ya swala ya usiku, unaswali rakaa mbili kisha unapiga salamu, kisha unaswali rakaa mbili kisha unapiga salamu, na ikiwa utaongeza zaidi, unaruhusiwa kufanya hivyo. Na ikiwa adhana ya alfajiri inakaribia, utaswali rakaa moja ya Witri.

Swala za sunna nyumbani ni bora kuliko swala katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie; kwa sababu Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa anaswali sunna nyumbani na Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie ulikuwa karibu naye, na alisema: «**Hakika swala bora ya mtu ni nyumbani mwake isipokuwa swala za faradhi**». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

Na itakapoadhiniwa Alfajiri, utakwenda kwenye Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie kwa ajili ya kuswali Alfajiri ndani yake.

**Baada ya Alfajiri:**

Unakaa katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie kwa ajili ya kusoma Qur-ani Tukufu, na kumdhukuru Allah - miongoni mwa tasbihi [kusema: Sub-haana llaah], tahmidi [kusema: Al-Hamdu lillaahi], tahlili [kesema: Laa ilaaha illa Allah], na takbiri [kusema: Allahu akbar] - hadi jua lichomoza.

**Baada ya Alasiri:**

Unajiunga na vikao vyao kusoma Qur-ani Tukufu katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie ili kusahihisha kisomo chako cha Qur-ani.

**Baada ya Magharibi:**

Unahudhuria masomo ya wanachuoni katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, na unauliza kuhusu mambo ya dini.

**Baada ya Ishaa:**

Unaenda kwenye makazi, na unalala mapema kujiandaa kwa ajili ya swala ya witr na alfajiri.

❖❖❖

# Fadhila za Mji wa Mtume

# Fadhila za Madina

Madina ya Mtume swala na salamu za Allah zimshukie ina cheo na hadhi ya juu, Allah ameitukuza na kuifadhilisha, na kuifanya kuwa sehemu bora baada ya Makkah, kwani ni nyumba ya wahyi, na mahali pa kushuka kwa Malaika kwa uongofu na rehema, na kila kheri iliyowafika watu wa ardhi basi ilitoka katika mji huu uliobarikiwa, kama ilivyotokea katika zama za Mtume swala na salamu za Allah zimshukie na masahaba, na kufadhilishwa kwa Madina ni kwa sababu ya kuwa Allah ameichagua kwa kuwepo ndani yake alama za dini, na miongoni mwa mambo yaliyochaguliwa na Allah kuwepo Madina pekee ni kama yafuatavyo:

## ❋ Kwanza: Fadhila za kiimani:

**na zinawakilishwa na yafuatayo:**

**1) Mapenzi ya Mtume swala na salamu za Allah zimshukie kwake:**

Mtume swala na salamu za Allah zimshukie aliupenda mji wake wa Makkah upendo mkubwa, kama alivyosema kuhusu Makkah: «**Wewe ni mji mzuri ulioje na unapendekeza zaidi kwangu, na lau kama watu wangu hawakunitoa kwako nisingeishi sehemu nyingine isiokuwa wewe**». Imepokewa na At-Tirmidhi.

Kisha akahama kutoka Makkah kwenda Madina na akamuomba Mola wake ampendekezee Madina kama alivyoipenda Makkah au zaidi; hivyo alikuwa akisema: «**Ewe Mola wangu, tujaalie tuipende Madina kama ulivyotufanya kuipenda Makkah au zaidi**». Imepokewa na Al-Bukhari. Na Allah aliikubali dua yake, akaipenda Madina sana, akawa anaposafiri kuondoka Madina, kisha [wakati wa kurudi] anapoona nyumba zake [Madina], basi alikuwa akiharakisha mwendo kuifikia Madina kwa ajili ya anavyoipenda. Anas Allah amridhie

alisema: «Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa anapotoka safari na kuona kuta za Madina, alikuwa akiharakisha mwendo wa ngamia wake, na ikiwa yuko juu ya mnyama mwengine wa kupanda, alikimpeleka haraka kwa sababu ya mapenzi yake kwa Madina». Imepokewa na Al-Bukhari. Amesema Ibnu Hajar Allah amrehemu: «Na kila muumini ana kitu moyoni kinachomsukuma kwenda Madina kutokana na mapenzi yake kwa Mtume swala na salamu zimshukie»[1].

**2) Kuongezeka kwa thawabu za swala katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie:**

Miongoni mwa fadhila za Madina ni kwamba swala katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie ni bora kuliko swala elfu moja katika misikiti mingine, isipokuwa Al-Masjidul-Haraam.

**3) Imani hurudi Madina:**

Allah aliichagua Madina kuwa makao ya imani, mwanzoni na mwishoni, kwani katika mwanzo wa Uislamu, Madina ilikuwa makao ya imani. Alisema Allah Mtukufu:

﴿وَٱلَّذِينَ تَبَوَّءُو ٱلدَّارَ وَٱلۡإِيمَٰنَ﴾

«Na wale walioishi nyumba [ya kuguria Mtume] na wakawa na Imani…» [Al-Hashr: 9].

Na imani itarudi Madina kama ilivyoanza humo. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Hakika imani itarudi Madina, kama nyoka anavyorudi kwenye shimo lake.** (Yaani: Kama nyoka anavyorudi kwenye shimo lake akiogopeshwa na kitu, kisha anatoka nje baada ya kujisikia na amani)». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

1 Fat-hul-Baari, 4/93.

**4) Unakula miji:**

Mtume alielezea kuwa Madina ni mji unaokula miji mingine, akasema: «**Niliamrishwa kuguria mji unaokula miji, wanauita: Yathrib, nao ni Madina**». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

Maana ya «**…unaokula miji**» Yaani: utashinda miji mingine.

Na kumesemwa: Maana yake ni kuwa utakuja kuleta ghanima (ngawira).

Na mawili haya, ni yenye kuambatana na yametokea, kwani limetokea mji huu kushinda miji mingine; kukatoka ndani yake walinganizi na wapiganaji waliokwenda kufungua miji, wakatoa watu gizani hadi katika nuru kwa idhini ya Mola wao, alisema Ibnu Abdul-Barr Allah amrehemu: «Kutokea Madina, miji yote ilipata kufunguliwa»[1].

Na vilevile pia, lilitokea la kupatikana ngawira, zikaletwa hadi Madina kama hazina za Kisra na Kaisar, na Umar bin al-Khattwaab Allah amridhie akazigawanya.

1 At-Tamhid, 23/170.

## ❋ Pili: Kuwa ni mji mzuri:

Kama vile ni mji wa imani, pia ni mzuri unaofukuza uovu na watu wake, na hii inajidhihirisha katika yafuatayo:

**1) Unafuta dhambi:**

Allah ameifanya Medina kuwa mji unaofuta dhambi - yaani, unayafuta; ima yale yanayompata mtu miongoni mwa mitihani yanayompata mja ndani yake, au kwa ajili ya fadhila yake, Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Hakika huo ni Twayba (Madina); huondoa dhambi, kama vile moto unavyoondoa uchafu wa fedha -yaani, uchafu wake na ile ilio mbaya-**». Imepokewa na Al-Bukhari.

**2) Inaondoa watu waovu:**

Allah aliifanya Madina kuwa nzuri, na yeyote atakayekuwa mbaya basi Madina inamfukuza na kumuondoa ndani yake, Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Inaondoa watu -yaani, wabaya wao-, kama vile mvukuto unavyoondoa uchafu wa chuma**». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea, na katika riwaya ya Muslim: «**…Inamtoa aliye muovu…**».

Na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie aliifananisha na mvukuto kwa nguvu yake ya kuondoa uchafu; akasema: «**Madina ni kama mvukuto inayoondoa uchafu wake, na uzuri wake unaangaza**». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

**3) Uzuri wake unazidi kuangaza:**

Mwenye kuikaa Madina, akiwa na imani na wema, jina lake na kazi yake zinazidi kuangaza, kama Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alivyosema: «**…Na uzuri wake unaangaza**». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea. Al-Nawawi Allah amrehemu alisema: «Yaani, unazidi kuwa maridadi, safi

uliotakata na wenye uzuri wa kipekee»[1].

Vilevile kama wanazuoni na watu wema wanakuwa wazuri humo, vivyo hivyo matendo mema ndani yake yanazidi kung'aa na kuonekana na watu.

1 Sharhu Swahiih Muslim, 9/156.

## ❋ Tatu: Kuwepo amani ndani yake:

Hii inajidhihirisha katika mambo yafuatayo:

**1) Kuwa wenyewe ni mji wa amani:**

Allah aliifanya Madina kuwa mji wa amani; ili ibada za Uislamu zifanyike ndani yake, na dini ienee kutoka humo. Amesema Sahal ibnu Hunaif Allah amridhie: «Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie alielekeza mkono wake kuelekea Madina, kisha akasema: «**Hakika ni mji mtukufu wenye amani**». Imepokewa na Muslim, na amani ndani yake inaonekana katika mambo kadhaa:

a) Yeyote atakayeukusudia mji wa Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie kwa ubaya, Allah atamuangamiza, amesema Nabii swala na salamu za Allah zimshukie: «**Yeyote atakayeukusudia kwa ubaya; Allah atamyeyusha, kama vile chumvi inavyoyeyuka ndani ya maji**». Imepokewa na Ahmad.

b) Yeyote atakayewatishia wakazi wake, basi Allah atamtishia na kumuahidi laana, amesema Nabii swala na salamu za Allah zimshukie: «**Yeyote atakayewatia hofu watu wa Madina hali ya kuwa anawadhulumu; Allah atamtia hofu, na atapata laana ya Allah, malaika na watu wote, haikubaliwi kutoka kwake faradhi yoyote, wala sunna**». Imepokewa na An-Nasaai.

c) Yeyote atakayewapangia njama watu wa Madina na kuwafanyia vitimbi vibaya, Allah atamuangamiza duniani na hatamwachilia, amesema Nabii swala na salamu za Allah zimshukie: «**Hakuna anayewapangia njama watu wa Madina, isipokuwa (mtu huyo) atayeyuka kama chumvi inavyoyeyuka ndani ya maji**». Imepokewa na Al-Bukhari.

d) Yeyote atakayewakusudia watu wake kwa ubaya, basi Allah amemuandalia akhera adhabu kali katika moto, amesema Nabii swala na salamu za Allah zimshukie: «**Hakuna**

**anayewakusudia watu wa Madina kwa ubaya; isipokuwa Allah atamyeyusha motoni kama vile risasi inavyoyeyuka, au chumvi inavyoyeyuka ndani ya maji**». Imepokewa na Muslim.

**2) Madina ni "Haram":**

Allah amefanya Makkah na Madina kuwa "Haram", na maana ya hizo sehemu mbili kuwa "Haram" ni kuwa kuna mambo ya halali ambayo yanaruhusiwa kufanywa katika nchi nyingine, lakini katika Makkah na Madina ni haramu kufanywa. Au pengine mambo hayo ni haramu katika nchi nyingine, lakini katika Makkah na Madina ni haramu zaidi.

Na hakuna "Haram" nyingine katika ardhi isipokuwa Makkah na Madina, kwa hivyo hakusemwi Msikiti wa al-Aqsa: "ya tatu katika Haram mbili", kwa sababu huo si "Haram".

Na Sababu ya kuharamishwa baadhi ya mambo katika Makkah na Madina ni kwa sababu ya cheo yake kwa Allah, kwani Ibrahim salamu zimshukie aliiharamisha Makkah na Mtume wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie aliiharamisha Madina, amesema Mtume swala na salamu za Allah zimshukie: «**Hakika Ibrahim aliiharamisha Makkah, na mimi nimeiharamisha Madina**». Imepokewa na Muslim.

Mipaka ya Haram ya Madina ni kama ifuatavyo:

* Kaskazini: Mlima Thaur, na kusini: Mlima A'yr, amesema Mtume swala na salamu za Allah zimshukie: «**Madina ni "Haram" inayoanzia A'yr hadi Thaur**». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

* Mashariki na magharibi: sehemu za lava[1] mbili, amesema Mtume swala na salamu za Allah zimshukie: «**…Nimeharamisha Madina ilioko baina ya lava zake mbilie**». Imepokewa na Muslim.

---

1 Lava: Miamba iliyoyeyushwa inayotoka kwenye volcano au mpasuko kwenye uso wa sayari (kama vile dunia), pia: Mwamba kama huo ambao umepoa na kuwa mgumu.

**Na hukumu zinazoambatana na kuwa Madina ni Haram ni hizi zifuatazo:**

a) Mauaji bila haki ni haramu kila mahali na kila wakati, lakini katika mji wa Madina ni haramu zaidi kuliko kwengine. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amesema: «**…Hakumwagwi damu ndani yake (Madina)…**». Imepokewa na Muslim.

b) Hakubebwi silaha kwa ajili ya kupigana. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amesema: «**…Hakubebwi silaha kwa ajili ya kupigana ndani yake…**». Imepokewa na Muslim.

c) Hairuhusiwi kuwinda wanyama wake, kwa mfano njiwa. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amesema: «**…wala hakuwindwi wanyama wake wa pori**». Imepokewa na Muslim. Na maana ya neno "swayd" ni mnyama wa porini anayeliwa, aliye wa mwitu kwa asili yake. Yaani: ambaye hakai na binadamu; badala yake, anamkimbia.

d) Haukatwi mti wake. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amesema: «**…Haukatwi mti wake wa miba**». Neno "i'dhwaauhaa" linamaanisha kila mti wenye miba. Imepokewa na Muslim. Miti ambayo ni haramu kuyakata ni ile iliyoota yenyewe, lakini miti iliyopandwa na watu, basi wanaweza kuikata.

e) Hakutingiswi mti wowote katika Madina kwa ajili ya kuangusha majani yake, isipokuwa kwa ajili ya chakula cha mifugo. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amesema: «**…na miti yake isipigwe (kwa ajili ya kuangusha majani), isipokuwa ikiwa ni kwa ajili ya chakula cha mifugo…**». Imepokewa na Muslim.

f) Kumeharamishwa kuanzisha uzushi ndani yake, na kumuweka mzushi au mhalifu ndani yake. Vitendo hivi viwili ni haramu katika maeneo mengine yote, lakini katika Madina makatazo yake ni zaidi. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amesema: «**Yeyote atakayezusha uzushi wowote katika Madina, au akamhifadhi mzushi, basi laana ya Allah,**

**Malaika na watu wote iwe juu yake. Haikubaliwi kutoka kwake sunna wala faradhi**». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

**3) Allah ameihifadhi Madina kutokana na Dajali na vitisho vyake:**

Katika mwisho wa zama, Masihi Dajali atatoka, na atatembea katika miji, akidai kuwa yeye ni Mola wa viumbe wote. Basi makafiri watamwamini kwa sababu ya mambo ya ajabu ambayo Allah atampa na kumtuma nayo.

Na watu watakaposikia habari zake, watamwogopa na kukimbia majabalini, isipokuwa Madina, kwani hofu yake haiingii humo. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amesema: «**Hofu ya Masihi Dajali haiingii Madina**». Imepokewa na Al-Bukhari.

Miongoni mwa mambo ambayo Allah ameyahifadhi nayo Madina: ni kwamba amemharamishia Dajali kuingia humo. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amesema: «**…Dajali atakuja, na ni haramu kwake kuingia milango ya Madina**». Imepokewa na Al-Bukhari.

Dajali atajaribu kuingia Madina mara kwa mara, lakini Allah anailinda kwa Malaika wenye panga ambao wanamzuia. Hakika imekuja katika hadithi inayoelezea kuhusu Dajali, kuwa amesema: «**…Hakika yangu niko karibu kupewa ruhusa ya kutoka, nami nitatoka, nitembee katika ardhi, na wala sitaacha kijiji chochote isipokuwa nitakitembelea katika (mda wa) siku arobaini, isipokuwa Makkah na Madina, kwani zote mbili zimeharamishwa kwangu. Kila ninapotaka kuingia mojawapo kati ya hizo mbili, Malaika mwenye upanga mkali ananipokea ananizuia nisiweze kuingia…**» Imepokewa na Muslim.

**4) Ugonjwa wa Tauni hauingii ndani yake:**

Allah ameulinda Mji wa Madina kutokana na ugonjwa wa Tauni, ambao ni ugonjwa wa kuambukiza sana unaosababisha kifo. Allah aliweka Malaika kwenye kila njia ya kuingia Madina ili wazuie ugonjwa wa Tauni kuingia ndani yake. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amesema: «**…Kwenye njia za kuingia Madina kuna Malaika ambao hawataruhusu Tauni**

**wala Dajali kuingia**». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

**5) Malaika wanaulinda:**

Mojawapo wa mambo yanayoonyesha kuwepo amani katika Madina ni kwamba Allah amewaeka Malaika kuulinda kutokana na Dajali, kwa hivyo njia zake zote zimehifadhiwa na Malaika kutokana na Dajali. Amesema Nabii swala na salamu za Allah zimshukie: «**… Kwenye njia za kuingia Madina kuna Malaika ambao wanaulinda…**». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

Bali Madina imezungukwa na Malaika kutoka pande zote. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amesema: «**…Dajali atakuja Madina, atakuta Malaika wanailinda…**». imepokewa na Al-Bukhari. Imam An-Nawawi Allah amrehemu amesema: «hii inaonyesha wingi wa walinzi na kwamba wanaenea katika maeneo yote ya Madina»[1].

**6) Madina hakuna magonjwa ya mlipuko:**

Mji wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie ulikuwa na mabonde na magonjwa yalikuwa yakizidi ndani yake. Na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alipogura yeye na masahaba zake kwenda Madina, walipata homa. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie akaomba kwamba Madina isiwe na ugonjwa wa mlipuko, akasema: «**Ewe Allah, tufanyie Madina kuwa ya afya**» Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea. Ibnu Hajar Allah amrehemu amesema: «Hivyo, Madina ilirudi kuwa mji wenye afya zaidi katika miji ya Allah, ambapo kabla ya hapo ilikuwa tofauti»[2].

1 Sharhu Swahiih Muslim, 9/148.

2 Fat-hul Baari, 10/191.

## ❋ Nne: Utukufu wa kuishi Madina

Miongoni mwa fadhila za Madina ni utukufu wa kuishi humo. Hii inajidhihirisha katika mambo yafuatayo:

**1) Fadhila ya kuishi Madina:**

Madina ni mji uliobarikiwa, na kuishi humo ni bora zaidi kuliko kuishi mahali pengine, hata kama mahali pengine kuna maisha mazuri zaidi. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alipendekeza watu kukaa Madina kwa kusema: «**Itawajia watu wakati ambapo mtu atamwita binamu yake na jamaa yake wa karibu: "Njoo kwenye maisha ya raha, njoo kwenye maisha ya raha", (lakini) Madina ni bora kwao lau wangejua!**» Imepokewa na Muslim.

Mtu yeyote atakayeishi Madina akiwa na imani na wema, Allah atadhihirisha uzuri wake katika sehemu za mbali. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**…Na uzuri wake unang'aa**». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

Na yeyote atakayeiacha Madina hali ya kuwa anaichukia, Allah atamleta badala yake mtu bora kuliko yeye. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Hakuna yeyote atakayeiacha kwa sababu ya kuichukia isipokuwa Allah atamleta badala yake aliye bora kuliko yeye**». Imepokewa na Muslim.

Lakini ikiwa faida ya Muislamu nje ya Madina ni yenye kuenea, kwa mfano mwenye kutoka Madina kwa ajili ya kulingania dini, au mfano wake, basi hakuna ubaya kwake kuondoka Madina, kwani Mtume swala na salamu za Allah zimshukie aliwatuma baadhi ya masahaba wake, kama vile Ali ibnu Abi Twaalib, Muadh ibnu Jabal, Abu Musa Al-Ash'ariyyu, na wengineo, aliwatuma nje ya Madina kwa ajili ya kulingania dini ya Allah.

Na sehemu ambayo mtu atakuwa mchaji Allah zaidi ndani yake basi hapo kwake yeye ndio itakua bora. Amesema Sheikhul Islaam Ibnu Taymiyyah Allah amrehemu: «Kukaa katika kila

mahali ambapo sababu ndani yake zinaruhusu zaidi utiifu kwa Allah na Mtume wake, kufanya kheri na matendo mema, kwa njia ambayo yeye mwenyewe anaifahamu zaidi, ana uwezo zaidi nayo, na ana uchangamfu zaidi, ni bora kuliko kukaa katika mahali ambapo hali yake ya utiifu kwa Allah na Mtume wake itakuwa chini ya hapo»[1].

**2) Kuvumilia shida zake ni sababu ya kupata maombezi au ushahidi wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie:**

Maisha ni magumu na majaribio yake ni ya mara kwa mara, na Allah ametuamuru tuvumilie misiba, na ameahidi kuwa pamoja na wanaovumilia na kwamba malipo yao hayatakua na kikomo.

Na Allah aliipa Madina fadhila ya pekee; kuwa mwenye kuvumilia kile anachokutana nacho ndani yake miongoni mwa shida na majaribio; hakika ameahidiwa -pamoja na kupata thawabu kubwa- maombezi au ushahidi wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie siku ya Kiyama. Abu Sa'id -mawla wa Al-Mahri[2], alimwendea Abu Sa'id Al-Khudri katika masiku ya Al-Harrah[3], na akamuomba ushauri kuhusu kuondoka Madina, Akamlalamikia bei za juu zilizopo humo na familia yake kubwa, na akamwambia kuwa hawezi kuvumilia tena ugumu wa Madina na mazingira yake magumu. Abu Sa'id Al-Khudri akamwambia: «Ole wako! Sitakushauri ufanye hivyo. Kaa Madina usiondoke, kwani nilimsikia Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie akisema: «**Hakuna yeyote atakayevumilia ugumu wa**

---

1 Fataawa Sheikhul Islaam, 27/39.

2 «Mawla» ni mtu aliyekua mtumwa akaachwa huru, kwa hivyo huitwa ni Mawla wa yule aliyemwacha huru.

3 «Al-Harrah» kwa Kiarabu ina maana "eneo la lava". Tukio hili linarejelea vita vilivyofanyika mwaka wa 63 Hijria, karibu na Madina kwenye eneo la lava, kati ya watu wa Madina na jeshi liliotumwa na Yazid ibnu Mu'awiya, Khalifa wa Bani Umayyah. Yazid alituma vikosi vyake Madina ili kukabiliana na uasi wa watu wa Madina dhidi ya utawala wake.

**maisha ya Madina, kisha afe; isipokuwa mimi nitakuwa muombezi wake au shahidi wake siku ya Kiyama ikiwa atakuwa Muislamu**». Imepokewa na Muslim.

Kwa hivyo, mtu yeyote ambaye amepata shida katika Madina, haipaswi kuhamia mahali pengine katika miji kutafuta ustawi na maisha mazuri. Badala yake, anapaswa kuvumilia kile kilichomfikia humo, na hakika ameahidiwa ujira mkubwa na thawabu nyingi kutoka kwa Allah.

## ❈ Tano: Baraka zake:

Baraka za Madina ni za aina kadhaa:

**1) Baraka ya jumla:**

Baraka haiwi katika kitu kidogo isipokuwa inakikithirisha, na wala haiwi katika kingi isipokuwa inaongeza manufaa yake. Na hakika, Mtume swala na salamu za Allah zimshukie aliomba baraka katika Madina, na hilo linajitokeza katika mambo yafuatayo:

A) Aliomba Mji wa Madina uwe wenye baraka, Mtume swala na salamu za Allah zimshukie akasema: «**Ewe Allah, tubarikie katika Mji wetu**» Imepokewa na Muslim.

B) Aliomba kuwe na baraka mbili pamoja na ile moja, akasema: «**Ewe Allah, tujaalie pamoja na baraka baraka nyingine mbili**» Imepokewa na Muslim.

C) Aliomba baraka ndani ya Madina iwe maradufu ya baraka ilio Makkah, akasema: «**Ewe Allah, ijaalie Madina iwe na baraka mara mbili ya baraka ya Makkah**» Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

**2) Baraka ya chakula chake:**

Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alikiombea baraka chakula cha Madina, na hilo lilijitokeza katika mambo yafuatayo:

A) Baraka katika pishi[1] yake na kibaba[2] chake - yaani, baraka katika chakula chake, kwani chakula kidogo kinawatosha wengi na faida yake inaongezeka, Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Ewe Allah, tubarikie katika pishi yetu, Ewe Allah, tubarikie katika kibaba chetu**» Imepokewa na Muslim. Imam An-Nawawiy Allah amrehemu alisema: «Lilio dhahiri ni kwamba baraka

(1) Pishi: Ni kipimo ambaco hutumika mkebe maalumu unaotumika kupimia nafaka au chakula, kwa kipimo cha kilogramu inakurubia 3kg.

(2) Kibaba: Ni kipimo ambacho hutumika mkebe maalumu unaolingana na robo ya pishi.

ilitokea katika kipimo chenyewe, kwani kibaba (kimoja) katika Madina kinatosha kwa kiasi ambacho hakitoshei katika sehemu nyingine, na jambo hili linaonekana kwa wale wanaoishi humo»[1].

B) Baraka katika matunda yake, Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Ewe Allah, tubarikie katika matunda yetu**» Imepokewa na Muslim. Kwa hivyo, matunda ya Madina na mazao ya mimea yake ni yenye baraka.

1 Sharhu Swahiih Muslim, 9/142.

## ❋ Sita: Tende zake:

Kwa ajili ya cheo cha Madina, Allah alizifadhilisha tende zake kuliko tende za miji mingine. Na tende za Madina, kuna baadhi ni bora kuliko nyingine, nazo ni daraja tatu:

**Daraja ya kwanza:** Tende za “Ajwaat al-Aaliyah”, ambazo ndio tende bora zaidi.

Mahali pake: al-Aaliyah - sehemu hii ni ardhi ilioko kusini mashariki mwa Msikiti wa Mtume, na umbali wake kutoka Al-Masjidun-Nabawi ni takriban kilomita tano, sehemu hii ipo karibu na Msikiti wa Quba.

Fadhila yake: Ni dawa ya magonjwa -kwa idhini ya Allah-, kama vile asali, mbegu nyeusi na maji ya Zamzam ni dawa.

Njia ya matumizi yake: Zinaliwa asubuhi kabla kutia chochote tumboni, bila kuwa na idadi maalumu, yaani, mtu anaweza kula tende moja au zaidi.

Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amesema: «**Hakika mna dawa katika tende za al-Aaliyah, au tende hizo ni Tiryaaq** -yaani, ni dawa ya sumu- **(zikiliwa) asubuhi ya mapema** -yaani, huliwa asubuhi tumbo likiwa tupu-». Imepokewa na Muslim.

**Daraja ya pili:** Tende za Madina kwa ujumla.

Fadhila yake: Zinazuia sumu na uchawi -kwa idhini ya Allah-

Njia ya matumizi yake: Zinaliwa tende saba asubuhi kabla kutia chochote tumboni.

Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amesema: «**Mwenye kula tende saba za Ajwaa kila siku asubuhi haitamudhuru sumu wala uchawi katika siku hio**». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

**Daraja ya Tatu:** Aina yoyote ya Tende za Madina.

Fadhila yake: Zinazuia sumu - kwa idhini ya Allah-.

Njia ya matumizi yake: Zinaliwa tende saba asubuhi kabla ya kutia chochote tumboni. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amesema: «**Mwenye kula tende saba (katika tende za Madina) zilizo baina ya maeneo ya lava mbili, haitamudhuru sumu yoyote hadi jioni**». Imepokewa na Muslim.

## ❋ Saba: Sehemu mashuhuri zilizoko ndani yake:

1 - **Msikiti wa Mtume:** itakuja kuelezewa mbele.
2 - **Msikiti wa Quba.** itakuja kuelezewa mbele.
3 - **Mlima wa Uhud.**

Mlima wa Uhud uko kaskazini mwa Msikiti wa Mtume, na uliitwa Uhud kwa sababu ya upweke wake kati ya milima mingine, kwani haukuungana na milima mingine. Na ndio mlima ambao vita vya Uhud vilifanyika hapo. Na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alisema kwamba Waislamu wanaupenda Mlima wa Uhud na Mlima wa Uhud unawapenda wao. Anas Allah amridhie alisema: Mlima wa Uhud ulidhihirika kwa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, kisha akasema: **“Huu ni mlima unaotupenda, na sisi tunaupenda”**». Imepokewa na Muslim. An-Nawawi amesema: «Na (kauli) ilio sahihi ni kwamba: maana yake ni hio ya dhahiri, na kwamba inamaanisha: Mlima wenyewe unatupenda, na Allah ameujaalia kuwa na uwezo wa kupambanua»[1]. Na kuupenda Mlima wa Uhud ni kwa moyo tu bila kuamini kuwepo baraka ndani yake, au kujisugua na mawe yake.

Na haijathibiti kuwa ni miongoni mwa milima ya Peponi.

4 - **Bonde la Aqiiq.**

Ni bonde linaloenea kutoka kusini mwa Madina hadi kaskazini mwake, na juu yake kuna miqat ya Dhul-Hulayfa. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alitangaza kwamba bonde hili ni bonde lililobarikiwa. Umar Allah amridhie alisema: Nilimsikia Mtume swala na salamu za Allah zimshukie -huko Bonde la Aqiiq- akisema: **“Usiku huu, amenijia kutoka kwa Mola wangu mwenye kunijia -naye ni Jibril salamu zimshukie-, akasema: Swali katika bonde hili lililobarikiwa, na useme: *Umra iwe ndani ya Hija*”**». Imepokewa na Al-Bukhari.

1 Sharhu Swahiih Muslim, 9/163.

Na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie aliwahi kulala katika bonde hili alipotoka Madina akielekea Hija. Ibnu Umar Allah amridhie amesema: «Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alionyeshwa -yaani katika ndoto- alipofika katika Bonde la Aqiiq mwishoni wa usiku kutoka Dhul-Hulayfa katikati ya bonde, akaambiwa: "Hakika wewe uko kwenye Bat-haau ililobarikiwa". Bat-haau: ni eneo pana la mteremko wa bonde, na kuna mawe madogo ndani yake». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

Wala haifai kutabaruku kwa mchanga wake, au vijiwe vyake, au vinginevyo; kwa sababu baraka yatoka kwa Allah pekee - Yeye ndiye Mwenye kutoa baraka, na kutoka kwake kunatarajiwa kupata baraka, na pia kwa sababu Mtume swala na salamu za Allah zimshukie na masahaba zake hawakufanya hivyo.

## ❋ Fadhila ya kufa katika Madina:

Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amesema kuwa mtu yeyote atakayekufa katika Madina akiwa katika imani, basi hakika atapata maombezi yake au atakuwa shahidi wake Siku ya Kiyama. Ndiyo maana Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alipendekeza sana mtu kuishi na kufariki Madina, akasema: «**Yeyote kati yenu anayeweza kufa katika Madina, basi afanye hivyo, kwani mimi nitakuwa muombezi au shahidi wake**». Imepokewa na An-Nasaai.

Na Umar ibnu al-Khattwaab Allah amridhie alikuwa akimuomba Mola wake afarikie katika Madina, na katika dua zake alisema: «Ewe Mola wangu, niruzuku nife shahidi katika njia yako, na jaalia kifo changu kiwe katika mji wa Mtume wako swala na salamu za Allah zimshukie». Imepokewa na Al-Bukhari.

Lakini yule aliyekufa nje ya Madina, kisha akazikwa ndani yake, hatapata fadhila hizo, wala hakuna fadhila yoyote ya kuzikwa ndani yake.

## ❋ Madina utakuwa mji wa mwisho kuharibika:

Katika zama za mwisho, miji yote ya Kiislamu itaharibika mmoja baada ya mwingine. Lakini Kwa sababu cheo cha Madina, mji huu utakuwa wa mwisho kuharibika. Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Mji wa mwisho katika miji ya Kiislamu kuharibika ni Madina**». Imepokewa na at-Tirmidhy.

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie pia alifafanua hali yake katika siku za mwisho, akasema swala na salamu za Allah zimshukie: «**Watu wataiacha Madina katika hali yake bora ilivyokua, na hakuna atakayeiingia isipokuwa wanyama mwitu wawindaji na ndege.** Yaani: hawataingia isipokuwa wanyama wawindaji na ndege wakitafuta riziki». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

Imam Nawawi Allah amrehemu amesema: «Maoni yanayokubalika zaidi ni kwamba kuiacha Madina huku kutakuwa katika zama za mwisho, wakati wa kusimama Kiyama»[1].

Na hii ndio hali ya dunia, kila kitu ndani yake kitatoweka. Dunia ni nyumba ya kupita tu kuelekea nyumba ya makazi ya kudumu, ima Peponi au Motoni.

❖❖❖

1 Sharhu Swahiih Muslim, 9/160.

# Msikiti wa Mtume

# (Al-Masjidun-Nabawi)

## Fadhila ya Msikiti wa Mtume

Allah ameuchagua Msikiti wa Mtume kwa kuupa fadhila nyingi, miongoni mwazo ni:

**1)** Nabii swala na salamu za Allah zimshukie ndiye aliyeujenga, kwa hivyo ni mojawapo ya misikiti mitatu iliyojengwa na manabii wa Allah. Kwani Al-Masjidul-Haraam (Makkah) ulijengwa na Ibrahim salamu zimshukie, Al-Masjidun-Nabawi (Madina) ulijengwa na Mtume wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie, na Al-Masjidul-Aqswaa (Msikiti wa Al-Aqsa) inasemekana ulijengwa na Adam salamu zimshukie.

**2)** Ni msikiti wa mwisho ulijengwa na nabii. Kwa kuwa Mtume wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie aliujenga Al-Masjidun-Nabawi, na hakuna nabii mwingine baada yake, basi hakuna msikiti utakaojengwa na nabii baada yake. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amesema: «**Hakika mimi ni nabii wa mwisho, na hakika msikiti wangu ni msikiti wa mwisho**». Imepokewa na Muslim.

**3)** Msikiti wake umejengwa juu ya msingi wa Taqwa (uchaji Allah). Abu Sa'id Al-Khudri Allah amridhie alisema: «Ewe Mtume wa Allah! Ni msikiti gani kati ya misikiti miwili ulijengwa juu ya msingi wa Taqwa?” Mtume swala na salamu za Allah zimshukie akaichukua kiganja cha kokoto, akazipiga chini, kisha akasema: “**Ni msikiti wenu huu**” - akimaanisha Msikiti wa Madina». Imepokewa na Muslim.

**4)** Swala katika Msikiti huo ni bora kuliko swala elfu moja (katika misikiti mingine). Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Swala moja katika msikiti wangu huu ni bora kuliko swala elfu katika misikiti mingine isipokuwa Al-Masjidul-Haraam**». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

**5)** Ni mmoja wa misikiti mitatu ambayo tumeambiwa tufunge safari kuiendea.

# Ujenzi wa Msikiti wa Mtume na Upanuzi wake Katika Historia

Mtume swala na salamu za Allah zimshukie aliujenga msikiti wake mwanzo alipofika Madina. Akazifanya kuta zake ni za matofali, nguzo zake za mashina ya mtende, na paa lake kuwa la majani ya mtende. Ukubwa wake ulikuwa 32.5m x 28m.

Baadaye, Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie ulipata hatua kadhaa za upanuzi, kama ifuatavyo:

**Upanuzi wa Kwanza**: Mtume swala na salamu za Allah zimshukie aliupanua mwaka wa 7 Hijria, baada ya vita vya Khaibar. Eneo lake likaongezeka hadi 46m x 46m.

**Upanuzi wa Pili**: Umar ibnu Al-Khattwaab Allah amridhie aliupanua mwaka wa 17 Hijria, sehemu ya upande wa magharibi na kusini, na eneo lake likawa 65m x 55.5m.

**Upanuzi wa Tatu**: Uthmaan ibnu Affaan Allah amridhie aliupanua mwaka wa 29 Hijria sehemu ya upande wa magharibi, kusini, na kaskazini. Eneo lake likawa 74m x 69.5m.

**Upanuzi wa Nne:** Katika utawala wa Al-Waliid ibnu Abdulmalik Allah amrehemu, mnamo mwaka 88 Hijria, aliupanua msikiti upande wa mashariki, magharibi, na kaskazini, na akaingiza vyumba katika msikiti, na eneo la msikiti likawa 93m x 93m.

**Upanuzi wa Tano:** Katika utawala wa Al-Mahdi ibn Al-Mansur Allah amrehemu, mnamo mwaka 162 Hijria, aliupanua msikiti upande wa kaskazini kwa 245$m^2$.

**Upanuzi wa Sita**: Katika utawala wa Sultan Qayitbay al-Mamluki Allah amrehemu, mnamo mwaka 888 Hijria, aliupanua msikiti upande wa mashariki kwa 120$m^2$.

**Upanuzi wa Saba**: Katika utawala wa Sultani wa Ottoman Abdulmajiid Khan Allah amrehemu, alianza upanuzi wake mwaka wa 1265 Hijria, na ukakamilika mwaka wa 1277 Hijria. Alibomoa sehemu ya msikiti na kuujenga upya, na akaongeza 1293$m^2$ katika

upande wa kaskazini. Jengo la zamani katika upande wa kusini wa Msikiti wa Mtume yalioko wakati huu pamoja na mapambo yake yalifanywa katika enzi yake.

**Upanuzi wa Nane**: Ulianza katika utawala wa Mfalme Abdulaziz Al Saud Allah amrehemu mnamo 13/3/1372 Hijria, kisha akafariki mnamo 2/3/1373 Hijria, Allah amrehemu. Upanuzi huu ulikamilishwa na Mfalme Saud Allah amrehemu, na upanuzi wenyewe ulikuwa upande wa kaskazini wa msikiti. Hatimaye upanuzi huu ulikamilika katika utawala wa Mfalme Saud Allah amrehemu mnamo 5/3/1375 Hijria, ambapo eneo lake lilikuwa 6024$m^2$.

**Upanuzi wa Tisa**: Ulikua katika utawala wa Mfalme Faisal ibnu Abdulaziz Al Saud Allah amrehemu, mnamo mwaka wa 1395 Hijira, ambapo aliongeza kwenye ardhi ya msikiti 35,000$m^2$ katika upande wa magharibi wa msikiti. Japo upanuzi huu haukuhusisha msikiti wenyewe; badala yake, alifanya eneo hilo kuwa muswalla mkubwa, na akaweka miavuli juu yake. Kisha akaongeza 5,550$m^2$, na akaweka miavuli juu yake pia.

**Upanuzi wa Kumi**: Katika utawala wa Mfalme Khalid ibnu Abdulaziz Al Saud Allah amrehemu, mwaka wa 1397 Hijria, aliongeza 43,000$m^2$ katika upande wa kusini-magharibi wa ardhi ya msikiti kwa nje. Na upanuzi huu haukuhusisha msikiti wenyewe; badala yake, aliweka miavuli juu yake, na akatenga sehemu kwa ajili ya maegesho ya magari.

**Upanuzi wa Kumi na Moja**: Katika utawala wa Mfalme Fahd ibnu Abdulaziz Al Saud Allah amrehemu mwaka wa 1405 Hijria, aliupanua msikiti upande wa kaskazini, magharibi-kaskazini, na mashariki-kaskazini. Eneo lake likawa 82,000$m^2$. Na kwa upanuzi huu, eneo la Msikiti wa Mtume liliongezeka zaidi ya mara tano.

**Upanuzi wa Kumi na mbili**: Katika utawala wa mtumishi wa misikiti miwili mitukufu, Mfalme Abdullah ibnu Abdulaziz Al Saud Allah amrehemu, aliamuru upanuzi mkubwa mwaka wa 1433 Hijria. Ikaanza kazi hio ya kuupanua msikiti, lakini mfalme alikufa mwaka wa 1436 Hijria. (Mfalme aliyetawala baada yake) Mtumishi wa misikiti miwili mitukufu, Mfalme Salman ibnu Abdulaziz Al

Saud Allah amuhifadhi akaamuru kazi hio ikamilishwe.

Na kazi hio ya upanuzi bado inaendelea hadi leo.[1]

1 Al-Bidaayah wan-Nihayah 12/419, Al-Kaamil fii at-Tarikh 4/14, Wafaau al-Wafaa 1/361, Taarikh Makkah wal-Madiinah cha Ibnu Ad-Dhiyaa 1/267, Ad-Durratu Ath-Thamiinah, uk. 87, Qiswatu at-Tawsi'atul Kubraa, uk. 253, Ujenzi na Upanuzi wa Msikiti wa Mtume, taarifa iliyotolewa na "Uongozi Mkuu wa masuala ya al-Masjid al-Haraam na al-Masjidun-Nabawi".

## Rawdha

Katika Msikiti wa Mtume kuna sehemu ambayo Mtume swala na salamu za Allah zimshukie aliieleza kuwa ni bustani miongoni mwa mabustani ya Peponi. Alisema: «**Baina ya nyumba yangu na mimbari yangu ni bustani miongoni mwa mabustani ya Peponi**». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

«**Baina ya nyumba yangu na mimbari yangu ni bustani miongoni mwa mabustani ya Peponi**». Imepokewa na Ahmad.

Wanachuoni wamefafanua maana ya «**bustani miongoni mwa mabustani ya Peponi**». Ibnu Hajar Allah amrehemu amesema: «“Bustani miongoni mwa bustani za Peponi” — yaani, ni kama bustani miongoni mwa bustani za Peponi katika kushuka kwa rehema na kupata furaha kutokana na kuendelea kukaa katika vikao za kumtaja Allah, hasa katika zama zake (Mtume) swala na salamu za Allah zimshukie»[1].

Kwa hivyo, kila mahali duniani ambapo kuna vikao vya kumtaja na kumkumbuka Allah, iwe ni swala, mawaidha, au kufundisha elimu ya sheria; ni bustani miongoni mwa bustani za Peponi. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amesema: «**“Mtakapopita katika mabustani ya Peponi, basi mchume na kula ndani yake”**. Wakasema: “Ewe Mtume wa Allah, na ni nini bustani za Jannah?” Akasema: **“Vikao vya dhikr”**». Imepokewa na At-Tirmidhi.

1 Fat-hul Baari, 4/100.

# Mihirabu

Katika Msikiti wa Mtume kuna mihirabu tatu:

**1) Mihirabu iliyowekwa katika mahali pa imamu alipokuwa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie akiwaswalisha waumini.** Nayo ni ile iliyoko upande wa kushoto wa mimbari kuelekea vyumba vya Mtume swala na salamu za Allah zimshukie. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akiswali katika sehemu hii au karibu nayo bila mihirabu, kwani Msikiti wa Mtume haukuwa na mihirabu katika zama zake swala na salamu za Allah zimshukie, wala zama za makhalifa waongofu. Mtu wa kwanza kuanzisha mihirabu katika msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa Al-Waliid ibnu Abdulmalik mwaka wa 91 Hijria, kisha ilijengwa upya mwaka wa 888 Hijria katika utawala wa Sultan Qaitbay Allah amrehemu, ikabaki hivyo hadi sasa.

**2) Mihirabu iliyoko upande wa kulia wa mimbari.** Ilianzishwa mwaka wa 948 Hijria katika utawala wa Sultan Suleiman Kanuni Allah amrehemu, mmoja wa watawala wa Dola ya Ottoman.

**3) Mihirabu ambayo imamu anaswali leo.** Uthmaan ibnu Affaan alikuwa anaswalisha akiwa imamu katika sehemu hii wakati alipopanua Msikiti wa Mtume, kisha Al-Waliid ibnu Abdulmalik aliweka mihirabu katika mahali alipokuwa akiswali Uthmaan Allah amridhie mnamo mwaka wa 91 Hijria, kwani hakukuwa na mihirabu katika zama za Uthmaan Allah amridhie, kisha Sultan Qaitbay Allah amrehemu akaipanua na kuifanya katika hali yake ya sasa mwaka wa 888 Hijria[1].

1 Al-Durratu ath-Thamiinah 1141, Wafaau al-Wafaa 1/282.

# Mimbari

## 1 - Historia yake:

Mimbari imepitia hatua kadhaa katika historia, ambazo ni:

1) Mwanzo wa Mtume kuujenga Msikiti wake hakukuwa na mimbari ambayo angehutubia watu juu yake. Badala yake, alikuwa akihutubu akiwa anategemea kigogo cha mti karibu na mahala anaposwali. Baadaye, alijiwekea mimbari ambayo ilikuwa na daraja tatu.

2) Katika utawala wa Muawiya ibnu Abi Sufyaan Allah amridhie, mwaka wa 50 Hijria, aliongeza daraja sita kwenye mimbari, hivyo ikawa na daraja tisa na kiti cha kukalia.

3) Mnamo mwaka wa 654 Hijria, wakati Msikiti wa Mtume ulipoungua, mimbari pia iliungua. Kwa hivyo, Mfalme Al-Mudhaffar, bwana wa Yemen, alituma mimbari mpya.

4) Mnamo mwaka wa 664 Hijria, Al-Dhwaahir Bibars alituma mimbari mpya.

5) Mnamo mwaka wa 797 Hijria, Al-Dhwaahir Barkuk alituma mimbari mpya.

6) Mnamo mwaka wa 820 Hijria, Sultan Al-Mu'ayyad Al-Mahmudi alituma mimbari mpya.

7) Mnamo mwaka wa 886 Hijria, Msikiti wa Mtume uliungua, na minbar pia iliungua. Kwa hivyo, watu wa Madina walijenga mimbari mpya ya matofali.

8) Mnamo mwaka wa 888 Hijria, Sultan Qaitbay Al-Mamluki Allah amrehemu alijenga mimbari mpya ya marumaru.

9) Mnamo mwaka wa 998 Hijria, Sultan Murad Al-Uthmaani

Allah amrehemu alituma mimbari iliyopo mpaka sasa[1].

### 2 - Maelezo yaliopokewa kuhusu mimbari ya Mtume:

A) Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alisema kwamba mimbari yake iko juu ya haudh (birika) yake, akasema: «**na mimbari yangu iko juu ya haudh yangu**». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

Maana yake ni kwamba mimbari yake itawekwa juu ya birika yake siku ya Kiyama.

Na kumesemwa: kuwa birika yake ipo katika Uwanja wa Mahshara, juu ya mahali ambapo mimbari yake iko ardhini.

B) Yamekuja makemeo kwamba yeyote atakayeapa akiwa mimbari ya Mtume swala na salamu za Allah zimshukie hali ya kuwa ni mrongo, basi mashukio yake itakua ni motoni. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Yeyote anayeapa kiapo cha uongo karibu na mimbari hii, basi ajiandalie makao yake motoni, hata kama ni (kiapo kwa ajili ya) kipande cha mswaki wa kijani**». Imepokewa na Ibnu Maajah.

Na yamekuja makemeo kwa mtu yeyote anayeapa uongo karibu na mimbari hiyo atalaaniwa. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Yeyote atakayeapa kwenye mimbari yangu hii kwa kiapo cha uongo ili kuchukua mali ya muislamu, basi iwe juu yake laana ya Allah, Malaika na watu wote, Allah hatakubali kutoka kwake faradhi wala sunna**». Imepokewa na An-Nasaai.

1 Wafaau al-Wafaa 2/130, Taariikh Makkah wal-Madiinah, uk. 270, Ad-Durratu Ath-Thamiinah, uk. 93, Fusuul min Taariikh al-Madiinah, uk. 71.

## Kuchomeka kwa Msikiti wa Mtume

Msikiti wa Mtume (katika historia yake) uliungua moto mara mbili:

**Moto wa kwanza:** Mnamo mwaka wa 654 Hijria, na sababu yake: ni kuwa mmoja wa watumishi wa Msikiti wa Mtume aliingia kwenye ghala ili kuchukua kandili za minara ya msikiti huku akiwa na moto aliokuwa akiutumia kumulikia nao njia, akaghafilika nao, moto huo ukashika baadhi ya ala zilizokuwa kwenye ghala, na ukaenea na kufika paani kwa kasi, watu wakashindwa kuuzima, na haikuchukua mda hadi misikiti mzima ukaungua, na sakafu ya nyumba ya Mtume pia iliungua. Kila kitu kilichomo kwenye msikiti kiliharibika - ikiwemo mimbari, milango, maghala na masanduku.

**Moto wa pili:** Mnamo mwaka wa 886 Hijria. Moto huu ulitokea kwa sababu kulikuwa na radi kali, kisha radi ilishuka kwenye mnara mkuu ulio karibu na kuba, radi ikagonga sehemu ya mwezi wa mnara, na mwezi ukaanguka upande wa mashariki wa msikiti ukiwa na tete kama moto, hivyo sakafu ya msikiti ikachomeka, kisha moto ukaenea katika sehemu nyingine za msikiti, na moto huo ukaichoma mimbari, sakafu nzima ya msikiti, milango yake, na vyote vilivyo ndani yake ikiwemo maghala ya vitabu na misahafu[1].

❖❖❖

1 Wafaau al-Wafaa, uk 2/371, al-Dhayl 'ala al-Rawdhatayn, uk.194, al-Maghanim al-Mutwaabah, uk.177, al-'Ibar fii Khabari Man Ghabar, uk. 3/272.

# Swala katika Msikiti wa Mtume

## Dua ya kuingia Msikiti wa Mtume

Hakuna dua maalumu ya kuingia Msikiti wa Mtume, lakini mtu anapoingia Msikiti wa Mtume hufanya kama anavyofanya katika misikiti mingine; anaingiza mguu wake wa kulia na kusema: «***Allahumma iftah lii abwaaba rahmatika*** **/Ewe Allah, nifungulie milango ya rehema yako/**». Imepokewa na Muslim.

# Kuongezeka kwa thawabu za swala katika Msikiti wa Mtume

Swala moja katika Msikiti wa Mtume ni bora kuliko swala elfu moja katika misikiti mingine. Na fadhila hii ni ya swala ya faradhi na ya Sunna. Kwa dalili ya neno la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie: «**Swala moja katika msikiti wangu huu ni bora kuliko swala elfu moja katika msikiti mwingine, isipokuwa Al-Masjidul-Haraam**». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea. Kwa hivyo, fadhila inakusanya swala yoyote (iwe ya faradhi au sunna); Imam An-Nawawi Allah amrehemu alisema: «Inakusanya swala ya faradhi na ya sunna zote mbili»[1].

Ingawa swala ya sunna katika Msikiti wa Mtume ina thawabu kubwa, ila kuiswali nyumbani ni bora zaidi. Kwa sababu Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa anaswali swala ya sunna nyumbani kwake, pamoja na kuwa Msikiti wake umeambatana na nyumba yake. Na alisema: «**Swala bora zaidi ya mtu ni nyumbani kwake, isipokuwa swala ya faradhi**». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

1 Sharhu Swahiih Muslim, 9/164.

## Niswalie sehemu gani swala ya jamaa katika Msikiti wa Mtume?

Kumkaribia imamu ndio bora. Hii ni kwa sababu ya hadithi ya Mtume swala na salamu za Allah zimshukie: «**Wale wenye akili na hekima wawe nyuma yangu (karibu nami)**». Imepokewa na Muslim. Na neno la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie: «**Safu bora kwa wanaume ni za kwanza, na safu mbaya zaidi kwao ni za mwisho. Na safu bora kwa wanawake ni za mwisho, na safu mbaya zaidi kwao ni za kwanza**». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

## Ni lipi bora: kuswali katika Rawdha au kuswali nyuma ya imamu?

Kuswali swala ya jamaa katika safu za kwanza pamoja na imamu ni bora kuliko kuswali katika Rawdha. kwa sababu Rawdha si safu ya kwanza, na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Safu bora kwa wanaume ni za kwanza, na safu mbaya zaidi kwao ni za mwisho**». Imepokewa na Al-Bukhari. Na neno lake Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, aliposema: «**Lau watu wangejua (fadhila) iliyo ndani ya kuadhini na safu ya kwanza, kisha wasipate njia ya kuyafikia hayo isipokuwa kwa kura, basi wangepiga kura kwa ajili yake**» Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

## Kukamilisha safu ni jambo la kisheria

Ni sheria kukamilisha safu ya kwanza kisha inayofuata, na maamuma haswali katika safu ya nyuma ikiwa safu iliyo mbele yake haijakamilika. Amesema Jabir ibnu Samurah Allah amridhie: «Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie alitoka mbele yetu na kusema: «**"Je, hamfungi safu kama vile malaika wanavyoweka safu zao mbele ya Mola wao?** Tukamuuliza: "Ewe Mtume wa Allah! Kwani malaika wanafungaje safu mbele ya Mola wao?" Akasema: **"Wanakamilisha safu za kwanza mwanzo zikifuatiwa na nyingine, na wanakaribiana kwenye safu"**». Imepokewa na Muslim.

Na haisihi swala ya mtu peke yake nyuma ya safu, kwa sababu ya kauli ya Mtume swala na salamu za Allah zimshukie: «**Hakuna swala kwa mtu (anayeswali) peke yake nyuma ya safu**». Imepokewa na Ahmad. isipokuwa ikiwa ni mwanamke ambaye hana mwanamke mwingine wa kuswali naye, au kwa mtu aliye na udhuru - kama vile mtu ambaye hakupata nafasi katika safu.

# Hukumu ya Kupita Mbele ya Mwenye Kuswali

Kupita mbele ya mwenye kuswali kunagawanyika mara mbili:

1) Ikiwa mwenye kuswali ni mtu peke yake au ni imamu, basi haitafaa kupita mbele yake ikiwa hakuna sutra mbele yake, sawa iwe ni msikiti wa Mtume au kwengineko, kwa dalili ya maneno ya Mtume swala na salamu za Allah zimshukie: «**Lau mwenye kupita mbele ya mtu anayeswali angejua kinachompata -yaani katika madhambi-, basi angeona kusimama arobaini ni bora kwake kuliko kupita mbele ya anayeswali**». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

Na ikiwa mmoja anaswali katika njia za kupita msikitini, basi mtu anaweza kupita mbele yake kwa sababu ameswali sehemu ambazo ni njia za kupita watu msikitini[1]. Vilevile ikiwa kuna msongamo mkubwa msikitini (inaruhusiwa kupita mbele yake), kwa dalili ya neno lake Allah mtukufu:

﴿فَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ مَا ٱسۡتَطَعۡتُمۡ﴾

«Muogopeni Allah kwa kadri ya uwezo wenu» (At-Taghabun: 16).

2) Na akiwa mwenye kuswali ni maamuma na amfuata imamu katika swala ya jamaa, basi inajuzu mtu kupita mbele yake, kwa sababu sutra ya imamu ni sutra ya wale walio nyuma yake, kwa dalili ya neno la Ibnu Abbas Allah amridhie: «Niliondoka nikiwa nimepanda punda - na siku hiyo nilikuwa karibu na umri wa kubalehe - na Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akiongoza swala sehemu ya Minaa, basi nikapita mbele ya safu, nikashuka (punda), na kumwachia punda achunge, na nikaingia kwenye safu (kuswali). Wala hakuna mtu yeyote aliyenikosoa kitendo hicho». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

1 Fataawaa Shaykh Muhammad ibnu Ibrahim, 3/38.

## Hukumu ya kuswali mbele ya Imamu

Sunna ni maamuma wasimame nyuma ya Imamu; kwa dalili ya kauli ya Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, alisema: «**Kwa hakika, imamu amewekwa ili afuatwe**». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

Ikiwa maamuma wataswali mbele ya imamu bila kuwepo na haja yoyote, basi swala zao hazitakubalika. Amesema Ibnu Qudaamah Allah amrehemu: «Sunna ni maamuma wasimame nyuma ya Imamu. Na ikiwa watasimama mbele yake, basi swala haitasihi»[1].

Na ikiwa kuna haja - kama vile kuwe na msongamano mkubwa - basi hakuna ubaya kuswali mbele ya Imamu. Amesema Sheikhul Islaam (Ibnu Taymiyyah) Allah amrehemu: «Ikiwa mtu hakuweza kuswali kwa jamaa isipokuwa mbele ya Imamu, basi katika hali hii ataswali mbele yake -kwa sababu ya haja hio- . Na hii ni kauli ya makundi katika wanachuoni, na ni mojawapo ya kanuni za jumla za sheria: kwamba jambo (ambalo mtu analazimika kulifanya) katika sheria, lakini haliwezekani kwake, basi italiondoa la wajibu» [2].

1 Al-Mughni, 2/157.

2 Fataawaa Sheikhul Islaam, 20/559.

## Namna ya Kuswali Swala ya Janaza

Uislamu umehimiza kuiswalia Jeneza, na kuifuata hadi maiti azikwe, na ukaweka thawabu kubwa kwa ajili yake. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amesema: «**“Atakayeshuhudia Jeneza hadi iswaliwe, atapata qiraati, na atakayeshuhudia hadi izikwe, atapata qiraati mbili”**. Kukaulizwa: “Ni nini qiraati mbili?” Akasema: **“Ni mfano wa milima miwili mikubwa”**». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea. Na katika tamko la Muslim: «**Qiraati ni mfano wa Mlima wa Uhud**».

Na kuswali swala ya Janaza ni sheria kwa wanawake kama ilivyo sheria kwa wanaume.

Na kwa sababu ya kukaririka kwa swala ya Janaza baada ya kila swala ya faradhi (mara nyingi) katika Al-Masjidun-Nabawi, tutataja namna ya kuiswali swala hii:

1) Baada ya takbira ya kwanza: Unasoma Suratul Fatiha.

2) Baada ya takbira ya pili: Unamswalia Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

3) Baada ya takbira ya tatu: Unamuombea maiti msamaha, rehema, na mfano wa hayo.

4) Baada ya takbira ya nne: Unanyamaza kwa muda mfupi, kisha unatoa salamu moja upande wa kulia.

## Ikiwa kuna jeneza nyingi, Je qiraati zitaongezeka?

Ikiwa kuna jeneza nyingi, basi qiraati katika thawabu zitaongezeka kwa idadi ya jeneza. Kwa dalili ya kauli ya Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, aliposema: «**Atakayeswalia jeneza (moja), atapata qiraati**». Imepokewa na Muslim.

Sheikh Abdul-Aziz ibnu Baaz Allah amrehemu amesema: «Hadithi zinaonyesha kwamba qiraati zitaongezeka kwa idadi ya Jeneza (zilioko)»[1].

1 Majmuu' Fataawaa ibnu Baaz, 13/137.

## Je naweza kuswali swala ya Sunna katika kila wakati?

Nyakati zote zinaruhusiwa kuswali swala ya Sunna isipokuwa nyakati tatu:

1) Kuanzia baada ya swala ya Alfajiri hadi baada ya kuchomoza jua kwa dakika kumi.

2) Dakika kumi kabla ya adhana ya adhuhuri hadi Adhuhuri itakapoadhiniwa.

3) Kuanzia baada ya swala ya Alasiri hadi adhana ya Magharibi.

Uqba ibnu Aamir Al-Juhani Allah amridhie amesema: «Kuna saa tatu ambazo Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alitukataza kuswali au kuzika maiti zetu ndani yake: Wakati jua linapochomoza hadi linapoinuka. Na wakati jua linaposimama katikati hadi linapopindukia upande wa machweo. Na wakati jua linapokaribia machweo hadi linapozama». Imepokewa na Muslim.

Na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Hakuna swala baada ya swala ya Alasiri hadi jua lizame, na hakuna swala baada ya swala ya Alfajiri hadi jua lipambazuke**». Imepokewa na Muslim.

## Nifanye nini katika Msikiti wa Mtume kando na kuswali?

Chukua fursa ya wakati wako kwa kuswali swala za sunna katika vipindi visivyokatazwa, pia kithirisha kusoma Qur-ani zaidi, kumdhukuru Allah mtukufu, kumuomba msamaha, kuleta dua, na kuhudhuria darasa za wanazuoni. Na ufanye ibada zote katika Msikiti wa Mtume kama unavyofanya katika misikiti mingine.

Alisema Sheikhul Islaam Allah amrehemu: «Wema waliotangulia walikuwa wakifanya katika msikiti wake kile kilichowekwa sheria kufanywa katika misikiti mingine; ikiwemo swala, kusoma Qur-ani, kumdhukuru Allah, kuomba dua, kukaa itikafu, kufundisha Qur-ani na elimu pamoja na kujifunza, na mengineo»[1].

1 Fataawaa Sheikhul Islaam, 26/156.

## Je kuswali swala arobaini za faradhi katika Msikiti wa Mtume ina asili yoyote?

Kuna hadithi inayosema kwamba «**tu yeyote atakayeswali katika msikiti wangu swala arobaini, bila kukosa hata swala moja, ataandikwa kinga kutokana na moto, ataokolewa na adhabu, na atatakasika na unafiki**». Hadithi hii imepokewa na Ahmad, lakini sanad yake ni dhaifu na matni yake ni Munkar. Kwa hivyo, haifanyiwi kazi.

Pia, kutakaswa na unafiki hakupatikani isipokuwa kwa kuuacha unafiki. Kwa sababu unafiki ni ukafiri wa ndani, na njia ya kujiokoa nao ni kutubia. Na lau mnafiki ataswali kadri awezavyo, swala yake haitakubaliwa mpaka atubie. Amesema Allah aliyetukuka:

﴿وَمَا مَنَعَهُمۡ أَن تُقۡبَلَ مِنۡهُمۡ نَفَقَٰتُهُمۡ إِلَّآ أَنَّهُمۡ كَفَرُواْ بِٱللَّهِ وَبِرَسُولِهِۦ﴾

«Na hakuna kilichozuia kukubaliwa kutoka kwao wanavyovitoa isipokuwa kwa kuwa wao wamemkufuru Allah na Mtume wake» [At-Tawbah: 54].

## Kupaza Sauti Katika Msikiti wa Mtume

Kuinua sauti katika misikiti ni jambo liliokatazwa, na makatazo haya yanatiliwa mkazo zaidi katika Msikiti wa Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie. Na Umar ibnu Al-Khattwaab Allah amridhie aliwaona watu wawili wakipaza sauti zao katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, akasema kuwaambia: «Lau mngekuwa ni wenyeji wa mji huu, ningewapa adhabu! Hivi mwainua sauti zenu katika Msikiti wa Mtume wa Allah!» Imepokewa na Al-Bukhari.

## Dua ya Kutoka Msikiti wa Mtume

Hakuna dua maalumu ya kutoka Msikiti wa Mtume, bali huwa ni kama misikiti mingine. Mtu anapotaka kutoka msikitini, anatanguliza mguu wake wa kushoto na kusema: «***Allahumma innii as-aluka min fadhlika*** **/Ewe Allah, hakika mimi nakuomba fadhila zako!/**». Imepokewa na Muslim.

## Mtu aliyehiji lakini hakuzuru Msikiti wa Mtume, Je Hija yake ni pungufu?

Si katika sunna za Hija au kukamilika kwake kuutembelea Msikiti wa Mtume, kabla au baada ya Hija. Kwa sababu kuutembelea Msikiti wa Mtume ni jambo la sunna tu, sio la lazima. Kwa hivyo, ikiwa mwenye kuhiji hajautembelea Msikiti wa Mtume basi hatapata dhambi. Wala hakuna uhusiano kati ya Hija na kuutembelea Msikiti wa Mtume. Kwa kuwa hizi ni ibada mbili tofauti ambazo hazina uhusiano wowote moja kwa nyingine.

Kwa hivyo, mtu ambaye amefanya Hija halazimiki kuutembelea Msikiti wa Mtume. Vilevile, ambaye ameutembelea Msikiti wa Mtume wakati wa Hajj halazimiki kwenda kufanya Hija. Na ikiwa mtu atachanganya kati ya Hajj, Umra na kutembelea Msikiti wa Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie katika safari moja, basi hakuna ubaya wowote.

❖❖❖

# Nyumba za Mtume swala na salamu za Allah zimshukie

# Nyumba za Mtume swala na salamu za Allah zimshukie

Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa na nyumba tisa kwa idadi ya wake zake, ambao aliwaacha alipoaga dunia. Na hakika Allah alizinasibisha kwa Mtume wake swala na salamu za Allah zimshukie katika kauli yake Allah aliposema:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ لَا تَدْخُلُوا۟ بُيُوتَ ٱلنَّبِىِّ إِلَّآ أَن يُؤْذَنَ لَكُمْ﴾

«Enyi mlioamini! Msiingie nyumba za Mtume isipokuwa mkisha ruhusiwa» [Al-Ahzaab: 53].

Na akazinasibisha nyumba hizi kwa wake za Mtume katika Kauli yake:

﴿وَقَرْنَ فِى بُيُوتِكُنَّ﴾

«Na kaeni majumbani mwenu» [Al-Ahzaab: 33].

## ❋ Vipengele vya Nyumba:

Nyumba za Mtume swala na salamu za Allah zimshukie zimegawanyika katika aina mbili kulingana na vipengele vyake:

A) Nyumba zenye chumba kimoja pekee, na zinaitwa “Bayt”. Na idadi yake ni tano.

B) Nyumba zilizokusanya sehemu mbili: sehemu moja ni “Bayt” (yaani chumba), na nyingine “Hujra” (yaani ua). Na idadi yake ni nne.

## ❋ Maandiko yaliokuja kuhusu “Bayt” (chumba) na Hujra (uani)

Nyumba na vyumba vya Mtume swala na salamu za Allah zimshukie zimetajwa katika maandiko kadhaa, miongoni mwazo ni:

1) Kauli ya Allah aliyetukuka:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تَدۡخُلُواْ بُيُوتَ ٱلنَّبِيِّ إِلَّآ أَن يُؤۡذَنَ لَكُمۡ﴾

«Enyi mlioamini! Msiingie nyumba za Mtume isipokuwa mkisha ruhusiwa» [Al-Ahzaab: 53].

2) Na Kauli ya Allah aliyetukuka:

﴿وَقَرۡنَ فِي بُيُوتِكُنَّ﴾

«Na kaeni majumbani mwenu» [Al-Ahzaab: 33].

3) Na kauli ya Allah aliyetukuka:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ يُنَادُونَكَ مِن وَرَآءِ ٱلۡحُجُرَٰتِ﴾

«Hakika wale wanaokuita kutoka nyuma ya vyumba…» [Al-Hujuraat: 4].

4) Imekuja katika “Swahiih Al-Bukhari” na “Swahiih Muslim”, kwamba «Kuna watu wawili ambao walipaza sauti zao msikitini hadi Mtume wa Allah akawasikia sauti zao akiwa nyumbani kwake, Mtume akawatokea akafunua pazia ya chumba chake».

5) Imekuja katika “Swahiih Al-Bukhari” na “Swahiih Muslim”: Amepokewa Anas ibnu Malik Allah amridhie: «Kwamba Abu Bakr alikuwa akiongoza watu katika swala wakati Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie alipokuwa na ugonjwa ambao alifariki nao. Ilipofika siku ya Jumatatu na hali masahaba wakiwa wamepiga safu kwenye swala, Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie alifunua pazia ya chumba chake na kututazama».

6) Aisha Allah amridhie amesema: «Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akinijia wakati akiwa katika i'tikafu msikitini, akategemea kwenye kizingiti cha mlango wa chumba changu, basi nami nikamwosha kichwa chake nikiwa

katika chumba changu, na hali ya kuwa mwili wake mzima uko msikitini». Imepokewa na An-Nasaai.

7) Aisha Allah amridhie amesema: «Naapa kwa Allah, nimemwona Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie akiwa amesimama kwenye mlango wa chumba changu, na Wahabeshi wanacheza na mikuki yao katika msikiti wa Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie, akanisitiri mimi kwa nguo yake, ili niweze kutazama uchezaji wao». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

8) Aisha Allah amridhie amesema: «Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akiswali chumbani, hali ya kuwa mimi niko nyumbani». Imepokewa na Ahmad.

9) Aisha Allah amridhie amesema: «Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akiswali usiku katika chumba chake (cha kuswali), na ukuta wa chumba hicho ulikua mfupi, watu wakaona sura ya Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, hivyo watu wakasimama na kuswali wakimfuata swala yake». Imepokewa na Al-Bukhari.

10) Kilikuwa kisomo cha Mtume swala na salamu za Allah zimshukie pengine anakisikia aliye kwenye Hujra (uani), wakati yeye alikuwa katika Bayt (chumba cha faragha)». Imepokewa na At-Tirmidhi.

Ibnu Taymiyya Allah amrehemu amesema: «Katika hadithi hizi, neno “Hujra” halimaanishi nyumba nzima, kama ilivyo katika aya ya Qur-ani:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ يُنَادُونَكَ مِن وَرَآءِ ٱلۡحُجُرَٰتِ أَكۡثَرُهُمۡ لَا يَعۡقِلُونَ﴾

«Hakika wale wanaokuita kutoka nyuma ya vyumba, wengi wao hawana akili» [Al-Hujuraat: 4].

Bali, lina maana ya sehemu inayofanywa ukumbi wa nje kutoka mlangoni mwa chumba cha faragha, kama vile ua wa

nyumba. Chumba hiki kilikuwa kinatengenezwa kwa majani ya mitende, tofauti na vyumba ambayo ni vya makazi, hivi vilikuwa vinatengenezwa kwa matofali»[1].

## ❋ Aina ya jengo lake:

A) Bayt (chumba cha faragha): -ambacho ndio chumba chenyewe cha kuishi- kuta zake ni za matofali, na sakafu yake ni ya majani ya mitende.

B) Hujra (sehemu ya nje ya chumba): -ambako ni uani-: kimetengenezwa kwa majani ya mitende, na hakina sakafu[2].

## ❋ Mahali pake:

Nyumba za Mtume swala na salamu za Allah zimshukie ziko katika pande tatu:

1) Katika upande wa mashariki wa Msikiti wa Mtume, zimeshikana na misikiti, kama vile nyumba ya Aisha Allah amridhie.

Pia, nyumba ya Sauda Allah amridhie, iko baada ya uzio wa chuma kutoka upande wa kushoto - upande wa “Baabu Jibriil” mlango wa Jibrili.

2) Katika upande wa kusini wa Msikiti wa Mtume, zimeshikana na misikiti, kama vile nyumba ya Hafswa Allah amridhie, ambaye iko jirani na nyumba ya Aisha Allah amridhie kutoka upande wa kusini -kiasi cha sehemu yake iko ndani ya uzio wa shaba, na sehemu nyingine iko nje ya uzio huo, na mahali ndipo ambapo watu wanasimama leo kwa ajili ya kumsalimia Mtume

1 Al-Radd 'ala al-Ikhnaai, uk. 323.

2 Twabaqaat Ibnu Sa'd, 1/499, Wafaau al-Wafaa, 2/53, Ad-Durratu ath-Thamiinah, uk. 90, al-Wafaa bi Ahwaal al-Mustwafaa, uk. 258, Tahqiiq an-Nusra, uk. 49.

swala na salamu za Allah zimshukie na masahaba zake Allah awaridhie wote wawili-.

3) Katika upande wa kaskazini wa Msikiti wa Mtume, na nyumba hizi hazikushikana na misikiti; kati yake na Msikiti wa Mtume kuna nyumba za masahaba Allah awaridhie. Katika upande huu kuna nyumba za wake zake: Juwayriyya, Swafiyyah, Ummu Habibah, na Maimunah Allah awaridhie wote, na nyumba zao hazikuwa zimeshikana na Msikiti; kwa sababu Mtume swala na salamu za Allah zimshukie wakati alipowaoa hawa baada ya vita vya Khaibar, tayari kulikuwa na nyumba za masahaba Allah awaridhie ambazo zimeshikana na Msikiti, ndio Mtume swala na salamu za Allah zimshukie akajenga nyumba zao hawa nyuma ya nyumba za masahaba Allah awaridhie ili asiwasonge.


Na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie hakuwa na nyumba zozote katika upande wa magharibi wa Msikiti wa Mtume[1]. Amesema Muhammad ibnu Hilaal: «Nilizipata nyumba za wake za Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, zilikuwa za majani ya mtende, zilizofunikwa na sufu, zilikuwa zimepangwa kwenye (upande wa) Kibula, upande wa mashariki, na upande wa Shaam, wala hakukuwa na nyumba zao hata moja katika upande wa magharibi ya msikiti»[2].

---

1 Wafaau al-Wafaa 2/299, Ad-Durratu ath-Thamiinah, uk. 90, Tarikh Makkah wal Madiinah 1/268, Al-Ikhna'iyyah, uk. 136, Al-Bayaan wa al-Tahswiil 1/370, Fat-hul Baari cha Ibnu Rajab 3/209.

2 Subul al-Hudaa wa ar-Rashaad fii Siirat Khayr al-'Ibaad 3/349.

**Huu ni mchoro wa makadirio ya eneo la nyumba za Mtume swala na salamu za Allah zimshukie:**



# Wake za Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

### ⁕ Wake za Mtume swala na salamu za Allah zimshukie:

Wake za Mtume swala na salamu za Allah zimshukie walikuwa kumi na moja, wawili kati yao walifariki dunia mtume alipokua hai, nao ni Khadija binti Khuwaylid na Zaynab binti Khuzayma al-Hilaliyya, Allah awaridhie. Wakabaki chini yake wake tisa hadi alipokufa. Hapa ni orodha ya wake zake wote:

## 1. Khadija binti Khuwaylid, Allah amridhie:

Alikuwa mke wake wa kwanza, na ndiye wa kwanza kuamini katika umma huu. Alilelewa katika tabia njema, adabu, na ukarimu. Alijulikana na sifa ya kujihifadhi kujiheshimu na utukufu. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Kweli niliruzukiwa upendo wake.**». Imepokewa na Muslim.

Katika nyakati za mwanzo wa ulinganizi wake, Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alipata masaibu makubwa, na mateso yalimzidi. Khadija akawa msaada mkubwa kwake, alikuwa na moyo wa huruma na mwenye maoni ya busara. Mtume hakusikia chochote kinachomchukiza kutoka kwa watu, kisha arudi kwake isipokuwa alikuwa akimthibitisha na kumkhafifishia yaliyomsibu.

Watoto wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie wote walizaliwa na khadija isipokuwa Ibrahim. Tabia yake ilikuwa nzuri, hakumtolea maneno Mtume swala na salamu za Allah zimshukie hata siku moja, wala hakumuudhi na ugomvi.

Khadija alikuwa na nafasi kubwa katika moyo wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, hakuoa mwanamke mwingine wala kuwa na kijakazi wakati alipokua naye mpaka alipokufa, akahuzunika sana kwa kumpoteza.

## 2. Sauda binti Zama'a Allah amridhie

Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alimuoa baada ya kifo cha Khadija Allah amridhie, na aliishi naye (bila kuwa na mke mwingine) kwa takriban miaka mitatu, alikuwa mwenye hadhi na cheo, mwenye moyo msafi. Siku yake ya kuwa na Mtume alimpa Aisha Allah amridhie, kwa ajili ya kuutunza moyo wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie akitafuta kupata radhi za Mola wake.

## 3. Aisha binti Abu Bakr as-Swiddiiq Allah amridhie

Alikulia katika nyumba ya imani; kwani mama yake ni sahaba, dada yake Asma binti Abi Bakr as-Swiddiiq ni sahaba, kaka yake ni sahaba, na baba yake ni mkweli wa umma huu. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie hakuoa bikra mwingine ila yeye, na wahyi haukushuka katika shuka ya mwanamke mwingine isipokuwa yeye.

Allah alimpa akili nzuri, hifdhi kali, na ufahamu wa dini. Ibnu Kathiir Allah amrehemu alisema: «Hakukuwa katika kaumu (zilizopita) mfano wa Aisha Allah amridhie, katika kumbukumbu yake, elimu yake, ufasaha wake, na akili yake»[1]. Mwenye kufanya ibada nyingi, mwenye heshima na kujihifadhi nafsi yake.

Amr ibnu al-Aas Allah amridhie alimwuliza Mtume swala na salamu za Allah zimshukie: «“Ni nani unayempenda zaidi?” Akasema: **“Aisha”**. Nikasema: “Katika wanaume?” Akasema: **“Baba yake”**». Imepokewa na Al-Bukhari.

Alikuwa akikesha ili Mtume wetu swala na salamu za Allah zimshukie apate raha, akimtunza na kumhudumia akiwa mgonjwa, mpaka akafa nyumbani kwake kwenye usiku wake, akiwa kwenye

1 Al-Bidayah wa an-Nihayah 4/322.

kifua chake, na kichwa cha Mtume kikiwa kwenye kidevu chake.

## 4. Hafswa binti Umar ibnu Al-Khattwaab Allah amridhie

Aliinukia katika nyumba ya kutetea dini na kudhihirisha haki, watu saba wa familia yake walipigana katika vita vya Badr. Alikuwa mwanamke mwenye kuswali sana usiku na mwenye kufunga sana.

## 5. Zainab binti Khuzaimah Al-Hilaaliyyah Allah amridhie

Mwenye kutoa (katika njia ya Allah), na mwenye kukimbilia katika mambo ya kheri, anaitwa mama wa maskini kwa wingi wa wema wake, alikaa kwa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie miezi miwili kisha akafariki.

## 6. Ummu Habiiba Ramla bint Abu Sufyan Allah amridhie

Aliyeenda Hijra mbili; aligura kwenda Habasha[1]* na kwenda Madina, hakuna katika wake zake ambaye alipewa mahari mengi kuliko yeye, Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alifungishwa ndoa naye akiwa Habasha alipokimbia kuhifadhi dini yake, na mfalme wa Habasha alimlipia mahari yake na kumtayarishia Mtume.

## 7. Ummu Salamah Hind binti Abi Umayyah Allah amridhie

Mwenye subira na utunzaji, ni miongoni mwa Muhajirina wa kwanza, na alipotaka kuhamia Madina pamoja na mumewe Abu

1 Habasha ilikuwa katika eneo la Afrika Mashariki kipindi cha kale, ilijumuisha Ethiopia, sehemu za Sudan, Somalia na Kenya.

Salamah, watu wake walimtenganisha kati yake, mumewe na mtoto wake, akasema: «Nilikuwa nikitoka kila asubuhi na kukaa kwenye Abwath, na sikuacha kulia mpaka jioni, mwaka kamili au karibu ya hapo, mpaka wakanihurumia ndipo wakanirudishia mtoto wangu.».

Imani yake kwa Allah ilikuwa imara. Mumewe Abu Salamah alipokufa na kumwacha, aliomba dua ya kinabii; basi Allah akampa Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie awe mumewe badali yake. Alisema: «Nilimsikia Mtume swala na salamu za Allah zimshukie akisema: **"Hakuna Muislamu anayepata msiba, kisha akasema: *Innaa lillaahi wa innaa ilayhi raaji'uun, Allahumma aljurni fii mushibati, wa akhlif lii khayran minhaa* / Hakika sisi ni wa Allah na hakika kwake tutarejea, Ewe Allah, nipe malipo kwa msiba wangu, na nibadilishie bora kuliko (niliyempoteza katika) msiba huu!/ ; isipokuwa Allah atambadilishia bora kuliko aliyempoteza"**». (Ummu Salama) Akasema: «Basi alipokufa Abu Salamah, nilisema (nikifikiria): "Ni nani kati ya Waislamu aliye mbora kuliko Abu Salamah!? (Mtu ambaye) Familia yake ndio ya kwanza kuhama kwenda kwa Mtume wa Allah!". kisha nikaiomba dua hio, basi Allah akanipa badali yake Mtume wake swala na salamu za Allah zimshukie». Imepokewa na Al-Bukhari.

## 8. Zainab binti Jahsh Allah amridhie

Ni mke wa karibu zaidi kinasaba na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, kwani yeye ni binti wa shangazi yake. Mama yake ni Ummu Umayma binti Abd al-Muttwalib. Alineemeka kuwa kwenye familia yenye cheo na nasaba tukufu. Aisha Allah amridhie alisema kuhusu Zainab binti Jahsh: "Yeye ndiye aliyekuwa anafanana na mimi, katika wake za Mtume swala na salamu za Allah zimshukie". Allah alimuozesha kwa maandiko yalio kwenye kitabu chake bila kuwepo walii au shahidi. Alisema Allah Mtukufu:

﴿فَلَمَّا قَضَىٰ زَيْدٌ مِّنْهَا وَطَرًا زَوَّجْنَٰكَهَا﴾

«Basi Zaid alipomaliza haja yake naye tulikuoza wewe» [Al-Ahzaab: 37].

Kufunga ndoa Mtume naye swala na salamu za Allah zimshukie ilikuwa ni baraka kwa wanawake wa kiislamu hadi siku ya Kiyama, kwani hijabu ilifaradhishiwa wanawake baada ya yeye kuolewa.

Alikuwa ni mwenye kufanya mema na kutoa sadaka kwa wingi. Pamoja na kuwa na cheo kitukufu na hadhi yake ya juu, alikuwa akifanya kazi kwa mikono yake mwenyewe, akipaka ngozi, kuchonga, na kutoa sadaka kutokana na mapato yake. Aisha Allah amridhie alisema juu yake: «Sijawahi kuona mwanamke bora katika dini kuliko Zainab; alikuwa mchaji Allah zaidi, na mkweli zaidi katika mazungumzo, aliyeunganishwa zaidi kizazi, na mtoaji zaidi wa sadaka».

## 9. Juwayriyya binti Al-Haarith Allah amridhie

Baba yake alikuwa kiongozi anayeheshimiwa na Kusikilizwa na watu wake. Alikuwa mwingi wa ibada na mwenye baraka katika nafsi yake na kwa watu wake. Aisha Allah amridhie alisema: «Sijaona mwanamke ambaye alikuwa na baraka kubwa zaidi kwa watu wake kuliko yeye». Watu mia moja wa familia kutoka kwa Bani al-Mustwalaq waliachiliwa huru kwa sababu yake; kwa sababu Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alimuoa, na yeye atoka kwenye kabila la Bani al-Mustwalaq.

Alikuwa na matendo mengi ya ibada, alikuwa akikaa mahali pake pa kuswali akidhukuru Allah hadi katikati ya mchana. Alisema: «Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie alikuja kwangu asubuhi na mimi nilikuwa nikileta tasbih, kisha akaondoka kuelekea shughuli zake, kisha akarudi karibu na katikati ya mchana, akasema: **"Je, bado uko hapo umekaa (unamdhukuru Allah)?"** Nikamwambia: "Ndio"». Imepokewa na Ahmad.

## 10. Swafiyya binti Huyay Allah amridhie

Ametoka katika kizazi cha Harun salamu zimshukie, alikuwa mwenye cheo na akili, mwenye hadhi, dini, subira na utukufu. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alimwambia: «**Hakika wewe ni binti wa nabii (yaani Harun), na ami yako ni nabii (yaani Musa), na wewe upo chini ya nabii**». Imepokewa na At-Tirmidhi.

## 11. Maimuna binti Al-Haarith Al-Hilaliyya Allah amridhie

Alikuwa mmoja wa wanawake watukufu, alikuwa ni mwenye kuunga kizazi, Allah alimtumuku usafi wa moyo, tabia njema na mwenye kulazimiana na ibada. Aisha Allah amridhie alisema: «Hakika yeye alikuwa miongoni mwa wenye kumcha Allah zaidi na mwenye kuunganisha kizazi zaidi kati yetu».

## Maisha yao pamoja na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

Hawa ndio wake wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, waliishi naye katika nyumba zilizojengwa kwa matofali na majani ya mitende, lakini zilikuwa zimejaa imani na taqwa. Walivumilia pamoja na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie umaskini na njaa. Ilikuwa ikiwapitia Mwezi mmoja au miwili bila kuwashwa moto katika nyumba zao, na siku nyingine zinawafikia hali ya kuwa hakuna kitu katika nyumba zao isipokuwa tende moja, na wakati mwingine wakati mrefu unapita kukiwa hakuna chakula chochote, isipokuwa maji.

Watano kati yao waliolewa na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie na wakiwa na umri wa miaka baina arobaini hadi sitini. Kwa njia hii, alihakikisha utunzaji wa wajane na malezi ya watoto wao yatima.

Mtume alimuoa Khadija Allah amridhie akiwa na umri wa miaka arobaini, na alikuwa na watoto watatu kutoka kwa mume mwingine, ambapo yeye alikuwa hajawahi kuowa kabla ya hapo. Alimuoa Zainab binti Khuzayma Allah amridhie ambaye alikuwa mjane aliyefikia miaka sitini. Akamuoa Umm Salama Allah amridhie ambaye alikuwa mjane mwenye watoto sita. Akamuoa Sauda Allah amridhie ambaye alikuwa mjane mwenye umri wa miaka hamsini na tano.

Alikuwa mume mwema kwao, mwenye huruma, mkarimu, aliyekua mzuri katika kuishi nao, mwenye tabasamu kila wakati, na mwenye upole nao. Kwa hivyo, mtu yeyote anayetaka furaha lazima amfanye kiumbe bora Mtume swala na salamu za Allah zimshukie ndio kielelezo chake. Upande mwingine mwanamke wa Kiislamu anapaswa kufuata nyayo za wake zake wema, kwani hakuna wokovu kwa mwanamke isipokuwa kwa kufuata sifa zao katika kujisitiri, wema, uchaji Allah, na kumfanyia ihsani mume na mtoto.

# Al-Hujratun-Nabawiyyah

# Al-Hujratun-Nabawiyyah

**Al-Hujratun-Nabawiyyah** (Nyumba ya Mtume) – ni nyumba ambayo Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akiishi na mkewe, Mama wa Waumini, Aisha binti Abu Bakr. katika enzi ya Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, vilevile wakati wa makhhalifa wake waongofu, na mwanzo wa ukhalifa wa Banu Umayyah, nyumba hii ilikuwa nje ya Msikiti wa Mtume upande wa mashariki-kusini. Nyumba yake ikawa maarufu kama «Al-Hujratun-Nabawiyyah», kwa sababu Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alikufa na kuzikwa humo.

## ❋ Maelezo ya Al-Hujratun-Nabawiyyah

Al-Hujratun-Nabawiyyah ambayo Aisha binti Abu Bakr alikuwa akiishi humo ilipitia hatua kadhaa:

## ❋ Hatua ya kwanza

Ilijengwa na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie pamoja na msikiti wake katika mwaka wa kwanza wa Hijra.

**Vipengele vyake:**

Al-Hujratun-Nabawiyyah (ambayo ndio nyumba ya Aisha binti Abu Bakr) imekusanya vitu viwili:

**A) "Bayt" yake - ambacho ni chumba chake:** Imejengwa kwa matofali, na sakafu yake imetengenezwa kwa majani ya mitende. Ina mlango wa mbao upande wake wa kaskazini-mashariki unaofungua kwenye chumba chake. Amesema Muhammad bin Hilaal: «Niliziona nyumba za wakeze Mtume swala na salamu za Allah zimshukie... Na mlango wa Aisha - yaani, mlango wa chumba chake - ulikuwa unaelekea Shaam

(yaani upande wa kaskazini)»[1]. Na akasema Ash-Shaafi'iy Allah amrehemu: «Wameniambia watu waaminifu katika wenzetu kuwa kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie liko upande wa kulia wa anayeingia mlangoni, na limeambatana na ukuta»[2].

**Na urefu wa chumba chake:**

Urefu wa upande wa kusini: 4.90m.

Urefu wa upande wa kaskazini: 5.24m.

Urefu wa pande za mashariki na magharibi: 3.50m.[3]

Na jumla ya eneo lake lote: 17.75$m^2$.

Daud ibnu Qais alisema: «Niliziona nyumba za wake za Mtume swala na salamu za Allah zimshukie zikiwa zimefunikwa kwa nje na matawi ya mtende na kufunikwa na vazi [tambara] la manyoya. Nadhani upana wa nyumba kutoka mlango wa nyumba hadi mlango wa chumbani ni karibu dhiraa 6 au 7, na urefu wa ndani ya nyumba ni dhiraa 10. Na nadhani unene wake ni kati ya dhiraa 7 na 8. Pia nilisimama mbele ya mlango wa Aisha Allah amridhie na nikapata kuwa unaelekea upande wa magharibi[4]»[5].

**Urefu wake:** ni mita 2 takriban. Al-Hasan al-Basri Allah amrehemu alisema: «Nilikuwa nikiingia katika nyumba za Nabii

---

1 Subul al-Hudaa wa ar-Rashaad fii Siirat Khayr al-'Ibaad 3/349.

2 Al-Umm 2/147.

3 Khulaswat al-Wafaa 2/201, Al-Durratu ath-Thamiinah 2/358.

Urefu wa kuta mbili: ulipimwa na As-Samhuudi (Allah amrehemu) mwenyewe kwa kutumia tawi refu (la mtende) sawa na urefu wa dhiraa moja. Nami nikavibadilisha vipimo hivyo vya urefu kwa kutumia kitengo cha mita na kinachotawika chini yake. Na urefu wa dhiraa alioutegemea ni 0.46m. [Wafaau al-Wafaa 1/85, 50/2, 326, 330, Khulaswat al-Wafaa 2/201].

4 Magharibi ya Madina inamaanisha Shaam. Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «Watu wa magharibi wataendelea kuwa na nguvu». Imepokewa na na Muslim. Amesema Sheikhul Islaam Ibnu Taymiyyah Allah amrehemu alisema katika Fataawa 3/548: «Watu wa Madina walikuwa wanawaita watu wa Shaam: watu wa Magharibi».

5 Al-Adab Al-Mufrad cha Al-Bukhari, nambari 451.

swala na salamu za Allah zimshukie nikiwa kijana niliyekaribia kubaleghe na ningeweza kugusa sakafu kwa mkono wangu»[1].

**Manufaa ya chumba:**

Nyumba ya Nabii swala na salamu za Allah zimshukie ilikuwa na eneo dogo lakini ilikuwa imebarikiwa. Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alifaidika nayo kwa mambo mbalimbali, na miongoni mwao:

1) Alikuwa akiishi humo na mkewe.
2) Kulikuwa na kitanda ambacho alilala juu yake.
3) Aliswali rakaa za sunna ndani yake.
4) Alipokea wageni humo.
5) Kulikuwa kunaandaliwa humo chakula kwa ajili yake na wageni.
6) Kulikuwa na sehemu ya kuhifadhia vitu vya Aisha, na humo kulikuwa na kabati.

Vyote hivyo vikiwa katika chumba kimoja.

Na katika baadhi ya nyumba za Nabii swala na salamu za Allah zimshukie kulikuwa na watoto wasiokuwa wake – miongoni mwa watoto wa kulelea katika watoto wa wakeze - wanaoishi naye katika chumba kimoja, na idadi ya watoto hawa wa kulelea pamoja na mayatima katika nyumba zake inakuribia watoto kumi.

Kutokana na udogo wa nyumba ya Nabii swala na salamu za Allah zimshukie, alikuwa anaposujudu, akigusa miguu ya Aisha Allah amridhie ili aisogeze. Aisha Allah amridhie alisema: «Nilikuwa nalala mbele ya Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie na na miguu yangu ikiwa kwenye Kibula chake, na wakati anaposujudu akinigusa, hivyo nakunja miguu yangu, na anaposimama nainyoosha miguu yangu». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

1 Al-Adab Al-Mufrad cha Al-Bukhari nambari 450, Shu'ab Al-Imaan cha Al-Bayhaqi nambari 10250, Ar-Raddu ala al-Bakri 1/146, Khulaswat al-Wafaa 2/71.

**Na kukuribisha maana ya hadithi hii:** Upana wa nyumba ni 3.5m, na kitanda upana wake ni 1.5m takriban. Aisha Allah amridhie alilala ardhini kwa kiasi cha takriban 0.65m. Alishuhudia mwenyewe na kusema: «Hali ya kuwa nalala kwenye kitanda changu mbele ya Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie, wakati yeye mtume anaswali». imepokewa na An-Nasaai. Nabii swala na salamu za Allah zimshukie akimgusa ili akunje miguu yake ndipo hapo pawe mahala pa kusujudia, kuna upana wa takriban 1.35m.

**B) "Hujra" yake (uani kwake).** Ni sehemu nje ya nyumba, iliyozungukwa na matawi ya mtende, bila dari, amepokewa Aisha Allah amridhie kuwa alisema: «Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akiswali Alasiri hali ya kuwa jua bado li chumbani kwake, na kivuli hakijatokea (humo) bado». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

Ua huo ulikuwa na mlango katika upande wa magharibi unaofungua kuelekea Msikiti wa Mtume. Na mlango huo ulikuwa na kizingiti, kwa mujibu wa kauli ya Aisha Allah amridhie, alisema: «Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akija kwangu akiwa katika i'tikaf msikitini na akategemea kizingiti cha mlango wa ua wangu». Imepokewa na an-Nasa'i. Na kwenye mlango huo kulikuwa na pazia la sufi jeusi lenye urefu wa 1.4m na upana wa 0.46m.

**Vipimo vya ua:**


Urefu wa pande za kusini na kaskazini: kila mmoja 5.24m takriban.


Urefu wa pande za mashariki na magharibi: kila mmoja 3.5m takriban.

**Urefu wa kwenda juu wa kuta za ua:** 1.6m takriban.[1]

1 Al-Radd 'ala Al-Bakri 1/146, Shu'ab Al-Imaan cha Al-Bayhaqi, nambari 10250, Al-Radd 'ala Al-Ikhnaa'i uk. 323, Ad-Durratu ath-Thamiinah 2/358.

**Huu ni mchoro wa makadirio ya chumba pamoja na ua:**




## ❋ Hatua ya pili:

Mnamo mwaka wa 11 Hijria, baada ya kifo cha Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, Aisha Allah amridhie aliweka pazia chumbani kwake upande wa kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie ili kutenganisha baina yake na kaburi la mtume.

Amesema Sheikhul Islaam Ibnu Taymiyyah Allah amrehemu: «Hakika masahaba hawakuwa wakisimama msikitini ubavuni mwa kaburi, wala hawakukithirisha kuingia, bali wala hawakukithirisha kuingia hadi kwenye kaburi. Lakini Mtume alizikwa kwenye chumba, na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie aliwazuia watu -ikiwemo masahaba wake na wengineo- kuingia hadi kwenye kaburi lake. Lakini wale walioingia walikuwa wanaenda kwa Aisha Allah amridhie, ambapo yeye alikuwa upande mmoja wa chumba kando na kaburi. Na wakati mwingine baadhi ya Taabina walimuomba awaonyeshe kaburi, basi ndipo (Aisha) anawaonyesha; ili wajue sunna katika makaburi, na kwamba yanapaswa kuwa chini, sio kuinuliwa juu»[1].

1 Qaa'idatun 'adhwiima fii al-Farq bayna 'ibaadaat Ahl al-Islaam wal-Iimaan, uk. 79.

**Na huu ndio mchoro wake takriban:**




## ❋ Hatua ya tatu:

Alipofariki Abubakar Asswidiiq Allah amridhie mwaka wa 13 Hijria; kulitokea katika awamu hii mambo mawili:

1) Abubakar Allah amridhie alizikwa katika nyumba ya Aisha Allah amridhie pamoja na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie. Aisha Allah amridhie akaweka pazia baada ya kaburi la mtume swala na salamu za Allah zimshukie na kaburi la baba yake Abu Bakr Allah amridhie.

2) Umar ibnu al-Khattwaab Allah amridhie aliondoa matawi ya mtende yaliyokuwa uani - na akajenga sehemu yake ukuta wa matofali[1].

**Na huu ndio mchoro wake takriban:**




1 Wafaau al-Wafaa 2/301, Twabaqaat ibnu Sa'ad 1/294.

## ❋ Hatua ya nne:

Alipozikwa Umar ibnu al-Khattwaab Allah amridhie mnamo mwaka 23 Hijria katika chumba cha Aisha Allah amridhie pamoja na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie na Abu Bakr Allah amridhie, Aisha Allah amridhie alimuonea haya Umar, basi akajenga ukuta katika chumba chake kati yake yeye na makaburi matatu. Aisha Allah amridhie alisema: «Bado nilikuwa navua hijabu yangu na navaa mavazi ya kawaida katika chumba changu mpaka alipozikwa Umar ibnu al-Khattwaab ndani yake, nikawa naendelea kujistiri kwa nguo zangu hadi nilipojenga kati yangu mimi na makaburi hayo ukuta, ndipo nikavaa nguo za kawaida baadae»[1].

Na ukuta huu ulikuwa na uwazi ulio na pazia juu yake, baadhi ya Taabina[2] walikuwa wakimuomba Aisha Allah amridhie kuwaonesha kaburi basi akawa yuwawaonyesha ili waweze kujua mafundisho sahihi katika makaburi, na kwamba hayawi yenye kuinuliwa[3].

Amesema al-Qassim ibnu Muhammad: «Niliingia kwa Aisha Allah amridhie (ambaye ni khalati yake), nikasema: Ewe mamangu nifungulie kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie na rafiki zake wawili Allah awaridhie, akanifungulia makaburi matatu, hayakuwa yameinuliwa juu, na wala hayakuwa sawa na ardhi». Imepokewa na Abuu Daud.


Na Aisha Allah amridhie aliishi miaka 35 katika sehemu iliyobakia ya chumba chake, ambayo urefu wake ulikuwa ni 5.24m na upana wake takriban ni 0.72m pekee, na wala hakukiacha chumba chake na ua wake mpaka alipokufa Allah amridhie.


1 Twabaqaat ibnu Sa'ad 3/346.

2 Taabina: waliokuja baada ya masahaba.

3 Qaa'idatun 'adhwiima fii al-Farq, cha Sheikhul Islaam uk. 79.

**Na huu ndio mchoro wake takriban:**



## ❋ Hatua ya tano:

Wakati baadhi ya watu walipozidi kumwendea Aisha Allah amridhie kwa ajili ya kuyasalimia makaburi; basi aliifunga ile sehemu ndogo iliokuwa wazi na hakuna mtu yeyote aliyeweza kuingia kwenye makaburi hadi leo, isipokuwa mara mbili tu wakati wa ujenzi - kama itakavyokuja kuelezewa [1].


---

1 Wafaau al-Wafaa, 301/2, Tahqiiq an-Nusra, uk 105.

## ❋ Hatua ya sita:

Baada ya kifo cha Aisha Allah amridhie mnamo mwaka wa 58 Hijria, mlango wa chumba chake ulifungwa kabisa. Amesema Ibnu Taymiyyah Allah amrehemu: «Na baada yake (yaani, baada ya kifo cha Aisha Allah amridhie) chumba hicho kilifungwa hadi kilipoingizwa katika msikiti, na hapo mlango wake ulizibwa na ukajengewa ukuta mwingine juu yake»[1].

**Na huu ni mchoro wake takriban:**




1 Fataawaa Sheikhul Islaam 27/328.

## ❋ Hatua ya saba:

Mnamo mwaka 88 Hijria, Khalifah al-Waliid ibnu Abdulmalik alimuagiza mwakilishi wake huko Madina, Umar ibnu Abdul-Aziz, kutekeleza mambo matatu:

**Jambo la kwanza:** Kuuvunja Msikiti wa Mtume na kuupanua pande za mashariki, magharibi, na kaskazini, na kuingiza nyumba za wake za Mtume swala na salamu za Allah zimshukie ndani ya misikiti.

**Jambo la pili:** Kuziondoa kuta za nyumba ya Aisha Allah amridhie zilizojengwa kwa matofali, na kurejesha ujenzi wake kwa mawe meusi kwa kuzingatia msingi wa jengo aliolijenga Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, na vipimo vyake ni kama ifuatavyo:

Urefu wa upande wa kusini: 4.90m.

Urefu wa upande wa kaskazini: 5.24m.

Urefu wa kila moja ya pande mbili za mashariki na magharibi: 3.50m.

Urefu wake: 6.13m.

Unene wa ukuta wa mashariki: 0.63m, na unene wa kuta zilizobaki: 0.73m.

Na akafanya sakafu yake kuwa ya mbao.


Na hakuiwekea chumba cha Mtume mlango au dirisha. Wala hakuna mtu anayeweza kufikia kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie na wenzake wawil[i] (Abu Bakr na Umar)[1]. Alisema As-Samhuudi Allah amrehemu: «Na wala hatukupata kabisa kuwepo mlango kwenye nyumba ya ndani, wala hatukupata sehemu ya mlango»[2].

---

1 Fataawaa Sheikhul Islaam, 27/323.

2 Wafaau al-Wafaa 2/307.

**Na huu ni mchoro wa sura yake takriban:**



**Jambo la tatu:** Aliamrisha kuwekwa kwa ukuta mwingine wa umbo la pentagoni -yaani, wenye pembetano- uliojengwa kwa mawe meusi kuzunguka ukuta wa chumba, na kwamba mwisho wake ifanywe ya pembetatu ili watu wasiswali uani, wala kuelekea huko, na kwamba ukuta huu upotoshwe kutoka kuliani mwa Kibula, na hauna mlango au dirisha.

Ukuta huu unaambatana na ukuta wa chumba kutoka upande wa magharibi, na kuna nafasi ndogo kati yao upande wa kusini na mashariki, na nafasi nyingi kati ya ukuta wa kaskazini wa chumba hadi kona ya pembetatu ya ukuta wa umbo la pentagoni (pembetano).

Katika chini ya ukuta huu, upande wake wa magharibi-kusini, kuna kisanduku cha mbao, kinachoambatana na ardhi, kilio kwenye mstari mmoja sambamba na ukuta wa ndani wa chumba; na hutumika kama alama ya kuashiria ukuta wa chumba, urefu wake: 0.60m, upana wake: 0.50m, urefu wake wa kwenda juu: 0.80m, na kina chake ndani ya ukuta: 0.50m.

Unene wa ukuta huu katika pande zote ni 0.63m, na urefu wa kimo chake ni 6.13m.

Na ukuta huu ndio uliowekewa pazia leo, na pazia hio ndio inayoonekana kutoka kwenye uzio wa shaba wa nje [1].

**Urefu wa ukuta wa umbo la pentagoni ni kama ifuatavyo:**

urefu wa upande wa kusini – 7.80m.

Urefu wa upande wa magharibi – 7.75m. kisha unaelekea mashariki kwa urefu wa 1.15m.


Urefu wa pembetatu upande wa kaskazini-magharibi – 5.77m.

Urefu wa pembetatu upande wa kaskazini-mashariki – 6.44m.


Urefu wa upande wa mashariki – 5.77m.


1 Wafaau al-Wafaa 2/126, Khulaswat al-Wafaa 2/125, Jawaabun fii al-Hakif bi ghayr Allah cha Sheikhul Islaam uk. 14.

**Umbo la ukuta wa pentagoni unakaa hivi takriban:**



**Mchoro wa ukuta wa pentagoni pamoja na ukuta wa ndani unakaa hivi takriban:**




## ❋ Hatua ya nane:

Katika utawala wa Al-Mutawakkil (khilafa yake ilikuwa kutoka mwaka 232 hadi 247 Hijria) alijenga marumaru chini ya ukuta wa chumba, iwe kama nguo yake ya chini, na urefu wake kwenda juu ni mita 1 takriban[1].

**Na hii ndio sura yake takriban:**





1 Wafaau al-Wafaa 2/338, Al-Durratu ath-Thamiinah 2/393.

## ❋ Hatua ya tisa:

Katika ukhalifa wa Al-Muqtafii mnamo mwaka 548 Hijria; alifanya upya ukanda wa marumaru, na akafanya urefu wake kuwa 2m takriban.[1]

**Na hii ndio sura yake takriban:**




1 Wafaau al-Wafaa 2/338, At-Taarikh Al-Baahir uk. 118, Al-Maghanim Al-Mutwaaba uk. 165.

## ❋ Hatua ya kumi:

Katika utawala wa Mfalme Qaitbay Allah amrehemu kulikuwa na kubomolewa na kujengwa. Maelezo ni kama ifuatavyo:

### 1. Kubomolewa:

Mnamo tarehe 14 Sha'aban, mwaka 881 Hijria; walianza kubomoa ukuta wa nje na wa ndani, na maelezo ni kama ifuatavyo:

**A) Ukuta wa nje:** Kulibomolewa ukuta wa upande wa mashariki na pambizoni mwake kwenye sehemu inayofuatia kwenda upande uliopinda kuelekea kona ya kaskazini.

Na vipimo vyake (vilivyobomolewa) ni: 2.30m kuelekea kusini na kaskazini, na hiyo ni baada ya (kuvunjwa) 1.84m kutoka ardhini hadi juu ya ukuta.

Walibomoa upande huu kwa sababu ya kupatikana kupinda katika ukuta huu, na sababu yake ni: kupasuka kwa ukuta wa ndani na kupinda kwake kuelekea ukuta wa nje[1].

**B) Ukuta wa ndani:** Ulibomolewa kama ifuatavyo:

1 – Kulivunjwa ukuta wote wa ndani kwenye upande wa mashariki na kaskazini wa chumbani.

2 – Kulivunjwa takriban 1.84m ya ukuta wa ndani wa kusini katika upande wake wa mashariki hadi kufikia ardhi ya chumba.

3 – Kulivunjwa sehemu ya ukuta wa ndani wa magharibi katika upande wake wa kaskazini hadi chini, na hiyo ni takriban 2.30m.

4 – Kulivunjwa kutoka kwa juu 2.30m takriban ya kile kilichobaki katika kuta mbili za kusini na magharibi.


Na hakukubaki kwenye jengo la chumba cha asili katika kuta mbili za kusini na magharibi isipokuwa kiasi cha ile sehemu iliyosalia.

---

1 Wafaau al-Wafaa 2/401.

Na hakukubaki katika nguzo za chumba isipokuwa mkusanyiko wa ukuta wa kusini-mashariki na mkusanyiko wa ukuta wa magharibi-kaskazini.

## Na umbo liliovunjwa ni kama ilvyo hapa takriban:




1. Urefu wa kubomolewa kuelekea kusini na kaskazini ni 2.30m, na urefu wake kutoka ardhini hadi juu ya ukuta ni 1.84m.
2. Ukuta mzima ulibomolewa.
3. Ukuta ulivunjwa kiasi cha takriban 1.84m.
4. Kulibomolewa sehemu yake kiasi cha takriban 2.30m.
5. Kulivunjwa juu ya ukuta huu kiasi cha takriban 2.30m.

## 2. Ujenzi:

Mnamo tarehe 27 ya mwezi wa shabani mwaka 881 Hijria; walianza kurudisha ujenzi, na wakafanya yanayofuata:

**A) Kuta:**

1 – waliregesha yale waliyoyavunja kwa mawe yale yale ya ukuta wa chumba ambacho walivunja kupitia huko.

2 – waliziba nafasi iliyokuwa kati ya kuta mbili za mashariki za ndani na za nje kwa kuzijenga zikawa zimeshikana.

3 – na vilevile waliziba kati ya kuta mbili za kusini kwa ndani na kwa nje wakaziba vilevile kwa kuzijenga.

4 – waliweka takriban theluthi ya ukuta wa ndani kwa upande wa kaskazini mpana zaidi kuliko ulivyokuwa ili waingize nguzo ambayo iliyokuwa kwenye theluthi yake katika ukuta.

5 – ilifanywa upya sehemu ya chini ya chumba kwa marumaru.

Na wala hawakuweka katika chumba cha Mtume mlango wala dirisha, na hakuna yeyote anayeweza kufikia kaburi la mtume swala na salamu za Allah zimshukie na masahaba zake wawili – kama ilivyokuwa hali hiyo kabla –.

Na unene wa kuta za chumba cha Mtume baada ya kuzibwa kati ya kuta mbili – ukuta wa chumba na ukuta wa pembetano kwa upande wa kusini na upande wa mashariki – ni kama ufuatvyo:

Unene wa ukuta wa kusini kwa upande wa magharibi ni 1.59m, kisha unapanuka unene mpaka unafika 1.82m katika upande wa mashariki.

Na unene wa ukuta upande wa magharibi ni 1.36m.


Na unene wa ukuta wa pembe tatu kwa upande wa mbele wa mashariki na upande wa kaskazini kusini ni 0.63m.

Na unene wa ukuta wa mashariki kwa upande wa kusini ni 1.41m, kisha ukuta huo unazidi kupanuka hadi kufikia 1.72m katika upande wake wa kaskazini.

Na unene wa ukuta wa chumba kwa ndani kwa upande wa kaskazini-magharibi ni 0.73m.

Na unene wa ukuta wa chumba kwa ndani kwa upande wa kaskazini-mashariki ni 1.36m.

**Na huu ndio mchoro wa jengo hilo takriban:**




**B) Sakafu:**

Waliongeza kuba dogo lililotengenezwa kutokamana na mbao juu ya nyumba ya Aisha Allah amridhie badala ya sakafu ambayo iliyotengenezwa kutokamana na mbao, na wakaiweka (kuba) upande wa magharibi kwa mawe meusi, na ikakamilishwa kwa jiwe jeupe, na urefu ni 2.26m, na jumla ya urefu wa ukuta pamoja na kuba ni 8.39m.

Na hakika walimaliza kazi hizi mnamo tarehe 7 ya mwezi wa Shawwal, mwaka 881 Hijria.[1]

**Na umbile la jengo takriban pamoja na sakafu ni hivi:**





1 Wafaau al-Wafaa 2/339, 407, Khulaswat al-Wafaa 2/142.

## ❋ Hatua ya kumi na moja:

Baada ya moto wa pili mnamo mwaka 886 Hijria; mfalme Qaitbay Allah amrehemu alirudi kukiweka marumaru (kuta za) chumba, na akazidisha urefu wake ukafika takriban 3m, vilevile akaweka marumaru sehemu ilio kando yake[1].

**Na hivi ndivyo umbile lake takriban:**




1 Wafaau al-Wafaa 2/181.

## Urefu wa kuta za chumba cha mtume sasa hivi

Baada ya marumaru zilizowekwa na Sultan Qaitbay Allah amrehemu mnamo mwaka 886 Hijria, chumba cha Mtume kilibakia katika hali yake hio, hakikujengwa tena upya, urefu wake ni kama ilivyotangulia kutajwa, ama urefu wa kuta ulizidi baada ya kuwekwa marumaru juu yake, na hakuna yeyote aliyetaja urefu wa chumba cha Mtume - kuta za pembetano - baada ya kuwekewa marumaru juu yake.

**Na urefu wake sasa hivi baada ya kuwekwa marumaru juu yake ni inavofata:**

Urefu wa ukuta wa kaskazini ni 8m.


Urefu wa kwenda juu wa ukuta wa magharibi ni 7.86m, kisha unaelekea upande wa mashariki 1.60m.

Urefu wa ukuta wa pembetatu upande wa kaskazini-magharibi ni 6.60m.

Na urefu wa ukuta wa pembe tatu wa kaskazini mashariki ni 1.45m, kisha sehemu ya nguzo ya duara ilioshikana na ukuta kwa urefu wa 1.50m, kisha unanyooka ukuta kwa upande 4.85m.

Na urefu wa kwenda juu wa ukuta wa mashariki ni 5.66m.

**Na umbile lake liko hivi:**



# Uzio wa nje

Baada ya kuta zilizotajwa hapo juu: kuna kizuizi cha nje kilichotengezwa na shaba upande wa kusini - na kizuizi hiki ndicho ambao watu husimama karibu nacho leo wanapokuja kumsalimia Mtume swala na salamu za Allah zimshukie na wenzake wawili, na pia kuna kizuizi cha chuma kwenye pande nyingine zilizobaki, na juu yake kuna ukanda wa shaba.

**Uzio huu wa nje umepitia hatua kadhaa:**

1 – Mnamo mwaka wa 668 Hijria, katika utawala wa mfalme Al-Dhwaahir Biibars; aliweka ukuta wa mbao kukizunguka chumba baada ya kuta za awali zilizojengwa na al-Waliid ibnu Abdulmalik, wenye urefu wa 3.5m.

2 – Mnamo mwaka wa 694 Hijria, katika utawala wa mfalme mwadilifu Zainud-Diin Kitbugha Allah amrehemu; aliongeza ukuta wa mbao uliozunguka ukuta wa mbao.

3 – Mnamo mwaka wa 886 Hijria; Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie ulichomeka moto na hizi kuta mbili za mbao ziliungua pamoja nao, kwa hivyo mfalme Qaitbay Allah amrehemu aliweka ukuta kizuizi wa shaba upande wa Kibula, na pande nyingine zilizobaki aliweka ukuta kizuizi wa chuma uliopigwa rangi ya kijani, na akaweka juu yake ukanda wa shaba.

4 – Katika zama za Sultan wa Ottoman Abdul Majiid Khan - ambaye alianza upanuzi wa Msikiti wa Mtume mwaka wa 1265H na kumaliza mwaka wa 1277 Hijria - alifanya upya kizuizi cha shaba kilicho upande wa kusini. Hicho ndicho kizuizi ambacho watu husimama mbele yake leo kwa ajili ya kumsalimia Mtume swala na salamu za Allah zimshukie na wenzake wawili Allah awaridhie.

Kizuizi hicho cha nje bado kipo hadi sasa [1].

---

1 Wafaau al-Wafaa 2/387, Ad-Durratu ath-Thamiinah 2/360, At-Ta'rif uk. 39, Tahqiiq an-Nusra uk. 85.

**Kizuizi hicho kimekusanya maeneo yafuatayo:**

A) Chumba cha Aisha Allah amridhie.

B) Uani kwa Aisha Allah amridhie.


C) Sehemu ya nyumba ya Hafswa Allah amridhie.

D) Sehemu ya Rawdha.

E) Nyumba ya Fatima Allah amridhie.

F) Eneo wazi upande wa mashariki.


**Umbo la uzio wa nje pamoja na kuta alizozijenga Al-Waliid inakaa hivi:**



# Uzio wa Shaba na sehemu ilioko chumba cha Mtume ndani yake

Chumba cha Mtume: Kinapatikana upande wa kusini-mashariki wa ukuta wa shaba, na kuta za chumba cha Mtume zimepotoka kuelekea mashariki; ili zisilingane na Kibula, na masafa yalioko baina ya kuta za chumba na uzio wa shaba zatofautiana; sawa iwe katika upande mmoja au katika pande nyingine.

**Masafa baina ya kuta za chumba cha Mtume na uzio wa shaba kwenye mchoro ni kama ifuatavyo:**



## Masafa yalioko kati ya mtu anayemsalimia Mtume swala na salamu zimshukie na kaburi lake

Ikiwa mtu atakuja kumsalimia Mtume swala na salamu za Allah zimshukie kutakuwa na umbali kati yake na kaburi la Mtume swala na salamu za Allah kama ifuatavyo:

1 – Eneo wazi la urefu wa 0.92m ambamo husimama ndani yake waongozi ili kurahisisha mapito ya watu wakati wanapomsalimia Mtume swala na salamu za Allah zimshukie na wenzake wawili Allah awaridhie.

2 – Uzio wa shaba wenye urefu wa 0.10m.

3 – Eneo wazi baina ya ukuta wa shaba na ukuta wa pembetano: 4.14m.

4 – Ukuta wa pembetano, na upana wake ni 0.63m.

5 – Eneo wazi baina ya ukuta wa pembetano na ukuta wa chumba, kisha kulifungwa kati yao, na upana wake ni 0.25m.

6 – Ukuta wa chumba, na upana wake ni 0.73m.


7 – Eneo wazi baina ya ukuta wa chumba na kaburi: 0.23m.

8 – Kisha kuna kaburi la Mtume, swala na salamu za Allah zimshukie.

Kisha kuna kaburi la Mtume. Kwa hivyo, baina ya mtu anayetaka kumsalimia Mtume swala na salamu za Allah zimshukie na kaburi lake, kutakuwa na mita saba (7m).

Na Mtume wa Allah amechaguliwa na Allah kwa kumwekea malaika wanaomfikishia salamu za waumini, Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Na nifikishieni swala na salamu zenu, kwani salamu zenu zinanifika popote mlipo**». Imepokewa na al-Maqdisi katika Al-Mukhtarah. Ikiwa mtu anayemsalimia yu karibu na kaburi lake au mbali, yote ni sawa. Amesema al-Hasan ibnu al-Hasan Allah amrehemu: «Hamkuwa nyinyi na wale walioko Andalusia isipokuwa mko sawa (katika kumswalia mtu)».

**Na maelezo ya umbali baina ya mtu anayemsalimia Mtume na kaburi lake swala na salamu za Allah zimshukie kwenye mchoro ni kama ifuatavyo:**



## Masafa yalioko baina ya uzio wa shaba wa kushoto na kaburi la Mtume swala na salamu zimshukie

Umbali kati ya kizuizi cha shaba upande wa kushoto -yaani, kinyume cha mahali pa kumsalimia Mtume swala na salamu za Allah zimshukie- na kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie ni kama ifuatavyo:

1 – Kabati la shaba liliothibiti hapo liwekwalo ndani yake misahafu: 0.23m.

2 – Kizuizi cha shaba upande wa kaskazini: 0.10m.

3 – Eneo wazi lenye urefu wa 7m.

4 – Ukuta mwingine 0.10m.

5 – Eneo wazi lenye urefu wa 2.53m.

6 – Ukuta wenye unene wa 0.63m.

7 – Nafasi ndani ya pembetatu yenye urefu wa 2.68m.

8 – Ukuta wenye unene wa 0.63m.

9 – Nafasi ndani ya chumba cha Mtume swala na salamu za Allah zimshukie yenye urefu wa 2.60m.


10. Kisha katikati ya kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie: 0.50m.

Jumla ya umbali kati ya mtu anayesimama nyuma ya ukuta kizuizi wa kushotoni hadi kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie ni 17m.

Na yeyote anayedai fadhila ya kuelekea kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie katika mahali hapa hakupata lengo lake, kwani kati yake na kati ya kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie kuna umbali mrefu na kuta zinazozuia kulifikia.

Na mtu kukusudia kulielekea kaburi anaposwali, atakuwa amekwenda kinyume na sheria; kwani Allah aliamuru kuielekea Al-Kaaba.

**Na maelezo ya hayo katika mchoro ni kama ifuatavyo:**



## Je inawezekana kuingia kwenye chumba cha Mtume?

Kizuizi cha shaba kina mlango kwenye upande wake wa mashariki-kaskazini. Yeyote anayeingia kupitia mlango huo atafika kwenye ukuta wa pembetano ambao una pazia. Hata hivyo, haiwezekani kufika kwenye makaburi au kuyaona kutokana na kuwepo ukuta wa pembetano, na pia nyuma yake kuna ukuta wa chumba unaoambatana nao. Na kuta zote mbili hazina mlango au dirisha.

Na yeyote aliyesema kwamba ameingia kwenye chumba cha Mtume, ina maana kwamba aliingia nyuma ya kizuizi cha shaba na kufikia mpaka kwenye ukuta wa pembetano tu.

## Hekima ya kuta na vizuizi vya shaba

**Hekima ya hizi kuta:** ni kulinda kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie kulifikia yeyote, Mtume swala na salamu za Allah zimshukie kwani amekataza lifanywe kaburi lake idi, alisema: «**musifanye kaburi langu kuwa ni idi**». Imepokewa na Ahmad. Na akabainisha swala na salamu za Allah zimshukie hekima ya hili nayo ni asiabudiwe pasi na Allah, akasema: «**Ewe Allah! Nakuomba usilifanye kaburi langu ni sanamu lenye kuabudiwa**» Imepokewa na Maalik. Allah akaitikia dua ya Mtume wake swala na salamu za Allah zimshukie, kwa kuwa hakuna yeyote anayeweza kufika kwenye kaburi lake.

Na lau mmoja atataka kuswali kuelekea makaburi hayo hangeweza, kwa sababu limezungukwa kwa kuta za pembetatu kwa upande wa kaskazini, na huu ukuta wa pembe tatu ameuashiria Ibnul Qayyim Allah amrehemu katika kauli yake:

*Akajibu mola wa viumbe wote dua yake,*

*na akalizungusha kwa kuta tatu*[1]

Na baada ya hizi kuta vizuizi vya shaba; kati ya mwenye kuyaelekea makaburi kuna masafa makubwa -kama ilivyotangulia-.

1 Nuuniyyatu ibnul Qayyim nambari ya beti 4042.

# Sakafu ya Nyumba na Kuba

Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alifariki dunia katika nyumba ya Aisha Allah amridhie, na kuzikwa humo, Ukuta wa nyumba yake ulikuwa wa udongo na paa lake lilikuwa la majani ya mtende, katika mwaka wa 88 Hijria, katika utawala wa al-Waliid ibnu Abdulmalik Allah amrehemu alijenga upya nyumba yake kwa mawe na akafanya paa lake kuwa la mbao na kuizungushia ukuta wa pembe tano, hakukuwa na kuba iliyoelekea nyumba ya Mtume swala na salamu za Allah zimshukie katika zama za Masahaba, Tabiina, na Tabii Tabiina, ilivumbuliwa baada yao kwa karne nyingi.

## ❋ Sakafu ya Nyumba:

Sakafu ya nyumba ya Mtume swala na salamu za Allah zimshukie ilipitia hatua kadhaa:

1 – Alipokuwa akijenga Mtume swala na salamu za Allah zimshukie msikiti wake baada ya kuhama kwake kwenda Madina; alijenga nyumba ya Aisha Allah amridhie pamoja nao, na akafanya paa la msikiti na nyumba ya Aisha Allah amridhie paa la majani ya mitende.

2 – Katika mwaka wa 88 Hijria; Umar ibnu Abdul-Aziz Allah amrehemu kwa amri ya Khalifa al-Waliid ibnu Abdulmalik Allah amrehemu alibomoa nyumba ya Aisha Allah amridhie, na akaijenga upya kwa mawe, na akafanya paa lake kuwa la mbao.

3 – Katika mwaka wa 881 Hijria; Mfalme Qaitbay al-Mamluki Allah amrehemu aliunda kuba ndogo ya mbao juu ya nyumba ya Aisha Allah amridhie badala ya paa la mbao.

4 – Katika mwaka wa 1228 Hijria; Sultan wa Ottoman Mahmud wa Pili Allah amrehemu aliifanyia ukarabati kuba hili.

## ❋ Kuba Kubwa:

Kuba hili liko juu ya kuba dogo iliyo juu ya nyumba ya Aisha Allah amridhie -iliyotajwa hapo awali-.

**Kuba hili limepitia hatua kadhaa:**

1 – Mnamo mwaka wa 678 Hijria, Mfalme Qalawun al-Swaalihi Allah amrehemu aliunda kuba liliyoelekea nyumba ya Aisha Allah amridhie - na yeye ndiye aliyeianzisha -, na lilikuwa la mbao na juu yake kulikuwa na mbao za risasi.

2 – Mnamo mwaka wa 881 Hijria, Sultan Qaitbay al-Mamluki Allah amrehemu alilifanyia ukarabati kuba hili.

3 – Mnamo mwaka wa 886 Hijria, kuba lilichomeka.

4 – Mnamo mwaka wa 887 Hijria, Sultan Qaytbay al-Mamluki Allah amrehemu alilijenga upya baada ya kuchomeka.

5 – Mnamo mwaka wa 1233 Hijria, Sultan Mahmud wa Pili wa Ottoman Allah amrehemu alibomoa sehemu za juu za kuba lilio juu, na kulijenga upya, na akalipaka rangi ya buluu.

6 – Mnamo mwaka wa 1253 Hijria, Sultan Mahmud wa Pili wa Ottoman Allah amrehemu aliagiza kuba la nje lipakwe rangi ya kijani.[1]

**Chini ya kuba kubwa iliyopo sasa ni yafuatayo:**

A) Nyumba ya Aisha Allah amridhie, na sehemu kubwa ya chumba chake.

B) Sehemu ya nyumba ya Hafswa Allah amridhie iliyopo upande wa kusini wa nyumba ya Aisha Allah amridhie, ambayo sasa ni eneo ndani ya kizuizi.

C) Mita 3 karibu na Rawdha kwa upande wa magharibi wa nyumba ya Aisha Allah amridhie.


---

1 Al-Durratu ath-Thamiinah 2/394, Taarikh Makkah wa Al-Madina 1/329, Ar-Rihlat Al-Hijaziyya uk. 245, Khulaswat Al-Wafaa 2/142, Nuzhatun-Nadhiriin uk. 77.

D) Eneo la ukubwa wa mita moja takriban kwa upande wa mashariki wa nyumba ya Aisha Allah amridhie.

Na kuba hili halipo katikati ya nyumba ya Aisha Allah amridhie, bali inaelekea upande wa magharibi na kusini, nyumba ya Aisha Allah amridhie iko chini ya kuba kwa upande wa mashariki-kusini, ndiyo sababu wanazuoni wanasema kwamba inalingana na nyumba ya Aisha Allah amridhie.

## **Na hili ndilo umbo lake takriban:**



# Kaburi la Mtume swala na salamu zimshukie na wenzake wawili Allah awaridhie hayajaonekana isipokuwa mara mbili

Baada ya kufungwa mlango wa Aisha Allah amridhie baada ya kifo chake, makaburi haya hayakuonekana tena baada ya hapo isipokuwa mara mbili:

**Mara ya kwanza:** Mnamo mwaka wa 88 Hijria katika utawala wa Al-Waliid ibnu Abdulmalik Allah amrehemu, wakati alipobomoa ukuta wa chumba cha Mtume, na akakijenga upya na kuongeza ukuta wa pembetano nyuma yake.

**Mara ya pili:** Mnamo mwaka wa 881 Hijria; wakati Sultan Qaitbay Allah amrehemu, alipoamuru kubomolewa ukuta wa ndani wa chumba na sehemu ndogo ya ukuta wa nje wa pembetano. Wakaingia baadhi ya watu wa Madina kwenye chumba cha Mtume kwa ajili ya kujenga ukuta na kusafisha chumba cha Mtume kutokana na athari za moto miwili iliyoifikia Msikiti wa Mtume.

Yaani: Lilibaki kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie na wenzake wawili Allah awaridhie, hakuna mtu yeyote aliyeyaona kwa miaka 793 -kutoka mwaka wa 88 hadi 881 Hijria-.

Na walipoingia kwenye chumba cha Mtume, hawakuona sehemu yoyote ya makaburi iliyoinuliwa juu ya ardhi; lakini walipata ardhi ikiwa sawasawa. Amesema As-Samhuudi Allah amrehemu -na alikuwa miongoni mwa wanazuoni wa Madina walioiona kaburi mwaka wa 881 Hijria-: «Nilikitazama kwa kina chumba kitukufu; basi nikaona kuwa ni ardhi iliyo sawa, wala sikupata athari yoyote ya makaburi matukufu»[1].

Kwa hivyo, As-Samhuudi Allah amrehemu na wale waliokuwa naye katika kujenga kuta, walijitahidi kutafuta mahali

1 Wafaau al-Wafaa, 2/404.

pa makaburi, na wakaweka vijiwe kwenye maeneo matatu, ambayo baada ya utafiti waliona kuwa ndio maeneo ya makaburi matatu kwa mujibu wa yale waliyoyasoma kuhusu maelezo ya mahali pa makaburi[1].

Na tangu mwaka huo hadi sasa, hakuna yeyote aliyeona makaburi hayo.

1 Wafaau al-Wafaa 2/408.

# Je inafaa kujipangusa na ukuta wa chumba cha Mtume?

Ukuta wa chumba cha Mtume ni miongoni mwa vitu visivyo na uhai, hivyo basi haifai kujipangusa nao. Amesema Abu Hamid Al-Ghazaaliy Allah amrehemu: «Hakika kugusa na kubusu makaburi ni desturi ya Wakristo na Mayahudi»[1].

Kwa hivyo, haijuzu kujipangusa na ukuta wa chumba cha Mtume, au mihirabu, au mimbari, au nguzo, au milango, au kuta, au kuyabusu; kwa sababu hiyo ni njia inayopelekea kwenye ushirikina na sababu ya kufikia huko.

1 Asraar al-Hajj, uk. 157.

# Kutabaruku

Kutabaruku: ni kutaka baraka, na kuitarajia, na kuitakidi.

Na Allah aliyetakasika yeye ndio mwenye kubariki, kama alivyosema Allah aliyetukuka:

﴿تَبَٰرَكَ ٱلَّذِي بِيَدِهِ ٱلۡمُلۡكُ﴾

«Ametukuka ambaye mkononi mwake umo Ufalme» [Al-Mulk: 1].

Na baraka inapatikana kutoka kwa Allah alietukuka; na inatakwa kutoka kwake alietakasika kwa dua - kama kauli yako kusema: «Ewe Allah nibarikie katika jambo fulani». Vilevile baraka inapatikana kwa kutii, basi kila mja anapojikurubisha kwa Allah ndipo baraka inampata.

Na kutabaruku kunagawanyika mara mbili: kulikoruhusika kisheria na kulikokatazwa:

## ❋ Kigawanyo cha kwanza: Kutabaruku kwa njia ya kisheria,

Nako ni kule kulikopokelewa katika sheria, na katika mifano yake ni:

1. **Kutabaruku na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie katika maisha yake:**

Inafaa kutabaruku na mwili wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, au kitu alichokigusa, au kitu twahara kilichotokana naye.

Mfano jasho lake, kama alivyochkua Ummu Suleym Allah amridhie jasho lake alipolala kwake ili atabaruku nalo na aliweka kwenye marashi yake. Ameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

Na mfano wa nywele zake, kama alivyokua Mtume swala na salamu za Allah zimshukie akiwapa masahaba nywele zake katika hija yake ya kuaga. Imepokewa na Muslim.

Na mfano wa kutabaruku na nguo zake, kama alipompatia kikoi chake yule aliyemuosha binti yake Zainab Allah amridhie na akasema: «**Mfunikeni nacho, iwe nguo yake ya chini inayogusa mwili**». Wamefikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

Na sahii hakupatikani chochote katika nywele zake au nguo zake, na yale wanayoyadai baadhi ya watu kwa kupatikana baadhi ya nywele zake, au upanga wake, au nguo yake ya vita, au yasiokua hayo, hayo hayajathibiti.

2. **Yale yaliokuja kwa dalili kwamba kunapatikana baraka ndani yake kwa njia ya kisheria, na miongoni mwa hayo:**

A) Katika vinywaji – maji ya Zamzam.

B) Katika nyakati – usiku wa Laylatul qadr.

## ❋ Kigawanyo cha pili: Kutabaruku kulikokatazwa,

na miongoni mwa hayo ni:

1. **Kutabaruku na yale yanayonasibishiwa na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie leo hii katika athari:**

Haifai kutabaruku na chochote katika athari hizo; kwa sababu ya kutothibiti athari hizo kuwa ni za Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

2. **Kutabaruku na watu wema:**

Kinachotoka kwenye mwili wa muumini haifai kutabaruku nacho; kwa sababu masahaba hawakua wakitabaruku na nguo au kinachotoka miongoni mwa jasho au nywele za yeyote katika makhalifa waongofu au wengineo katika masahaba.

**3. Kutabaruku kwa kupitia miti na mawe:**

Kutabaruku na miti, mawe na mfano wa hayo; hili ni kumshirikisha Allah, sawa iwe ni mawe ya Madina au mchanga wake au vyenginevyo, amesema Allah aliyetukuka:

﴿أَفَرَءَيۡتُمُ ٱللَّٰتَ وَٱلۡعُزَّىٰ ۞ وَمَنَوٰةَ ٱلثَّالِثَةَ ٱلۡأُخۡرَىٰٓ﴾

«Je! Mmemuona Lata na Uzza, ۞ Na Manaat, mwingine wa tatu?» [An-Najm: 19-20].

Na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alipita kwa watu wanaoangika silaha zao juu ya mti wa mkunazi, wakitabaruku na mti huo. Baadhi ya waliokua naye wakasema -katika wale waliosilimu karibuni-: «Ewe Mtume wa Allah! tufanyie nasi kitu cha kuangikia kama ambavyo wao wanacho kitu cha kuangika!» Mtume swala na salamu za Allah zimshukie akasema: «**Allahu Akbar! Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu iko mkononi kwake, mumesema kama walivyosema Banuu Israil kumwambia Musa:**

﴿ٱجۡعَل لَّنَآ إِلَٰهٗا كَمَا لَهُمۡ ءَالِهَةٞۚ﴾

**«Tufanyie wa kuabudu kama walivyokua na waabudiwa» [Al-A'raaf: 138].**

**Mtafuata njia za waliokua kabla yenu!**» Imepokewa na At-Tirmidhi.

Ama kupangusa nguo ya Al-Kaaba, mihirabu au mimbari, vilevile kuwapangusa wanachuoni na watu wema, kwa njia ya upendo sio kwa kutabaruku; – hili ni jambo la haramu; kwa sababu ni njia ya kupelekea katika shirki.

Na kulibusu Al-Hajar al-Aswad (jiwe jeusi) sio kwa ajili ya kutabaruku na jiwe hilo, bali ni katika njia za kumuabudu Allah, kama alivyosema Umar Allah amridhie: «Naapa kwa Allah, hakika yangu mimi najua wewe ni jiwe haudhuru wala hanufaishi,

na lau kama mimi nisingemuona Mtume swala na salamu za Allah zimshukie akikubusu nisingekubusu». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

❖❖❖

# Kuzuru Kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie na wenzake wawili Allah awaridhie

# Mtume wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie

Yeye ni mjumbe wa Allah, Muhammad Ibnu Abdullah Ibnu Abdul-Muttwalib Ibnu Hashim, kutoka katika kizazi cha Ismail Ibnu Ibrahim kipenzi cha Allah. Alizaliwa Makkah na akainukia akiwa yatima wa wazazi wawili, akakulia katika umbile la Uislamu, na Allah alimtunuku tabia njema kabisa.

Alikuwa akikaa na watu kwa uzuri, akiwaheshimu wazee na kuwa mnyenyekevu kwa vijana, mwenye ulimi uliotakasika na maovu. Hakuwahi kumdhulumu yeyote wala kumdanganya yeyote, wala kumpiga yeyote kwa mkono wake. Mkono wake haukumgusa mwanamke yeyote asiye halali kwake.

Allah alimtumiliza alipokuwa na umri wa miaka arobaini. Ndipo watu wake walipomuudhi kwa maneno na vitendo, wakamtuhumu kwa wazimu na uchawi, na wakamtaja kuwa ni mwongo. Wakapigana naye katika vita kadhaa, na Mayahudi walimwekea sumu kwenye chakula chake na wakamroga.

Alipewa mtihani mkubwa katika maisha haya; kwani watoto wake sita na wake wawili walikufa katika maisha yake. Na alikuwa akipitiwa na mwezi mmoja au miwili hali ya kuwa hakuna moto uliowashwa nyumbani kwake (kupikia chakula), na akikaa masiku ya kufuatana akiwa na njaa na familia yake wasipate chakula cha jioni.

Allah alimchagua kwa kumpa fadhila kadhaa, Miongoni mwazo ni: kuwa amesamehewa madhambi yake yaliyopita na yajayo, ni wa kwanza atakayefufuliwa siku ya Kiyama, ni muombezi wa kwanza na wa kwanza atakayekubaliwa uombezi wake Siku ya Kiyama, ni Nabii mwenye wafuasi wengi zaidi, ni wa kwanza atakayevuka Swiraat (daraja lembamba kuliko unywele juu ya Moto wa Jahanamu) na wa kwanza atakayebisha mlango wa Pepo.

Tangu kupewa utume hadi kufa kwake, alikuwa akilingania kuabudiwa Mola wake na akikataza umma wake na ushirikina,

akiamrisha kila kheri na akikataza kila shari. Haidaii nafsi yake chochote katika yale yasiomilikiwa ila na Allah. Amesema Allah aliyetakasika:

﴿قُل لَّآ أَمۡلِكُ لِنَفۡسِي نَفۡعٗا وَلَا ضَرًّا﴾

«Sema: Siimilikii nafsi yangu manufaa wala madhara» [Al-Aaraaf: 188].

Nyakati zake zote zimeimarishwa katika kumtii Allah:

﴿قُلۡ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحۡيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ ٱلۡعَٰلَمِينَ * لَا شَرِيكَ لَهُۥۖ﴾

«Sema: Hakika Swala yangu, na ibada zangu, na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Allah, Mola Mlezi wa viumbe vyote, hana mshirika wake» [Al-An'aam: 162-163].

Na yeye ni mja wa Allah, alikuwa mgonjwa, alihisi njaa, alihuzunika na alifariki, na wala hana sifa zozote za uola na uungu; kwa hivyo haombwi wala hatakwi mahitaji, kwa sababu yeye hamiliki hayo. Amesema Allah aliyetakasika:

﴿قُلۡ إِنَّمَآ أَنَا۠ بَشَرٞ مِّثۡلُكُمۡ يُوحَىٰٓ إِلَيَّ أَنَّمَآ إِلَٰهُكُمۡ إِلَٰهٞ وَٰحِدٞۖ فَمَن كَانَ يَرۡجُواْ لِقَآءَ رَبِّهِۦ فَلۡيَعۡمَلۡ عَمَلٗا صَٰلِحٗا وَلَا يُشۡرِكۡ بِعِبَادَةِ رَبِّهِۦٓ أَحَدَۢا﴾

«Sema: Mimi ni mwanaadamu kama nyinyi. Ninaletewa Wahyi ya kwamba mwabudiwa wenu (wa haki) ni mwabudiwa mmoja (pekee). Basi anayetarajia kukutana na Mola wake basi afanye matendo mema na wala asimshirikishe na yeyote katika ibada ya Mola wake» [Al-Kahf: 110].

Na hakika anayemiliki hayo (ya kunufaisha na kudhuru) ni Mola Mlezi wa viumbe wote. Amesema Allah aliyetakasika:

﴿وَإِن يَمۡسَسۡكَ ٱللَّهُ بِضُرّٖ فَلَا كَاشِفَ لَهُۥٓ إِلَّا هُوَۖ وَإِن يُرِدۡكَ بِخَيۡرٖ فَلَا رَآدَّ لِفَضۡلِهِۦ﴾

«Na Allah akikuletea madhara, basi hakuna wa kukuondolea (madhara hayo) ila Yeye. Na akikutakia kheri, basi hakuna awezaye kuzuwia fadhila yake» [Yunus: 107].

## Abu Bakr As-Swiddiiq Allah amridhie

Yeye ni khalifa wa Mtume wa Allah, Abu Bakr As-Swiddiiq, na jina lake ni Abdullah Ibnu Uthmaan Ibnu Aamir Al-Qurashiy, Allah amridhie.

Na sababu ya kuitwa «As-Swiddiiq» (mkweli); ni kuwa aliharakisha kumsadikisha Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie, na akashikamana na ukweli, wala haukusajiliwa urongo wowote kutoka kwake.

Yeye ni wa kwanza wa Makhalifa waongofu, ni wa kwanza kati ya kumi waliobashiriwa Pepo, ni wa kwanza aliyeamini miongoni mwa wanaume. Ndiye mkamilifu zaidi katika masahaba na mbora wao, ni shujaa zaidi, mwerevu zaidi, mjuzi zaidi, na mwenye kutangulia mbele zaidi kati yao katika mambo ya kheri. Alitumia mali yake yote katika njia ya Allah, na hakuwahi kuabudu sanamu katika maisha yake. Alikuwa mwenye kumliwaza Mtume swala na salamu za Allah zimshukie katika nyakati za shida. Alikuwa na mtume peke yake pangoni, na akahama pamoja naye. Na ndiye sahaba aliyemlazimu zaidi Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

Hakuna katika masahaba hata mmoja ambaye baba yake, mama yake, watoto wake na wajukuu zake walisilimu wote, na wakamdiriki Mtume isipokuwa yeye tu.

Amesema Sheikhul Islaam Allah amrehemu: «Basi wao ni watu wa nyumba ya Imani, hakuna miongoni mwao mnafiki, wala hakujulikani katika masahaba mfano huu isipokuwa kwa nyumba ya Abu Bakr»[1].

Lau imani yake ingepimwa dhidi ya imani ya umma huu ikiwa Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie hayumo ndani yao basi angewashinda. Alikuwa akisoma Qur'ani hawezi kujizuwia na machozi, na watu hawawezi kusikia kisomo chake kwa ajili ya (wingi wa) kilio.

1 Minhaaj al-Sunnah al-Nabawiyyah 8/332.

Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie alimpenda sana, akamuoa binti yake Aisha Allah amridhie, na ndiye aliyekua akimpenda zaidi kati ya wake zake.

Yeye ndiye wa kwanza katika umma huu kuingia Peponi baada ya Mtume wake, Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amesema: «**Ama wewe, ewe Abu Bakr, ndiye wa kwanza kuingia Peponi katika umma wangu**». Imepokewa na Abu Dawud. Bali ataitwa katika milango minane ya Pepo.

Kuwapenda masahaba ni katika kumpenda Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, na masahaba wanaona kuwa kumpenda Abu Bakr ni katika Ibada. Amesema Jabir Ibnu Abdullah, Allah awaridhie wote wawili: «Kumpenda Abu Bakr na Umar ni katika Imani». Na yeyote anayewapenda watu atafufuliwa pamoja nao.

## Umar ibnu Al-Khattwaab Allah amridhie

Naye ni kiongozi wa waumini Al-Faaruuq Umar ibnu al-Khattwaab ibnu Nufail Al-Qurashi Allah amridhie.

Alimrithi uongozi Abu Bakr na ni rafiki yake Allah awaridhie, ni wa pili katika makhalifa waongofu, na ni mmoja kati ya kumi waliobashiriwa pepo, alikuwa anapendwa zaidi na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie baada ya Abu Bakr, amesema Ash-Shaafi'iy Allah amrehemu: «Hawajatofautiana yeyote katika masahaba wala katika Taabiina waliokuja baada ya masahaba katika kumfadhilisha Abu Bakr na Umar Allah awaridhie, na kuwatanguliza kuliko masahaba wote»[1].

Alikuwa akiwafundisha masahaba Qur-ani, na akipokezana na mmoja katika Answaar kwenye vikao vya Mtume swala na salamu za Allah zimshukie; ili isimpite chochote katika elimu, alikuwa mwenye kutukuzwa mwenye nguvu katika dini ya Allah shetani akimkimbia, amesema Mtume swala na salamu za Allah zimshukie: «**Ewe Ibnu al-Khattwaab, naapa kwa yule ambaye nafsi yangu iko mkononi kwake! Hajakupata shetani kabisa ukiwa umeshika njia flani isipokuwa yeye atashika njia isiyokua njia yako**». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

Allah ameinusuru dini kupitia yeye na ikaweza kuenea katika miji ya mbali, na umoja wa waislamu ukawa na nguvu. Amesema Sheikhul Islaam Allah amrehemu: «Na katika zama zake ulienea uislamu, na ukatokeza kwa namna ambayo haujatokeza kabla yake mfano wake»[2]. Alikuwa shujaa wa mbele katika vita, wafalme wa Fursi na wa Roma walimuogopa, na likaekwa taji la Kisraa mbele yake.

Alikuwa ni mwenye kuipa mgongo dunia, mwenye kuielekea Akhera, nakshi ya pete yake ilikuwa imeandikwa: «Yatosheleza

1 Al-I'tiqaad cha al-Bayhaqiy, nambari 356.

2 Minhaaj al-Sunnah al-Nabawiyyah 10/182.

mauti kua ni mawaidha ewe Umar». Alifungua Baitul Maqdis na akaondoa uchafu kwa nguo yake. Ibnu Kathiir Allah amrehemu amesema: «Alikuwa ni mnyenyekevu kwa ajili ya Allah, maisha magumu, chakula cha shida, mkali kwa mambo ya Allah, akishona nguo kwa ngozi iliopakwa rangi,na anabeba kiriba (chombo) kwa mabega yake, pamoja na ukubwa wa cheo chake»[1].

Abu Bakr as-Swiddiiq alikuwa anampenda, amesema Abu Bakr Allah amridhie: «Hakuna juu ya mgongo wa ardhi mtu anayependeza zaidi kwangu kuliko Umar».

1 Al-Bidaayah wa an-Nihaayah 10/182.

# Kuelezea kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie na wenzake wawili Allah awaridhie

Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alikufa mwaka wa 11 Hijria katika nyumba ya Aisha Allah amridhie, na akazikwa humo ndani ya nyumba. Kichwa chake kiko sehemu ya ukuta wa upande wa magharibi, ambapo umbali wake mpaka kufikia ukuta huu ni takriban 0.93m, na uso wake uko upande wa Kibula na umbali wake kutoka upande wa Kibula ni 0.23m [1].

Na baada ya kufa kwake kwa miaka miwili alikufa rafiki yake Abu Bakr as-Swiddiiq Allah amridhie, kisha akazikwa nyuma ya Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, na kichwa chake kiko upande wa miguu ya Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

Na katika mwaka wa 23 Hijria, Umar ibnu al-Khattwaab Allah amridhie alikufa, na kuzikwa nyuma ya Abu Bakr as-Swiddiiq Allah amridhie, na kichwa chake kiko upande wa miguu ya Abu Bakr as-Swiddiiq Allah amridhie.

**Na namna ya makaburi ni hivi:**

Kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie

Kaburi la Abu Bakr as-Swiddiiq Allah amridhie

Kaburi la Umar ibnu al-Khattwaab Allah amridhie

1 Fataawaa Sheikhul Islaam 26/146, Wafaau al-Wafaa 2/170-173.

# Je Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alizikwa msikitini?

Mtume swala na salamu za Allah zimshukie hakuzikwa msikitini, bali yeye swala na salamu za Allah zimshukie alikufa katika nyumba ya Aisha Allah amridhie, na akazikwa humo ndani, na nyumba ya Aisha Allah amridhie iko upande wa mashariki ya msikiti wa Mtume, na baada ya kufa makhalifa waongofu na masahaba wote waliokua Madina, msikiti wa Mtume ukapanuliwa upande wa mashariki, nyumba ya Aisha Allah amridhie ikaingia msikitini, wakadhani baadhi ya watu kuwa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alipokufa masahaba walimzika msikitini, na ufafanuzi wa hayo ni kama inavyofuata:

1. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amekataza kufanya makaburi kua ni miskiti, na akamlaani mwenye kufanya hivyo, na akaeleza ya kwamba, miongoni mwa watu waovu ni yule anayefanya makaburi kuwa misikiti, na hilo inakusanya pia kuingiza makaburi misikitini, kujenga misikiti juu ya makaburi, au kukusudia kuswali makaburini au kuyaelekea makaburi.

2 - Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alieleza kua manabii wanazikwa sehemu walizokufia, akasema: «**Allah hajamchukua nabii yeyote isipokuwa sehemu ambayo alipenda azikwe hapo**». Imepokewa na Ahmad.

3 – Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alikufa katika nyumba ya Aisha Allah amridhie, na akazikwa humo ndani; kwa sababu kila Nabii huzikwa sehemu anapokufia, kama ambavyo kuzikwa nyumbani kwake ni njia ya kukata mlango wa kushikamana na kaburi lake, na kuvuka mipaka kwake yeye, kama alivyosema Aisha Allah amridhie: «Mtume swala na salamu za Allah zimshukie - katika maradhi yake ambayo hakuweza kusimama tena (alikufa nayo) alisema: **“Allah awalaani Mayahudi na Manaswara, walifanya makaburi ya manabii wao kua ni miskiti”**». Alisema (Aisha): «Lau sio hivyo lingedhihirishwa kaburi lake, isipokuwa tu iliogopewa lifanywe

kuwa msikiti». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

4 – Nyumba ya Aisha Allah amridhie ambayo alizikwa humo Mtume swala na salamu za Allah zimshukie ilibaki kuwa ni jirani ya msikiti, pamoja na kuwa upanuzi wa msikiti ulikua mwingi zama za makhalifa wawili waongofu Umar ibnu al-Khattwaab na Uthmaan ibnu Affaan Allah awaridhie.

5 – Katika mwaka wa 88 Hijria, baada ya kufa Masahaba wote waliokua Madina; Khalifa wa dola ya Umawiyyah al-Waliid ibnu Abdulmalik Allah amrehemu aliamrisha kupanuliwa msikiti na kuingiza vyumba ndani ya msikiti, akasimamia hilo kiongozi wa Madina wakati huo Umar ibnu Abdul-Aziz Allah amrehemu.

6 – Nyumba ziliingizwa katika upanuzi kwa dharura, na haikua makusudio yao kutukuza chumba kwa wao kufanya hivyo, lakini walikusudia kupanua msikiti, kikaingia kile chumba kama mfano vyengine vilivyoingia katika upanuzi, amesema Sheikh Muhammad bin Abdul-wahhab Allah amrehemu: «Waliingiza nyumba katika msikiti kwa ajili ya upanuzi wa msikiti, hawakukusudia kukitukuza chumba kwa hilo, lakin walikusudia kupanua msikiti»[1].

7 – Na pamoja na haya, wanachuoni wema waliotangulia na wanachuoni wa Madina walipinga kitendo hiki - kwa mfano Sai'id ibnu Al-Musayyib, Abaan ibnu Uthman, na Khubeib ibnu Abdullah ibnu Az-Zubeyr-. Amesema U'rwa Allah amridhie: «Nilimjadili Umar ibnu Abdul-Aziz kuhusu kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie lisiwekwe kwenye msikiti, na nikagombana naye sana, lakini akakataa na kusema: “Barua (yenye maagizo) ya Amirul Muuminin hakuna budi lazima itekelezwe”»[2]. Na alisema Sheikh Muhammad ibnu Abdul-Wahhab Allah amrehemu: «Na pamoja na haya, wanachuoni wa Madina walimpinga mpaka kufikia Khubeib ibnu Abdullah ibnu

1 Ad-Durar as-Saniyyah 5/140.

2 Khulaswat al-Wafaa 2/129.

Az-Zubeyr kuuliwa kwa sababu ya kupinga kwake jambo hilo»[1].

8 – Chumba cha Aisha Allah amridhie ambacho ndani yake kuna makaburi kilibakia kimejengwa, kisha jengo lake likajengwa upya tena, na chumba hicho kikaongezewa kuta upande wa nyuma kukilinda, na kikapotoshwa (na kubadilishwa umbo lake); kikawa kwenye umbo la pembetatu upande wake wa mbele, na kwa upande wake wa nyuma kote kumefupishwa, yote haya ni kwa sababu ya kuchunga uzito wa tawheed, ili makaburi hayo yasifanywe kuwa ni misikiti au mtu asivuke mipaka katika (kuyatukuza) makaburi.

9 – Lau ikichukuliwa kwa mfano mmoja aweze kufikia makaburi - japokuwa hilo haliwezekani kwa sababu ya kupatikana kuta, na wala sio jambo lililoamrishwa; kwa sababu Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amekataza kufanywa kaburi lake kama siku ya idi - lau ikachkuliwa kwa mfano iwe hivyo, kisha akaswali, basi itakua ni jambo lililokatazwa, na wala isingesihi kwa mtu huyo anayeswali hapo kusema: «Nimeswali katika msikiti wa Mtume», – kwa sababu ameswali katika nyumba ya Aisha Allah amridhie, nayo si katika msikiti.

10 – Kwamba msikiti haukujengwa juu ya makaburi na wala Mtume swala na salamu za Allah zimshukie hakuzikwa katika msikiti wake, kama ambavyo haiwezekani kuuhamisha msikiti - kwani msikiti wake swala na salamu za Allah zimshukie hauhamishwi -, na wala haifai kuuvunja, na wala haiwezekani kulihamisha kaburi; kwa sababu Mitume wanazikwa sehemu walikokufia.

11 – Atakayeangalia vizuri kiuhakika hali ya chumba; atafahamu kuwa chumba hicho kiko jirani na karibu na msikiti, kimezungukwa na kuta pande zote, na wala haiwezekani kuyafikia makaburi; kwa sababu chumba hicho hakina mlango wala dirisha.

12 – Na pamoja na yote haya, wanachuoni bado wanaendelea

1 Ad-Durar as-Saniyyah 5/140.

kulikataza jambo hilo na wala hawaoni kua hio ni hoja ya kuruhusika kujenga misikiti makaburini, amesema Sheikh Abdul-Aziz ibnu Baaz Allah amrehemu: «Ama kutolea hoja kutoka kwa baadhi ya wasiojua kwa kupatikana kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie na makaburi ya wenzake wawili Allah awaridhie katika msikiti wake, basi hakuna hoja katika hilo; kwa sababu Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alizikwa nyumbani kwake na wala sio msikitini, na wenzake wawili Abu Bakr na Umar Allah awaridhie walizikwa pamoja naye, lakini wakati Al-Waliid ibnu Abdulmalik ibnu Marwaan alipopanua msikiti aliingiza nyumba ndani ya msikiti; kwa sababu ya upanuzi, na alikosea kwa hili. Ilikuwa wajibu wake asikiingize chumba msikitini; ili wasiojua na mfano wao wasitolee hoja kwa hilo, na kwa hakika wenye elimu walimkataza kwa hilo, kwa hivyo, hafai kufuatwa katika jambo hili»[1].

1 Majmuu' Fataawaa Ibnu Baaz 10/306.

# Namna ya kuzuru kaburi la mtume swala na salamu za Allah zimshukie na rafiki zake wawili Allah awaridhie

Mwenye kuzuru atakuja hadi kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie na makaburi mawili ya wenzake Allah awaridhie kwa upande wa mbele wa chumba cha Mtume, kisha ataelekea upande wa kaburi akikipa mgongo Kibula, na atasema: «*Assalaamu a'alaika ayyuhan-nabiyyu warahmatullahi wabarakaatuh* /Amani iwe juu yako ewe Nabii na rehema ya Allah na baraka zake/».

Kisha atapiga hatua upande wake wa kulia akiwa sawasawa na kaburi la Abu Bakr Allah amridhie, na atasema: «*Assalaamu a'alaika yaa Abaa Bakr warahmatullahi wabarakaatuh* / Amani iwe juu yako ewe Abu Bakr na rehema ya Allah na baraka zake/».

Kisha atapiga hatua upande wake wa kulia akiwa sawasawa na kaburi la Umar ibnu al-Khattwaab Allah amridhie, na atasema: «*Assalaamu a'alaika yaa Umar warahmatullahi wabarakaatuh* / Amani iwe juu yako ewe Umar na rehema ya Allah na baraka zake/».

Kisha ataondoka wala hataomba dua, wala hatorefusha kisimamo katika kusalimia. Amesema Sheikhul Islaam Allah amrehemu: «Abdullah ibnu Umar Allah amridhie alikuwa akisema: "*Assalaamu a'alaika yaa rasuulallah, Assalaamu a'alaika yaa Abaa Bakr, Assalaamu a'alaika yaa abatii* / Amani iwe juu yako ewe Mtume wa Allah, Amani iwe juu yako ewe Abu Bakr, Amani iwe juu yako ewe babangu!/". Kisha akasema (Ibnu Umar): Na hivi ndivyo masahaba walivyokua wakimsalimia»[1].

Na inachukizwa kuinua sauti kwa kutoa salamu au lengine lolote sehemu ya kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, amesema Ibnu Kathiir Allah amrehemu: «Wanachuoni walisema: "Inachukizwa kuinua sauti kwenye kaburi lake, kama

1 Fataawaa Sheikhul Islaam 26/146.

ilivyokua wakati wa uhai wake; kwa sababu yeye ni mwenye kuheshimika alipokua hai na akiwa kaburini kwake"»[1].

1 Tafsiir Ibnu Kathiir 7/368.

## Je Allah anaombwa kaburini kwa Mtume swala na salamu zimshukie?

Muislamu hamuombi isipokuwa Mola wake mlezi, na wakati wa kumuomba kwake haelekei kwa kaburi la yoyote - sio la Mtume wala mwengine yeyote -; kwa sababu ni njia ya kupelekea katika shirki; ndio maana hakua yoyote katika masahaba akilifanya hilo. Amesema Sheikhul Islaam Allah amrehemu: «Na wala mtu haombi pale huku ameelekea chumba, kwani hakika haya yote yamekatazwa kwa makubaliano ya maimamu»[1].

Na wala hatakiwi kuomba kaburini hata kama ni mwenye kuelekea Kibula; kwa sababu masahaba na wema waliotangulia wa umma huu hawakua hata mmoja wao akifanya hivyo. Amesema Sheikhul Islaam Allah amrehemu: «Wala asisimame kaburini kwa ajili ya kujiombea nafsi yake, kwani hili ni jambo la uzushi, na masahaba hawakua hata mmoja kati yao, akismama kaburini na kujiombea nafasi yake»[2]. Kwa sababu dua haiwi makaburini.

1 Fataawaa Sheikhul Islaam 26/22.

2 Fataawaa Sheikhul Islaam 26/22.

## Hukumu ya kuomba kwa cheo cha Mtume swala na salamu za Allah zimshukie

Kuomba kwa kupitia cheo cha Mtume swala na salamu za Allah zimshukie ni mfano wa mtu kusema: «Ewe Allah nakuomba uniponye kwa kupitia cheo cha Mtume swala na salamu za Allah zimshukie». Na tamko hili katika dua halifai; kwa sababu sheria haijatuletea tamko hili, na mfano wake vilevile lau atasema: «Kwa cheo cha *Laa ilaaha illallah*», au «Kwa haki ya *Laa ilaaha illallah*», au «Kwa haki ya Mtume swala na salamu za Allah zimshukie»; yote hayo ni matamshi yasiofaa.

Jambo la lazima ni kujifunga na yale yaliokuja katika sheria, na kufata Mitume katika dua zao, na hakika Allah ameeleza katika kitabu chake kuhusu dua za mitume, kama dua ya Nuuh salamu zimshukie:

﴿رَّبِّ ٱغۡفِرۡ لِي وَلِوَٰلِدَيَّ وَلِمَن دَخَلَ بَيۡتِيَ مُؤۡمِنٗا وَلِلۡمُؤۡمِنِينَ وَٱلۡمُؤۡمِنَٰتِۖ﴾

«Ewe Mola wangu Mlezi nisamehe mimi na wazazi wangu na kila aliyeingia nyumbani mwangu kuwa ni mwenye kuamini na Waumini wote wanaume na Waumini wanawake» [Nuuh: 28].

Na kama dua ya Ibrahim salamu zimshukie:

﴿رَبَّنَا وَتَقَبَّلۡ دُعَآءِ﴾

«Ewe mola wetu ikubali dua» [Ibrahim: 40].

Na kama dua ya Ayyub salamu zimshukie:

﴿أَنِّي مَسَّنِيَ ٱلضُّرُّ وَأَنتَ أَرۡحَمُ ٱلرَّٰحِمِينَ﴾

«Hakika yangu mimi yamenikuta ya kunidhuru na wewe ni mwingi wa rehema» [Al-Anbiyaa: 83].

Na wala hakuna Mtume yeyote aliyeomba kwa cheo cha mtu yeyote au kwa haki yake, na pamoja na hivyo Allah aliwakubalia dua zao[1].

---

1 Ighathatu al-Lahfaan 1/216, Ad-Durar as-Saniyyah 2/160, Majmuu' Fataawaa Ibnu Baaz 4/331.

## Je yafaa kutaka kitu kutoka kwa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie baada ya kufa kwake?

Mtume swala na salamu za Allah zimshukie ni mja kiumbe na hakika Allah alimfisha, na kutaka kitu chochote kutoka kwake (kwa mfano kuondsha shida, au kuponya ugonjwa, au uombezi, na mengineo – yote hayo) ni shirki kubwa ambayo mwenye kuifanya atabakishwa milele motoni, wala Allah hataimsamehe kabisa, na matendo yake mazuri yataanguka yote, amesema Allah mtukufu:

﴿وَلَقَدۡ أُوحِيَ إِلَيۡكَ وَإِلَى ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِكَ لَئِنۡ أَشۡرَكۡتَ لَيَحۡبَطَنَّ عَمَلُكَ وَلَتَكُونَنَّ مِنَ ٱلۡخَٰسِرِينَ﴾

«Na kwa yakini yamefunuliwa kwako na kwa walio kuwa kabla yako: “Bila ya shaka ukimshirikisha Allah, basi matendo yako yataanguka, na utakuwa miongoni mwa waliopata hasara”» [Az-Zumar: 65].

Basi haifai kutaka chochote kutoka kwa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, au apelekewe mahitaji; kwa sababu hivyo ni kumshirikisha Allah.

Na Allah Mtukufu yuko hai daima Muweza wa kila kitu, na yeye ndie mwenye kukidhi mahitaji na anajibu maombi na anatatua shida, amesema Allah Mtukufu:

﴿وَإِن يَمۡسَسۡكَ ٱللَّهُ بِضُرّٖ فَلَا كَاشِفَ لَهُۥٓ إِلَّا هُوَۖ وَإِن يُرِدۡكَ بِخَيۡرٖ فَلَا رَآدَّ لِفَضۡلِهِۦۚ يُصِيبُ بِهِۦ مَن يَشَآءُ مِنۡ عِبَادِهِۦۚ وَهُوَ ٱلۡغَفُورُ ٱلرَّحِيمُ﴾

«Na Allah akikuletea madhara, basi hakuna wa kukuondolea (madhara hayo) ila Yeye. Na akikutakia kheri, basi hapana awezaye kurudisha fadhila yake. Huifikisha kwa amtakaye katika waja wake, na Yeye ni Mwingi wa kusamehe, Mwingi wa kurehemu» [Yunus: 107].

Basi mahitaji yote yanatakwa kutoka kwa Allah peke yake, Allah Mtukufu alisema:

﴿وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ ۖ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ ۖ﴾

«Na waja wangu watakapo kuuliza kunihusu mimi, waambie kuwa Mimi nipo karibu. Naitikia maombi ya muombaji anaponiomba.» [Al-Baqarah: 186].

## Hukumu ya kusoma al-Faatiha kwenye kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie

Haifai kusoma Suratul-Faatiha wala sura nyengine yoyote kwenye kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie wala kwenye kaburi la mwengine yoyote; kwani kwa hakika hakua yoyote katika masahaba akizidisha zaidi ya kumsalimia au akifanya hivyo makaburini, amesema Ibnu Qudaamah Allah amrehemu: «Na imepokewa kutoka kwa Imam Ahmad yakwamba alisema: "Kusoma (Qur-ani) kaburini ni jambo la uzushi"»[1]. kwa sababu makaburi sio sehemu ya kusoma Qur-ani, au kumtaja Allah, au kuswali, wala makaburi hayafanywi kama miskiti katika kufanya mambo hayo.

1 Al-Mughniy 2/355.

## Hukumu ya kurefusha kusimama kwenye kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie

Kusimama kwenye kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie au wenzake wawili au wengineo hakurefushwi; kwa sababu hilo linapelekea kuvuka mipaka, amesema Sheikhul Islaam Allah amrehemu: «Kusimama kwa ajili ya kumuombea Mtume swala na salamu za Allah zimshukie pamoja na kukithirisha kumfikishia swala na salamu; jambo hili alilichukia Maalik na alisema: “Hilo ni jambo la uzushi, halikufanywa na wema waliotangulia”»[1].

1 Fataawaa Sheikhul Islaam 27/384.

## Hukumu ya kurudiarudia kwenye kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie kwa ajili ya kumsalimia

Hakua yeyote katika masahaba alikithirisha kurudiarudia kwenye kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie kwa ajili ya kumsalimia yeye kwenye kaburi lake, na kwa yakini alisema Mtume swala na salamu za Allah zimshukie: «**Msifanye kaburi langu ni kama idi (bimaana msifanye sehemu inayokuja kurudiwarudiwa kila mara)**». Imepokewa na Ahmad, na Allah amewafanyia waislamu wepesi wamswalie na wamsalimie kila mahali bila kua na haja ya kufika kwenye kaburi lake, amesema Mtume swala na salamu za Allah zimshukie: «**Na mniswalie, kwani kwa hakika salamu zenu zinanifikia popote mlipo**». Imepokewa na al-Maqdisi katika Al-Mukhtaarah.

## Hukumu ya kuelekea kaburi kwa mbali

Baadhi ya watu wakiwa katika ukumbi wa msikiti wa Mtume au ndani ya msikiti analielekea kaburi na anainamisha chini kichwa chake, na baadhi yao anaweka mkono wake juu ya kifua chake kama vile mwenye kuswali akiwa kwenye swala yake na anamsalimia Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, na hiki kitendo hakifai; kwa sababu kunyenyekea kunafanyiwa Allah, na wala haikupokelewa namna hii ya salamu kutoka kwa masahaba wala wema waliotangulia wa umma huu, na Allah ameamrisha kumswalia Mtume wake akasema:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ صَلُّواْ عَلَيۡهِ وَسَلِّمُواْ تَسۡلِيمًا﴾

«Enyi mlio amini Msalieni na mumsalimu kwa salamu». [Al-Ahzaab: 56].

Na wala haikuja amri wakati wa kumsalimia mtu alielekee kaburi, au aweke mkono wake kwenye kifua, na mfano wa hivyo.

## Hadithi ambazo hazikusihi kuhusu ziara ya kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie

Yale yaliyopokelewa katika hadithi zinazozungumzia ulazima wa kuzuru kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie baada ya hija, au ubora wa kumzuru baada ya kufa kwake, na mfano wa hayo; hazijasihi kutoka kwa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, na katika hizo ni:

**1) «Atakayehiji, na asinizuru; atakua amenichukia».**

**2) «Atakaye zuru kaburi langu; umemuwajibikia uombezi wangu».**

**3) «Atakaye kua na uwezo, na wala asije kwangu; basi atakua amenichukia».**

**4) «Atakaye nizuru baada ya kufa kwangu, basi atakua ni kana kwamba amenizuru wakati wa uhai wangu, na atakaye nizuru baada ya kufa kwangu, atapata maombezi yangu».**

Amesema Sheikhul Islaam Allah amrehemu: «Hakika ya hadithi za kuzuru kaburi lake zote ni dhaifu hazitegemewi katika dini»[1].

❖❖❖

1 Fataawaa Sheikhul Islaam 1/234.

# Masjid Qubaa

# Masjid Qubaa

Qubaa: asli yake ni jina la kisima; na kijiji hicho kikajulikana kwa jina hilo, na umbali wake ni kilomita tatu takriban kutoka upande wa mbele wa msikiti wa Mtume, na sasa hivi kimeingia kijiji hiki katika mji wa Madina.

Na alipogura Mtume swala na salamu za Allah zimshukie kwenda Madina na akaukurubia na akafika Qubaa, aliweka msingi hapo wa msikiti uliojengwa kwa ajili ya uchaji Allah kuanzia siku ya kwanza, amesema Allah Mtukufu:

﴿لَّمَسۡجِدٌ أُسِّسَ عَلَى ٱلتَّقۡوَىٰ مِنۡ أَوَّلِ يَوۡمٍ﴾

«Msikiti uliojengwa juu ya msingi wa uchaji Allah tangu siku ya mwanzo». [At-Tawbah: 108].

Sheikhul Islaam Allah amrehemu amesema: «Aya hii ilishuka kwa sababu ya msikiti wa Qubaa, lakini hukumu yake inaufikia (msikiti huu) na inaingia pia (msikiti) ulio na haki zaidi kuuliko, nao ni msikiti wa Madina»[1].

Na Allah aliwasifu watu wake kwa kusema:

﴿فِيهِ رِجَالٞ يُحِبُّونَ أَن يَتَطَهَّرُواْ﴾

«Humo mna watu wanaopenda kujitakasa» [At-Tawbah: 108].

Kisha Mtume swala na salamu za Allah zimshukie akaendelea kuikamilisha safari yake ya kuguria Madina, Ijumaa ikampata katika familia ya Banuu Saalim akaswali hapo, kisha akaendelea na safari mpaka akafika Madina na kujenga msikiti wake hapo.

1 Minhaaj al-Sunnah al-Nabawiyyah 7/47.

## Ubora wa kuswali katika msikiti wa Qubaa

Ni jambo la kupendekezwa kwa watu wa Madina na kwa yule mwenye kufika Madina kufanyia ziara msikiti wa Qubaa na kuswali humo, amesema Ibnu Umar Allah amridhie: «Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akija katika msikiti wa Qubaa kila wiki, kwa kutembea na kwa kupanda kipando». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea. Basi kukiwa na wepesi kwa mtu kuuendea siku ya jumamosi basi hivyo ni bora zaidi, lakini ikiwa hakuna wepesi basi atauendea siku yoyote katika masiku ya wiki, na anaweza kuuzuru na kuswali humo kila wakati, usiku ama mchana, isipokuwa katika nyakati zilizokatazwa.

Na inapendekezwa kutawadha nyumbani kwake, au nyumba ambayo yeye yuko, amesema Mtume swala na salamu za Allah zimshukie: «**Yoyote atakayejitwahirisha nyumbani kwake, kisha akaja msikiti wa Qubaa, kisha akaswali humo swala yoyote; atapata malipo kama malipo ya kufanya Umra**». Imepokewa na Ibnu Maajah.

❖❖❖

# Kuzuru Makaburi

## Hikma ya Kuzuru Makaburi

1 – Kukumbuka umauti, amesema Mtume swala na salamu za Allah zimshukie: «**Fanyeni ziara makaburini; kwani hakika yanawakumbusha umauti**». Imepokewa na Muslim.

2 – Kuwatendea wema maiti waislamu kwa kuwaombea dua ya msamaha na rehema; kwa sababu maiti ananufaika kwa dua, na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa anapozuru Al-Baqi'i anawaombea mazuri, na maiti wanaombewa mazuri na wala hawaombwi pamoja na Allah.

# Aina za Kuzuru Makaburi

Kuzuru makaburi kunagawanyika mara mbili: kwa kisheria, na kusokua kisheria.

## ❋ Kigawanyo cha kwanza: Kuzuru kwa kisheria:

Nako ni kule kunakotekelezwa kwa njia ilioafikiana na yale yaliofundishwa katika sheria. Na kuzuru kwa aina hii ndiko kunakomnufaisha alio hai mwenye kuzuru, akapata kukumbuka mauti, Akhera na maandalizi yake. Pia ananufaika nako maiti mwenye kuzuriwa kwa kuombewa msamaha na rehema.

**Na namna yake:**

Inapendekezwa anapoingia makaburini aseme dua iliopokewa wakati wa kuingia makaburini, amesema Burayda Allah amridhie: «Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akiwafundisha (masahaba) watokapo kuenda makaburini waseme: «***Assalaamu 'alaikum Ahlad-diyyari minal- Muuminina wal-Muslimina, wa innaa in shaa Allahu lalaahiquun. As-alu-llaha lanaa wa-lakumul- 'aafiyah*** **/Amani iwe juu yenu watu wa majumba haya katika waumini na waislamu, na sisi Allah akitaka tutaungana na nyinyi, namuomba Allah kwetu sisi na nyinyi afya/**». Imepokewa na Muslim. Na atawaombea msamaha, rehema na mfano wa hayo, na huu ndio muongozo wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie katika kuzuru makaburi.

## ❋ Kigawanyo cha pili: Kuzuru kusokua kisheria:

Nako ni kule ambako kunakotekelezwa kwa njia isiokua ya kisheria, na kunagawanyika aina mbili:

1. **Aina ya kwanza: Kuzuru kwa njia ya kishirikina.**

Nayo ni ile ambayo mwenye kuzuru anamuelekezea maiti ibada -kwa mfano kumuomba maiti amkidhie mahitaji, au kutatua shida, na mfano wa hayo-, amesema Allah Mtukufu:

﴿يُولِجُ ٱلَّيۡلَ فِي ٱلنَّهَارِ وَيُولِجُ ٱلنَّهَارَ فِي ٱلَّيۡلِ وَسَخَّرَ ٱلشَّمۡسَ وَٱلۡقَمَرَۖ
كُلّٞ يَجۡرِي لِأَجَلٖ مُّسَمّٗىۚ ذَٰلِكُمُ ٱللَّهُ رَبُّكُمۡ لَهُ ٱلۡمُلۡكُۚ وَٱلَّذِينَ
تَدۡعُونَ مِن دُونِهِۦ مَا يَمۡلِكُونَ مِن قِطۡمِيرٍ * إِن تَدۡعُوهُمۡ لَا يَسۡمَعُواْ
دُعَآءَكُمۡ وَلَوۡ سَمِعُواْ مَا ٱسۡتَجَابُواْ لَكُمۡۖ وَيَوۡمَ ٱلۡقِيَٰمَةِ يَكۡفُرُونَ بِشِرۡكِكُمۡۚ
وَلَا يُنَبِّئُكَ مِثۡلُ خَبِيرٖ﴾

«Anauingiza usiku katika mchana, na anauingiza mchana katika usiku. Na amelifanya jua na mwezi kutumikia. Kila kimojapo kinakwenda kwa muda maalumu. Huyo ndiye Allah Mola wenu Mlezi. Ufalme ni wake. Na wale mnaowaomba badala yake hawamiliki hata ugozi wa kokwa ya tende. Mkiwaomba hawasikii maombi yenu; na hata wakisikia hawatawajibu. Na Siku ya Kiyama watakataa ushirikina wenu. Na hapana atakayekupa khabari vilivyo kama Yeye Mwenye khabari». [Faatwir: 13-14].

Na kuzuru kwa namna hii kunamuudhi maiti - akiwa ni mwema - wala hafaidiki na ziara hii; kwa sababu hakumuombea msamaha wala rehema na yeye ni muhitaji wa maombi hayo, na anadhurika kwa ziara hii alioko hai; kwa sababu ameingia katika shirki kubwa.

**2. Aina ya pili: Kuzuru kwa njia ya kizushi.**

Kama kumuomba Allah makaburini, au kusoma Qur-ani, au kuleta uradi, au kumuomba Allah kwa kupitia cheo chao, na mfano wa hayo; kwa sababu hayakupokelewa hayo katika Qur-ani wala hadithi wala hawakuyafanya hayo wema waliotangulia.

Amesema Sheikh Abdul-Aziz ibnu Baaz Allah amrehemu: «Ama kuwazuru kwa malengo ya kuomba dua makaburini kwao, au kukaa hapo, au kuwaomba kukidhi mahitaji, au kuponya wagonjwa, au kumuomba Allah kwa kupitia hao, au kwa kupitia cheo chao na mfano wa hayo; huku ni kuzuru kwa njia ya kizushi

kuliko katazwa, Allah hajayaweka haya katika sheria wala Mtume wake wala hawakuyafanya hayo wema waliotangulia Allah aweradhi nao; bali ni katika kusema maneno mabaya ambako alikokukataza Mtume swala na salamu za Allah zimshukie aliposema: «**Fanyeni ziara ya makaburi, na wala musiseme maneno mabaya**».

Na haya mambo yaliyotajwa yanakusanyika yote kuwa ni uzushi, lakin yametofautiana daraja:

Baadhi yake: ni uzushi na sio shirk - kama kumuomba Allah makaburini, na kumuomba kwa haki ya maiti na cheo chake, na mfano wa hayo -.

Na baadhi yake: ni katika shirki kubwa - kama kuwaomba maiti, na kutaka msaada kwao, na mfano wake»[1].

1 At-Tahqiiq wal-Iidhaah, uk 106.

## Hukumu ya wanawake kuzuru makaburi

Kuzuru makaburi ni jambo lililopendekezwa kwa wanaume, ama wanawake kuzuru makaburi; basi kwa hakika Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amekataza wanawake kuzuru makaburi, Amepokewa Abuu Hureyra Allah amridhie: «Kwamba Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amewalani wanawake wenye kuzuru sana makaburi». Imepokewa na At-Tirmidhi. Na hii ni kwa sababu wanawake wana udhaifu, na uchache wa kusubiri kujizuia na kulia, kupiga ukelele na kubabaika wakati wa kuona makaburi, na kwa hekima nyinginezo azijuazo Allah.

## Kurusha mbegu na kutia marashi juu ya makaburi

Haifai kunyunyizia nafaka kwa ajili ya ndege juu ya makaburi, na hili ni katika kuyatukuza makaburi kwa njia isiyokua ya kisheria, Yeyote anayetaka kuwalisha ndege basi na awalishe mbali na makaburi.

Vilevile haifai kuweka marashi juu ya makaburi; kwa sababu hili ni katika kuvuka mipaka kwa makaburi, na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Nawatahadharisha na kuvuka mipaka katika dini**». Imepokewa na An-Nasaai. Na maiti hafaidiki na marashi haya bali anafaidika na dua za walio hai wakimuombea msamaha na rehema.

❖❖❖

# Al-Baqi'i

# Al-Baqi’i

**Al-Baqi’i** – ni sehemu ilokuwa nje ya Madina, inapatikana mashariki ya msikiti wa Mtume, na kulikua na mti wa Gharqad, na saa hii mti huu haupo katika Al-Baqi’i.

Na pia vilevile inaitwa «Baqi’i al-Gharqad».

## ❋ Kuzuru makaburi ya Al-Baqi’i

Kuzuru makaburi ya Al-Baqi’i kunapendekezwa kama kunavyopendekezwa kuzuru makaburi mengine ikiwa itakua ni kuzuru kwa njia ya kisheria, na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akizuru Al-Baqi’i kwa ajili ya kupata mawaidha na mazingatio na kuwaombea maiti, amesema Aisha Allah amridhie: «Mtume swala na salamu za Allah zimshukie - kila inapofika usiku wa zamu yangu - alikuwa akitoka mwisho wa usiku kuenda Al-Baqi’i». Imepokewa na Muslim.

## ❋ Je kuna kaburi la yeyote katika masahaba linalojulikana ndani ya Al-Baqi’i?

Katika Al-Baqi’i walizikwa baadhi ya Masahaba na Taabiina (waliokuja baada ya masahaba), lakini masahaba wengi hawakuzikwa Al-Baqi’i; kwa sababu ya kuenea kwao katika ardhi ili kueneza dini na kufikisha ulinganizi. Na kwa sababu ya zama za Masahaba na Taabiina na waliowafwata Taabiina kuwa mbali na sisi ndio maana halijulikani kaburi la yeyote miongoni mwao kwa njia mahususi, na atakayehusisha kaburi la yeyote miongoni mwao basi atakua hana uthibitisho katika madai yake hayo.

## Je kuzikwa Al-Baqi'i kuna ubora wowote?

Kuthibitisha ubora wa zama fulani au sehemu fulani ni jambo la kuachiwa sheria linalohitaji dalili sahihi, kwa hivyo, haifai kuhusisha zama ama sehemu fulani kuwa na ubora isipokuwa kwa dalili ya kisheria.

Na kuzikwa Al-Baqi'i hakuna ubora mahususi, wala hakujathibiti dalili yoyote kuhusu hilo, na jumla ya yanayotajwa katika hili:

- Ima haikusihi, kwa kuwa ni dhaifu au ni maneno aliyosingiziwa Mtume.

- Na ima hakuna kinachoonyesha ubora wa kuzikwa Al-Baqi'i.

Na maelezo ya haya ni kama ifuatavyo:

**1. Yaliopokewa lakini hayana kitu kinachojulisha ubora wa kuzikwa Al-Baqi'i:**

1) Yale yaliyokuja katika dalili zilizopokelewa katika jumla ya fadhila ya Madina hazihusishi Al-Baqi'i kwa ubora zaidi wa kuzikwa hapo kuliko kwengine katika sehemu za Madina. Na yeyote atakayehusisha Al-Baqi'i kwa ubora wa kuzikwa ndani yake, basi ni juu yake kutoa dalili inayotaja hilo. Kama sivyo, basi angedai mwenye kutaka chochote anachokitaka katika fadhila maalumu za sehemu maalumu katika mji wa Madina.

2) Hadithi: «**Yeyote anayeweza kufariki Madina; basi afe humo, kwani hakika mimi nitamuombea au nitamtolea ushahidi**». Imepokewa na An-Nasaai. Katika hadithi hii hakuna fadhila ya kuzikwa Al-Baqi'i, lakini ndani yake kunapatikana fadhila ya kufa Madina, kama ambavyo ndani yake kunapatikana mahimizo ya kuishi Madina, na kusubiria maisha yake.[1].

3) Ziara ya Nabii swala na salamu za Allah zimshukie kwa watu wa Al-Baqi'i, kitendo chake hiki ni kama mfano wake

1 Tazama: Haashiyat as-Sindi alaa Ibnu Maajah 2/267, Mirqaat al-Mafaatiih 5/1884, Faydh al-Qadiir 6/53, 'Uquud az-Zabarjad 2/6.

kuwazuru mashahidi wa Uhud na kaburi la mama yake na ni mfano wa ziara ya kisheria wa makaburi mengine. Wala haithibutu kwa hilo ubora wa sehemu iliofanyiwa ziara wala ubora wa kuzikwa hapo, ingekua hivyo basi pia kungethibiti ubora wa kuzikwa eneo la makaburi ya Uhud.

4) Hadithi: «***Assalaamu 'alaikum daara qawmin Muuminiin, wa ataakum maa tuu'aduun, ghadan muajjaluun, wa innaa in shaa Allahu Laahiquun, Allahumma ighfir li-Ahli Baqi'i al-Gharqad*. /Amani iwe juu yenu, makaburi ya watu walioamini, na yamewajieni (mauti) mlioahidiwa, mna mda mpaka kufufuliwa kesho (Kiyama), na sisi Allah akitaka tutaungana nanyi. Ewe Allah nakuomba uwasamehe watu wa Baqi'i al-Gharqad/**». Imepokewa na Muslim. Dua yake Mtume swala na salamu za Allah zimshukie kwa watu wa Al-Baqi'i ni mahususi  kwa watu waliozikwa wakati wa ziara yake swala na salamu za Allah zimshukie kwa dalili ya neno lake: «**Yamewajieni (mauti) mlioahidiwa**». Katika tamko hili kuna dalili ya kuonyesha wahusika ni wale waliokufa wakati wa hii dua yake; kwa sababu waliozikwa baada ya hapo bado mauti hayajawafikia.

Kama ambavyo kauli yake: «**na sisi Allah akitaka tutaungana nanyi**», inaonyesha kua dua hii ni mahususi kwa wale waliozikwa wakati alipoomba; kwa sababu aliyezikwa baada ya hapo basi Mtume swala na salamu za Allah zimshukie hatakua ni mwenye kuungana naye; bali yeye ndio atakua ni mwenye kuungana na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie atakapokufa.

5) Hadithi ya Aisha Allah amridhie kwamba Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Hakika Jibrili amenijia akaniita na kuniambia: "Hakika Mola wako anakuamrisha uende kwa watu wa Al-Baqi'i ukawaombee msamaha"**». (Aisha) akasema: «Nikasema: niwaambie vipi ewe Mtume wa Allah?" akasema: ***"Assalaamu 'alaikum Ahlad-diyyari minal- Muuminina wal-Muslimiina, wayarhamu-llahu al-mustaqdimiina minnaa wal-mustaakhiriin, wa innaa in shaa Allahu bikum lalaahiquun."***

**/Amani iwashukie mlio makaburini miongoni mwa waumini na waislamu, Allah awarehemu waliotangulia kati yetu na watakaochelewa, na sisi Allah akitaka tutaungana nanyi/**». Imepokewa na Muslim. Hadithi hii ina sehemu mbili:

a) Sehemu ya kwanza: «**Hakika Mola wako anakuamrisha uende kwa watu wa Al-Baqi'i ukawaombee msamaha**». Makusudio ni: waliozikwa Al-Baqi'i wakati yeye alipoomba, kwa dalili ya neno lake: «**uwaendee watu wa Al-Baqi'i**». Yule ambaye hakua amezikwa Al-Baqi'i wakati wa kuzuru kwake, basi huyo si katika watu wa Al-Baqi'i, wala haingii katika kuombewa msamaha huu, na atakayedai kuwa kila anayezikwa Al-Baqi'i mpaka siku ya Kiyama anaingia (katika fadhila hii) itamlazimu kuleta dalili.

b) Sehemu ya pili: «**Amani iwashukie mlio makaburini miongoni mwa waumini na waislamu, Allah awarehemu waliotangulia kati yetu na watakaochelewa, na sisi Allah akitaka tutaungana nanyi**». Na dua hii hakuiomba Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, bali alimfundisha Aisha Allah amridhie (pale alipomuuliza Mtume) akasema: «Niwaambie vipi ewe Mtume wa Allah?" Akasema: **"Sema: Amani iwashukie mlio makaburini..."**». Na hii ni dua inayoombwa wakati wa kuzuru makaburi ya waislamu kwa ujumla, wala sio dua maalum kwa makaburi ya Al-Baqi'i pekee, kwa dalili ya hadithi alioipokea Abdur-Razzak: «Kwamba (Aisha Allah amridhie) alisema: "Nilimuuliza Mtume swala na salamu za Allah zimshukie; Tuseme vipi wakati wa kuyasalimia makaburi? Akasema: **"Amani iwashukie mlio makaburini miongoni mwa waumini..."**»[1]. Kama ambavyo dua hii imewakusanya waumini wote wale walio hai na waliokufa, Amesema kwenye kitabu cha al-Mirqaat: «(**wa yarhamullahul mustaqdimiin**) – yaani wale ambao wametutangulia

1 Al-Muswannaf, nambari 6722.

katika kufa. (**minnaa**) – yaani, sisi waumini. (**wal-mustaakhiriina**) – yaani, wale watakaokufa baadae»[1].

Kwa hivyo, mtu atakapoomba dua hii wakat wa kuyazuru makaburi, basi dua yake itakua imekusanya walio hai na waliokufa miongoni mwa waumini. Ama yule ambaye hajazaliwa, basi haingii katika dua hii, wala hakumaanishwa na tamko la dua hii.

Dua hii, pamoja na ile ilio kabla yake katika kipengele cha nne; sio dua maalumu kwa watu wa Al-Baqi'i; bali ni sheria kuzisema wakati wa kuzuru makaburi yoyote ya Waislamu. Amesema An-Nawawiy Allah amrehemu: «Katika hadithi kunapatikana mapendekezo ya kusema maneno haya kwa mwenye kuzuru makaburi»[2]. Na kwa ajili hii, utapata maimamu - Allah awarehemu - waliweka milango katika vitabu vyao kuhusu mambo yanayofidisha hilo, utapata Abdur-Razzak aliweka mlango katika kitabu chake al-Muswannaf,[3] akasema: «Mlango wa kuzuru makaburi»; vilevile Al-Bayhaqiy aliweka mlango katika kitabu chake As-Sunanul-Kubraa[4], akataja: «Mlango wa anachokisema mtu aingiapo eneo la makaburi»; kadhalika An-Nawawiy aliweka anuwani katika kitabu Swahih Muslim[5] kwa kusema: «Mlango wa kinachosemwa wakati wa kuingia makaburini na kuwaombea watu wake».

Na hivi ndivyo walivyokuwa wema waliotangulia wakiwaombea maiti. Hilaal ibnu Khabbab Allah

---

1 Mirqatul-Mafaatiih 7/44.

2 Sharhu Swahiih Muslim 4/1259.

3 3/574, nambari 6718.

4 4/131.

5 2/669.

amrehemu amesema: «Nilisuhubiana na Mujaahid mpaka Makkah, alikuwa apitapo kwenye makaburi anasema: *“Assalaamu 'alaikum yaa Ahlad-diyyaril Muuminina wal-Muslimiina, yarhamu-llahu al-mustaqdimiina minkum, wa innaa in shaa Allahu bikum laahiquun”* / Amani iwashukie mlio makaburini ya waumini na waislamu, Allah awarehemu waliotangulia kati yenu, na sisi Allah akitaka tutakutana nanyi/»[1].

6) Yaliopokelewa kuhusu kuzikwa baadhi ya Masahaba katika Al-Baqi’i; hili halijulishi kuwepo na ubora wa kuzikwa hapo, kwani hapo alizikwa vilevile aliyekua sugu katika unafiki -kama Abdullah ibnu Ubayyi ibnu Saluul-, na ardhi haitakasi mtu, amesema Salmaan Al-Faarisiy Allah amridhie: «Hakika ardhi haitakasi mtu, bali kinachomtakasa mtu ni matendo yake»[2].

Na Masahaba wengi hawakuzikwa Al-Baqi’i, bali Makhalifa waongofu hakuna hata mmoja wao aliyezikwa hapo, Abu Bakr na Umar Allah awaridhie walizikwa kando ya Mtume swala na salamu za Allah zimshukie. Na Uthmaan Allah amridhie naye alizikwa Madina nje ya Al-Baqi’i. Amesema Ibnu Kathiir Allah amrehemu: «Ama sehemu ya kaburi lake hakuna khilafu kwamba: ni katika bustani la Kawkab, upande wa mashariki ya Al-Baqi’i»[3]. Ali ibnu Abii Twalib Allah amridhie naye alizikwa Al-Kuufah[4].

### 2. ambazo hazijasihi miongoni mwa hadithi dhaifu na zilizotungwa:

1) Kutoka kwa Abu Raafi Allah amridhie amesema: «Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa anawatafutia masahaba zake eneo la makuburi wazikwe hapo, basi akawa

1 Hilyatul Awliyaa wa Twabaqaat al-Asfiyaa 3/286.

2 Al-Muwatta 2/769.

3 Al-Bidaayah wan-Nihayah 10/324.

4 Minhaaj as-Sunnah 7/43.

anatafuta kandokando ya Madina na pembezoni mwake, kisha akasema: **Nimeamrishwa sehemu hii -akimaanisha Al-Baqi'i-**». Imepokewa na Al-Haakim. Amesema Adh-Dhahabiy: «Sanad yake ni "Waahin" (yaani ni dhaifu sana haiwezi kuwa hoja)»[1]. Na akasema Ibnu al-Mulaqqin: «Ndani yake kuna Al-Waaqidiy, na hali yake inajulikana, na Abu Bakr ibnu Abdullah Al-Madiini naye ni "Taalif" (yaani mdhaifu sana hazingatiwi)»[2].

2) «**Watafufuliwa watu elfu sabini kutoka Al-Baqi'i wakiwa na sura ya mwezi usiku wa mwezi kamili**». Imepokewa na At-Twabaraaniy. Amesema Al-Haythamiy: «katika wapokezi wa hadithi kuna ambaye simjui»[3]. na akasema Al-Albaaniy: «Ni hadithi Munkar)»[4].

3) «**Mimi ni mtu wa kwanza kufufuliwa siku ya Kiyama, kisha Abu Bakr, kisha Umar, kisha nitakuja kwa watu wa Al-Baqi'i wafufuliwe pamoja nami, kisha nitawasubiri watu wa Makkah...**». Imepokewa na At-Tirmidhi. Amesema Ibnul-Jawziy: «Hii hadithi haisihi; njia zake zote zapitia kwa Abdullah ibnu Naafi', amesema Yahya ibnu Mai'in kumhusu: " Mtu huyu si chochote (bimaana: ana udhaifu sana)". Na akasema Ali: "Anapokea hadithi Munkar". Na amesema An-Nasaai: "Ni mwenye kuachwa". Vilevile sanad ya hadithi hii inapitia kwa A'aswim ibnu Umar, ambaye amedhoofishwa na Ahmad (ibnu Hanbal) na Yahya (ibnu Ma'iin)". Na amesema Ibnu Hibban: "Haifai kutolea hoja kupitia mtu huyu"»[5].

4) «**Al-Hajuun** (sehemu ilioko Makkah yenye makaburi) **na Al-Baqi'i zitachukuliwa sehemu za pembezoni mwake na zitaenezwa peponi**». Amesema Al-'Ajluuniy: «Hadithi hii

1 Talkhiis al-Mustadrak 3/209.

2 Al-Badr al-Muniir 5/326.

3 Majma' az-Zawaaid wa Manba' al-Fawaa'id 4/12.

4.As-Silsilah al-Dha'ifah, nambari 5491.

5 Al-'ilal al-Mutanaahiyah fi al-Ahaadiith al-Waahiyah 2/432.

haijulikani asili yake»[1]. Hadithi hii pia imetajwa na Ash-Shawkaaniy katika kitabu chake Al-Mawdhuu'aat (yaani hadithi alizosingiziwa Mtume)[2].

5) «**Hakika yangu nimetumilizwa kwa watu wa Al-Baqi'i niwaswalie na kuwaombea**». Imepokewa na An-Nasaai. Amesema Al-Albaaniy: «Sanad (msururu wa wapokezi) ya hadithi hii ina udhaifu». Maana ya hadithi: Kuwaombea na kuwaswalia masahaba wale ambao hawakuswaliwa na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie. Amesema Ibnu Abdil Barr: «kauli yake aliposema: "**Hakika yangu nimetumilizwa kwa watu wa Al-Baqi'i niwaswalie na kuwaombea**", maneno haya kwa mujibu wangu yamekuja kumaanisha ujumla (yaani kuwaswalia maiti wote kwa jumla), lakini maana yake ni kwa kitu fulani mahususi, kana kwamba amesema: Nimetumilizwa kwa watu wa Al-Baqi'i ili niwaswalie wale ambao sijawaswalia katika masahaba zangu»[3].

**3. Katika mambo yanayozidisha msingi huu ubainifu ni haya yafuatayo:**

1) Katika mji wa Madina kuna maeneo zaidi ya kumi ya makaburi. Na lau waliotangulia wangejua ubora wa kuzikwa Al-Baqi'i basi wangepupia zaidi kuzikwa pale, ikatufahamisha kuwa kuzikwa Al-Baqi'i na maeneo mengine ya makaburi ya Madina yote ni sawa, wala hakuna fadhila maalumu kwa moja kuliko nyingine.

2) Mtume swala na salamu za Allah zimshukie aliwazika mashahidi wa Uhud karibu na mlima wa Uhud na miongoni mwao kuna ami yake Hamza Allah amridhie, na lau kama kuzikwa Al-Baqi'i kuna ubora angewahamisha huko.

---

1 Kashful-Khafaa wa Muziil al-Ilbaas 1/104.

2 Al-Fawaaid al-Majmuu'ah fi al-Ahaadiith al-Mawdhuu'ah 1/113.

3 Al-istidhkaar 3/121.

3) Ikiwa kuzikwa Al-Baqi’i kumepata ubora kutokana na ubora wa Madina, basi ardhi yote ya Madina na maeneo ya makaburi yake yanashirikiana katika hili na hakuna umahususi wa kuzikwa Al-Baqi’i kuliko sehemu nyingine ziliobakia ndani ya Madina.

4) Wema waliotangulia katika wale waliokuja baada ya masahaba na baada yao walifahamu kwamba hakuna umahsusi katika kuzikwa Al-Baqi’i kuliko maeneo mengine ya makaburi. Imam Maalik amepokea (na kupitia njia ya mapokezi yake kuna Ash-Shaafi'iy), kutoka kwa Urwa ibnu Az-Zubeir - naye ni katika Taabiina wakubwa, na mmoja kati ya wanachuoni wa Madina saba - kwamba amesema: «Sipendelei nizikwe Al-Baqi’i; ikiwa nitazikwa sehemu nyengine, basi hilo linapendekeza zaidi kwangu mimi kuliko kuzikwa hapo, kwani (ndani ya Al-Baqi’i) hakika nitapata mmoja kati ya watu wawili: ima awe mtu dhalimu basi sitapenda niwe jirani yake, ama awe ni mtu mwema, basi sitapenda kufukuliwe kwenye mifupa yake»[1].

Ikabainika katika maelezo yaliotangulia: kwamba kuzikwa Al-Baqi’i hakuna ubora maalumu kwa huko kuzikwa kwenyewe, isipokuwa tu kunapatikana watu wengi wanaoingia hapo kwa ajili ya kuwasalimia maiti na kuwaombea.

1 Al-Muwatta 2/326, Al-Umm 1/316.

## Je kuzikwa Madina kuna ubora wowote?

Ubora kwa hakika unapatikana kwa kufa Madina sio kuzikwa humo, amesema Mtume swala na salamu za Allah zimshukie: «**Yeyote anayeweza kufa Madina; basi afarikie humo, kwani hakika yangu mimi nitamuombea au nitamtolea ushahidi**». Imepokewa na An-Nasaai.

Basi yeyote atakayekufa nje ya Madina na akazikwa humo hataupata ubora huo.

❖❖❖

# Eneo la Makaburi ya Mashahidi wa Uhud

# Eneo la Makaburi ya Mashahidi wa Uhud

Makusudio ya “Eneo la makaburi ya mashahidi wa Uhud" ni makaburi ambayo masahaba waliokufa mashahidi Allah awaridhie walizikwa baada ya vita vya Uhud. Makaburi haya yapo kando ya mlima wa Uhud, na mlima wa Uhud uko kaskazini mwa Msikiti wa Mtume na una umbali wa takriban kilomita tatu kutoka huko.

Katika vita hivyo, masahaba Allah awaridhie walijitahidi pakubwa, na wakapata shahada sabini kati yao - miongoni mwao ni Hamza, mjomba wa Nabii swala na salamu za Allah zimshukie, Mus'ab ibnu Umayr, Abdullah ibnu Haraam, baba yake Jaabir ibnu Abdullah Allah awaridhie. Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akiwazuru. Na katika mwaka ambao Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alifariki, aliwaendea mashahidi wa Uhud na kuwaombea dua, kama kwamba anawaaga, ili kuwalipa kwa mchango wao kwa dini hii.

Katika eneo hili la makaburi, haijulikani kaburi la sahaba yeyote kati yao, kwa sababu ya kupitiwa na muda mrefu makaburi yao.

❖❖❖

# Masahaba, Allah awaridhie

## Fadhila za Masahaba Allah awaridhie

Masahaba Allah awaridhie walipata ubora na fadhila nyingi ambazo ziliwawezesha kuwapita wale walio kuwa kabla yao na wale waliokuja baada yao. Allah aliwapa habari njema za Pepo walipokuwa bado wako hai, kama alivyosema:

﴿وَكُلًّا وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلْحُسْنَىٰ﴾

«Na wote, Allah amewaahidi mema». [Al-Hadiid: 10]. Hapa maana ya «mema» ni: Pepo.

Na pia Allah alitangaza kuwa amewaridhia, kama alivyosema:

﴿وَٱلسَّٰبِقُونَ ٱلْأَوَّلُونَ مِنَ ٱلْمُهَٰجِرِينَ وَٱلْأَنصَارِ وَٱلَّذِينَ ٱتَّبَعُوهُم بِإِحْسَٰنٍ رَّضِيَ ٱللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا۟ عَنْهُ وَأَعَدَّ لَهُمْ جَنَّٰتٍ تَجْرِي تَحْتَهَا ٱلْأَنْهَٰرُ خَٰلِدِينَ فِيهَآ أَبَدًا ۚ ذَٰلِكَ ٱلْفَوْزُ ٱلْعَظِيمُ﴾

«Na wale waliotangulia, wa kwanza, miongoni mwa Muhajirina na Ansari na wale waliowafuata kwa wema, Allah ameridhika nao na wao wameridhika naye na amewaandalia Pepo zipitazo mito chini yake, watadumu humo milele. Huku ndiko kufuzu kukubwa» [At-Tawbah: 100].

Imani katika nyoyo zao ilikuwa kubwa kuliko milima. Usiku wao ulikuwa wa kusoma Qur-ani na kuswali Tahajjud. Alisema Nabii swala na salamu za Allah zimshukie: «**Hakika natambua nyumba za Ash'ariyyin kutokana na sauti zao za kusoma Qur-ani usiku**». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea. Na kutokana na wingi wa swala zao, mwanga wa Imani ulidhihirika katika nyuso zao,:

﴿سِيمَاهُمْ فِي وُجُوهِهِم مِّنْ أَثَرِ ٱلسُّجُودِ ۚ﴾

«Alama zao zi katika nyuso zao, kutokana na athari za kusujudu» [Al-Fat-h: 29].

Walivumilia shida kubwa kwa ajili ya dini. Amesema Sheikhul Islaam Allah amrehemu: «Kila Muislamu aliyemuamini Allah, basi Masahaba Allah awaridhie wana fadhila juu yake mpaka siku ya Kiyama. Na kila kheri ambayo Waislamu wako nayo, kwa hakika ni kwa baraka za waliyofanya masahaba»[1].

Kutaja fadhila zao ni wajibu, kuwapenda ni ibada, na kuwaheshimu ni dalili ya Imani. Amesema Nabii swala na salamu za Allah zimshukie: «**Maanswari, hawapendwi ila na Muumini, na hawachukiwi ila na mnafiki. Hivyo, yule anayewapenda, basi Allah anampenda, na yule anayewachukia, Allah anamchukia**». Imepokewa na Al-Bukhari.

Kuwapenda na kuwatukuza ni miongoni mwa sababu za kufufuliwa pamoja nao. Mtu mmoja alimuuliza Nabii swala na salamu za Allah zimshukie kuhusu Saa (Kiyama), akasema: «**Umejiandaa vipi kwa ajili yake?**» Yule mtu alisema: «Sijaiandalia kitu chochote, isipokuwa ninampenda Allah na Mtume wake swala na salamu za Allah zimshukie». (Mtume) akasema: «**Wewe utakuwa pamoja na wale uliowapenda**». Alisema Anas Allah amridhie: «Hatukuwahi kufurahia chochote kama tulivyofurahi kwa kauli ya Nabii swala na salamu za Allah zimshukie: «**Wewe utakuwa pamoja na wale uliowapenda**». Anas Allah amridhie akasema: «Basi mimi nampenda Nabii swala na salamu za Allah zimshukie, Abu Bakr, na Umar, na natarajia kuwa pamoja nao kwa sababu ya upendo wangu kwao, hata kama sitofanya matendo kama yao». Imepokewa na Al-Bukhari.

1 Minhaaj as-Sunnatu an-Nabawiyyah 6/376.

# Haki za Masahaba Allah awaridhie

Masahaba Allah awaridhie wana haki kubwa kwa Waislamu, ambazo ni pamoja na:

1 – Kuwapenda; kwani Allah aliwapenda na akawaahidi Pepo, Allah Mtukufu alisema:

﴿وَكُلًّا وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلۡحُسۡنَىٰۚ﴾

«Na wote, Allah amewaahidi mema» [Al-Hadiid: 10]. Ibnu Hazm Allah amrehemu amesema: «Masahaba wote Allah awaridhie waliokuwa na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, hata kwa siku moja, isipokuwa wanafiki; basi wote wako Peponi bila shaka, hakuna hata mmoja wao atakayeadhibiwa»[1].

2 – Kuridhika nao na kuwaombea dua; kwani Allah ameridhika nao, kama alivyosema Allah Mtukufu:

﴿وَٱلَّذِينَ جَآءُو مِنۢ بَعۡدِهِمۡ يَقُولُونَ رَبَّنَا ٱغۡفِرۡ لَنَا وَلِإِخۡوَٰنِنَا ٱلَّذِينَ سَبَقُونَا بِٱلۡإِيمَٰنِ﴾

«Na wale waliokuja baada yao husema: "Mola wetu Mlezi! Tusamehe sisi na ndugu zetu waliotutangulia katika imani"». [Al-Hashr: 10].

3 – Kuwa na nyoyo safi kwao; kwani wao ndio bora wa umma huu, kama alivyosema Allah Mtukufu:

﴿وَلَا تَجۡعَلۡ فِي قُلُوبِنَا غِلّٗا لِّلَّذِينَ ءَامَنُواْ﴾

«Na wala usitie katika nyoyo zetu chuki kwa walioamini» [Al- Hashr: 10].

1 Al-Durrah fiimaa Yaajibu I'tiqadahu, uk. 367.

4 – Kuitakidi ubora wao na fadhila zao; kama alivyosema Mtume swala na salamu za Allah zimshukie: «**Wabora wa umma wangu ni (watu wa) karne yangu, kisha wale wanaowafuata, kisha wale wanaowafuata**». Imepokewa na Al-Bukhari. Sheikhul Islaam Allah amrehemu alisema: «Hakukuwa wala hakutakuwa na kama wao»[1].

5 – Kutowatukana, kutowadharau, wala kupunguza hadhi yao; kwa mujibu wa kauli ya Nabii swala na salamu za Allah zimshukie: «**Msiwatukane Masahaba wangu; kwani lau mmoja wenu angelitoa sadaka ya dhahabu mfano wa mlima wa Uhud, hangefikia kibaba cha mmoja wao, wala nusu yake**». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

6 – Kuwafundisha watoto kuwapenda na namna walivyoishi; kwa sababu walisuhubiana na Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie na wakatusambazia Dini. Imam Malik Allah amrehemu alisema: «Wema waliotangulia walikuwa wanawafundisha watoto wao kuwapenda Abu Bakr na Umar, kama wanavyowafundisha sura katika Qur-ani»[2].

❖❖❖

1 Fataawaa Sheikhul Islaam 3/156.

2 Sharh Usuul I'tiqaad Ahl al-Sunnah wa al-Jama'ah" cha Al-Laalakaai, 7/1313.

# Sehemu ambazo haijuzu kisheria kuzizuru

## Hakufanywi ziara katika Madina isipokuwa misikiti miwili na makaburi mawili

**Misikiti ambayo ni sheria kuitembelewa katika Madina ni misikiti miwili, ambayo ni:**

1 – Msikiti wa Mtume.

2 – Msikiti wa Qubaa.

Kando na hii misikiti miwili katika Madina, misikiti iliobaki yote ni kama misikiti mingine, wala haikuja dalili yoyote katika sheria kupendekezwa kuyakusudia kuyazuru; Bali ni miongoni mwa mambo yaliozushwa na watu, na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie amesema: «**Yeyote atakayezusha katika jambo hili letu (la dini) kitu ambacho hakiko; basi itakua ni yenye kurudishwa**». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea, na katika riwaya ya Muslim: «**Yeyote atakayefanya amali yoyote ambayo haina amri yetu; basi itakua ni yenye kurudishwa**».

Amesema Sheikhul Islaam Allah amrehemu amesema: «Wala hakuna Madina msikiti ambao ni sheria kuutembelea isipokuwa msikiti wa Qubaa. Ama misikiti mingine iliobaki, basi ina hukumu kama misikiti mingine, na wala Mtume swala na salamu za Allah zimshukie hakuitenga kwa kuijia, na kwa sababu hii, wanachuoni katika watu wa Madina hawaikusudii sehemu yoyote katika maeneo hayo isipokuwa Qubaa pekee»[1].

**Maeneo mawili ya makaburi ambayo inapendekezwa kuyatembelea:**

1 – Makaburi ya Al-Baqi'.

2 – Makaburi ya Mashahidi wa Uhud.

Na hakika Nabii swala na salamu za Allah zimshukie aliyazuru maeneo hayo mawili ya makaburi.

---

1 Iqtidhwaa as-Swiraat al-Mustaqiim, 2/344.

Imam Malik Allah amrehemu alisema: «Hatuendi isipokuwa sehemu hizi: Msikiti wa Mtume, Msikiti wa Qubaa, maiti wa Al-Baqi' na Uhud; kwa sababu Nabii swala na salamu za Allah zimshukie hakukusudia kuyaendea isipokuwa misikiti hii miwili na maeneo haya mawili ya makaburi»[1].

1 Fataawaa Sheikhul Islaam, 27/381.

## Je Msikiti wa Qiblatain una fadhila yoyote?

Kuna baadhi ya watu wanauita Masjid al-Qiblatain (Msikiti wa vibula viwili), wanasema: Kwa sababu Masahaba walipokuwa katika swala, iliwajia habari ya kugeuzwa kwa Kibula kutoka Al-Masjid Al-Aqsa na kuwa Al-Masjid Al-Haraam wakiwa katika msikiti huu, wakageuka kutoka upande wa kaskazini na kuelekea upande wa kusini.

Wala haikuthibiti kuwa Msikiti wa «Al-Qiblatain» ndio mahali palipogeuziwa Kibula. Alisema As-Samhuudi Allah amrehemu: «Huu (msikiti uliogeuzwa Kibula ndani yake) ni miongoni mwa misikiti ambayo leo haijulikani mahali pake pako wapi»[1].

Na haikuthibiti kuwa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie aliutembelea msikiti huu, na hakuna fadhila yoyote iliyopokelewa kuhusu msikiti huu.

Vilevile, hakuna ubora wowote kwa msikiti huu katika kugeuziwa Kibula, kwani misikiti yote wakati huo - na ya kwanza ukiwa ni Msikiti wa Mtume, na Msikiti wa Qubaa - iliswaliwa ndani yake kuelekea pande zote mbili (Al-Aqsa na Makkah).

1 Wafaau al-Wafaa 3/46.

## Je «Al-Masajid as-Sab'a» kunatembelewa?

«Al-Masajid as-Sab'a» – (Misikiti saba): ni misikiti midogo iliyotawanyika nyuma ya mteremko wa Mlima Sal'i, ulioko upande wa magharibi-kaskazini wa Madina.

Na tangu ijulikane katika historia, idadi yake ni minne, lakini watu huiita: «Al-Masajid as-Sab'a».

Na yote hayo hayana msingi wowote, alisema As-Samhudi Allah amrehemu: «Wala sikupata msingi wowote kuhusu misikiti hio yote»[1].

Kwa hivyo, kuitembelea misikiti hii hakukuwekwa na sheria; kwa sababu haikuja katika Sunna, lakini si mengine, ni miongoni mwa mambo yaliozushwa na watu.

❖❖❖

1 Wafaau Al-Wafaa 3/43.

# Vita vya Mtume swala na salamu zimshukie vilivyokuwa Madina

# Vita vya Uhud

Waliposhindwa washirikina katika vita vya Badr, walishtushwa sana na pigo hilo, wakaazimia kujiandaa tena kukabiliana na Waislamu, na walitumia mwaka mzima katika maandalizi.

Na ilipofika mwezi wa Shawwal wa mwaka wa tatu wa Hijra (3 Hijria), walielekea Madina kukabiliana na Waislamu. Idadi yao ilikuwa wapiganaji 3,000, wakaweka kambi karibu na mlima wa Uhud, kaskazini mwa Madina.

Mtume swala na salamu za Allah zimshukie naye alitoka kuwakabili, lakini njiani kuelekea Uhud, Abdullah ibnu Ubayy bin Saluul - kiongozi wa wanafiki - alijiondoa na theluthi ya jeshi. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie akawaacha na kuendelea na wale waliokuwa pamoja naye, idadi yao ilikuwa wapiganaji 700, na wakaweka migongo yao kuelekea mlima wa Uhud.

Mtume swala na salamu za Allah zimshukie pia aliweka wapiga mishale 50 juu ya mlima wa ar-Rumaat, akawaamuru walazimiane na mahali hapo wasiondoke, -hali ya kuwa Jeshi la washirikina liko kati ya Waislamu na mji wa Madina.

Vikosi hivyo viwili vilipambana, na washirikina wakashindwa (mwanzoni), lakini pindi wapiga mishale walipoona kushindwa kwa makafiri, wakashuka masahaba 40 (miongoni ya wale 50) wakashuka mlima wa Rumaat. Ndipo Khalid ibnu Al-Waliid, ambaye wakati huo alikuwa bado yuko kwenye Ushirikina, alizunguka nyuma ya mlima wa Rumaat na kuwaua wale wapiga mishale 10 waliobaki juu ya mlima, wakaweza kuwazunguka waislamu na kuanza kuwashambulia kutoka pande zote. Kundi la Waislamu likashindwa, wengine wakatawanyika na kuuawa.

Washirikina wakamfikia Mtume swala na salamu za Allah zimshukie wakiwa wanataka kumuuwa, wakamjeruhi uso wake, wakavunja meno yake ya ruba'iyya (meno ya mbele) kwa jiwe, na vikuku viwili kutoka kwenye kofia yake ya chuma (mighfar) vilianguka usoni mwake. Wakavunja kofia yake ya chuma, na

wakampiga kwa mawe hadi akaanguka chini kwa ubavu wake, na kuangukia ndani ya shimo mojawapo ya mashimo yaliokuwa eneo la mapambano.

Washirikina wakampata Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, lakini kikundi cha Waislamu takriban kumi waliingia kati yake na adui ili kumlinda, wakapigana hadi wakauliwa wote.

Haya yote yalitokea siku ya Jumamosi, hatimaye vita vikapoa na kuisha. Waislamu waliokufa mashahidi walikuwa masahaba 70, ambao ni miongoni mwa masahaba bora, na upande wa washirikina, walikufa watu 22. Maiti wetu ni wa Peponi, na maiti wao ni wa Motoni.

# Vita vya Al-Ahzaab (makundi)

Allah ameelezea katika kitabu chake kuhusu vita vya Al-Ahzaab, na sura moja ya Qur-ani imepewa jina la vita hivi. Allahu Aliwaamuru waumini wakumbuke neema ya Allah juu yao katika vita hivi kila wakati. Alisema Allah mtukufu katika mwanzo wa sura hiyo:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱذۡكُرُواْ نِعۡمَةَ ٱللَّهِ عَلَيۡكُمۡ إِذۡ جَآءَتۡكُمۡ جُنُودٞ فَأَرۡسَلۡنَا عَلَيۡهِمۡ رِيحٗا وَجُنُودٗا لَّمۡ تَرَوۡهَاۚ وَكَانَ ٱللَّهُ بِمَا تَعۡمَلُونَ بَصِيرًا﴾

«Enyi mlioamini! Kumbukeni neema ya Allah kwenu yalipowajia majeshi, tukawapelekea upepo na majeshi msiyoyaona. Na Allah anayaona mnayoyatenda» [Al-Ahzaab: 9].

Na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, miongoni mwa yale aliyokuwa akisema anaporudi kutoka safarini au anapopanda Swafaa na Marwa, ni: «***Wa Hazamal-Ahzaaba wahdah* /Na akayashinda makundi peke Yake/**». Imepokewa na Muslim. Yote haya ni kwa ajili Waislamu wakumbuke neema ya Allah katika vita hivyo.

Vita hivi vilkuwa vigumu na vya kutisha, katika masiku ya baridi mnamo mwaka wa 5 Hijria, ambapo makundi mbalimbali yalikusanyika kupigana na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie.

Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, baada ya kusikia kuhusu maandalizi yao, aliwaamuru Waislamu wachimbe handaki kuzunguka Madina. Waliitikia amri hiyo wakiwa katika hali ya uchovu, baridi, na njaa. Jabir Allah amridhie, alielezea hali hiyo kwa kusema: «Jiwe kubwa sana lilikuwa mbele yetu. Wakaja kwa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie na kumwambia: “Kuna jiwe kubwa limetuzuia katika handaki”. Akasema: **“Nitashuka mwenyewe”**, Kisha akainuka hali ya kuwa tumbo lake limefungwa kwa jiwe (kutokana na njaa). Akasema (Jabir):

“Tukakaa siku tatu bila kula chochote”». Imepokewa na Al-Bukhari.

Makundi yalikusanyika kuelekea Madina yakiwa na wapiganaji 10,000, na Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie alitoka kuwakabili na Waislamu 3000, na handaki ndio liliokuwa kati yao na washirikina. Wakazingira Waislamu kwa mwezi mmoja. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie akamuelekea Mola wake na kumuomba, na katika dua yake ilikua: «**Ewe Allah, nakuomba uwashinde na uwatetemeshe**» Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea. Basi Allah akatia hofu katika nyoyo za washirikina, na akateremsha msaada wake, akawaadhibu kwa upepo mkali baridi, pia akamteremsha malaika waliowaogopesha na kukata nyoyo zao, Alisema Allah Mtukufu:

﴿فَأَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ رِيحًا وَجُنُودًا لَّمْ تَرَوْهَا﴾

«Tukawatumia upepo na majeshi ambayo hamkuyaona». [Al-Ahzaab: 9].

Basi wakatawanyika na kuondoka Madina wakiwa katika hali mbaya ya kushindwa na kupata hasara.

❖❖❖

# Maji ya Zamzam

## Fadhila za Maji ya Zamzam

Nchi hii - Allah aiafikie - huwa inasafirisha maji ya Zamzam kila siku kutoka Makkah Al-Mukarramah hadi Msikiti wa Mtume ili wageni wapate kunufaika nayo. Na Zamzam ina fadhila tatu:

**1 – Ni yenye Baraka:**

Zamzam ni maji yaliyobarikiwa. Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema kuhusu maji hayo: «**Hakika (maji ya Zamzam) ni yenye baraka**». Imepokewa na Muslim.

**2 – Ni Chakula:**

Maji ya Zamzam yana manufaa kwa mwili kama chakula kinavyonufaisha mwili. Amesema Nabii swala na salamu za Allah zimshukie: «**Hakika ni chakula chenye lishe)**». Imepokewa na Muslim. Abu Dharr Allah amridhie alisema: «Nilikunywa maji hayo, nikakaa kwa muda wa siku thelathini na masiku yake, nikiwa sina chakula kingine isipokuwa maji ya Zamzam, na nilinenepa mpaka matumbo yangu yakapasuka -yaani yalivimba kwa kunenepa- wala sikuhisi njaa.». Imepokewa na Muslim.

Ibnul Qayyim Allah amrehemu alisema: «Nimeona watu wakitumia maji ya Zamzam kama chakula kwa siku kadhaa, karibu nusu mwezi au zaidi, bila kuhisi njaa, na wanafanya Twawaaf pamoja na watu wengine bila kudhihirika na tofauti yoyote, na walinieleza kuwa wakati mwingine waliendelea hivi kwa siku arubaini»[1].

**3 – Ni Dawa:**

Zamzam -kwa idhini ya Allah- ni dawa ya magonjwa yote. Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema kuhusu maji hayo: «**Yana dawa ya maradhi**». Imepokewa na Al-Bazzaar. Ibnul Qayyim Allah amrehemu alisema: «Hakika mimi mwenyewe na wengine tumetumia maji ya Zamzam kama dawa

1 Zaad al-Ma'aad 4/361.

kwa mambo ya ajabu, nikajitibu nayo magonjwa kadhaa, nikapona - kwa idhini ya Allah»[1].

1 Zaad al-Ma'aad 4/361.

## Je yajuzu kutawadha kwa maji ya Zamzam?

Inaruhusiwa kutumia maji ya Zamzam kutawadha, kuoga, kufanya usafi, na mfano wa hayo; kwa sababu haya ni maji. Ibnul Qayyim Allah amrehemu alisema: «Inaruhusiwa kutawadha kwa maji yaliyobarikiwa, na baraka yake haisababishi kuchukizwe kutawadhia nayo. Kwa msingi huo, hakuchukizwi kutawadha kwa maji ya Zamzam»[1].

1 Zaad al-Ma'aad 3/584.

## Je manufaa ya maji ya Zamzam yanapotea yakitolewa nje ya Makkah?

Maji ya Zamzam baraka yake inabaki, sawa maji hayo yawe yako Makkah au yametolewa nje ya Makkah, manufaa yake hayapotei yakipelekwa nje ya Makkah. Amesema Sheikhul Islaam Allah amrehemu: «Yeyote anayebeba maji ya Zamzam anaruhusiwa, kwani wema waliopita walikuwa wakiyabeba»[1]. Wala hakuna tatizo kuchanganya maji ya Zamzam na maji mengine, kwani yote ni maji.

❖❖❖

1 Fataawaa Sheikhul Islaam, 26/154.

# Safari ya kwenda Makkah Al-Mukarramah

## Nitaweka nia ya Ihram wapi nikiwa natoka Madina?

Miiqaat (mpaka) ya wakazi wa Madina na wale wanaoipita ambao si wakazi wake ni: Dhul Hulaifah - jina hili ni aina ya mmea uliokuwepo eneo hilo. Pia inaitwa «Abyaar Ali». Eneo hilo liko upande wa kusini-magharibi mwa Msikiti wa Mtume na lina umbali wa takribani kilomita 10 kutoka msikitini.

Na Miiqaat hii ndio iliyo mbali zaidi kutoka Makkah Al-Mukarramah, ikiwa na umbali wa takriban kilomita 400 kutoka Makkah.

Kwa hivyo, yeyote anayetaka kufanya Hija au Umra akiwa Madina, sawa awe ni mkazi wa Madina au la, hairuhusiwi kwake kupita Miiqaat hii bila ya kuhirimia (kuweka nia ya Ihram). Ikiwa mtu atavuka Miiqaat hii bila nia ya Ihram, itamlazimu arudi na ahirimia kutoka pale. Ikiwa hatarejea, anatakiwa kutoa fidia ya damu (kuchinja mnyama kama fidia).

## Je yajuzu kuweka nia ya Ihram kutoka nyumbani Madina?

Inaruhusiwa kuoga na kuvaa mavazi yako ya Ihram kutoka nyumbani kwako Madina. Ukifika kwenye Miiqaat, weka nia ya Ihram Hali ya kuwa unatembea na useme: «*Labbayka Allahumma Labbayk*». Wala sio lazima kusimama kwenye Miiqaat ndio uweke nia au uswali rakaa mbili.

## Je mwanamke aliye kwenye hedhi atahirimia anapofika Miiqaat?

Mwanamke aliye kwenye hedhi anafanya kama wanavyofanya wengine - kuhusiana na kuweka nia ya Ihram, kusema “Talbiyah", kuepuka mambo yaliyoharamishwa wakati wa Ihram, na kadhalika. Ambacho hafanyi ni kutufu (kuzunguka) Al-Kaaba, hafai kutufu mpaka atwahirike (amalize hedhi).

## Ikiwa safari imekaribia na mwanamke ana hedhi, je atafanya Twawaaf?

Twawaaf (mzunguko kwenye Al-Kaaba) zinazobaki kwa mwanamke mwenye hedhi, ni mojawapo ya hizi:

1 – Ikiwa Twawaaf iliobaki kwake ni Twawaaf al-Ifaadhwa katika Hija, au Twawaaf ya Umra, na wakati wa kusafiri kutoka Makkah kuelekea nchi yake ukawa umefika, ikawa vigumu kwake kukaa Makkah hadi atakapotahirika, na hakutakuwa na wepesi kwake kurudi baada ya kusafiri, basi Sheikh Abdulaziz ibnu Baaz Allah amrehemu alisema: «Itajuzu kwake, kwa mujibu wa maoni sahihi (ya wanachuoni), ajihifadhi vizuri na afanye Twawaaf kwa nia ya Hija, na hilo litamtosheleza kwa mujibu wa kundi la wanachuoni, wakiwemo Sheikhul Islaam Ibnu Taymiyyah, na mwanafunzi wake mwanachuoni Ibnul Qayyim Allah amrehemu, na wengineo katika wenye elimu»[1].

2 – Ikiwa Twawaaf iliobaki kwake ni Twawaaf al-Widaa' (mzunguko wa kuaga): basi atasafiri na wala hatalazimika na kitu, na Hija yake ni sahihi, amesema Ibnu Abbas Allah awaridhie: «Watu waliagizwa kwamba jambo la mwisho wafanye wakiwa Makkah ni kuzunguka al-Kaaba, isipokuwa mwanamke mwenye hedhi amepunguziwa mzigo huo». Wameafikiana Al-Bukhari na Muslim kuipokea.

❖❖❖

1 Fataawaa Tata'allaqu bi-Ahkaam al-Hajj wal-Umrah waz-Ziyaarah 1/118.

# Mwenye Kuzuru
# Al-Madiinatu Al-Munawwarah

## Ujumbe unaoubeba kutoka Madina

Miongoni mwa neema za Allah ni kuwa mkamilifu wa ibada kwake, na yeyote aliyefanya Hija au Umra, au alitembelea Msikiti wa Mtume; anapaswa kurudi nyumbani akiwa katika hali bora zaidi. Na miongoni mwa sababu zinazosaidia jambo hilo ni:

1 – Kubaki juu ya Tawhidi (Kumpwekesha Allah), na kutowaomba maiti na makaburi, kutowataka msaada na kutowataka wakidhi mahitaji, Amesema Allah aliyetakasika:

﴿فَٱسۡتَقِمۡ كَمَآ أُمِرۡتَ﴾

«Basi simama sawa sawa (kwenye dini) kama ulivyoamrishwa» [Huud: 112].

2 – Kufuata mwenendo wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie katika mambo yote, kama alivyosema Allah aliyetukuka:

﴿لَّقَدۡ كَانَ لَكُمۡ فِي رَسُولِ ٱللَّهِ أُسۡوَةٌ حَسَنَةٞ لِّمَن كَانَ يَرۡجُواْ ٱللَّهَ وَٱلۡيَوۡمَ ٱلۡأٓخِرَ وَذَكَرَ ٱللَّهَ كَثِيرٗا﴾

«Hakika yenu mna mfano mwema wa kuiga kutoka kwa Mtume wa Allah kwa anayemtaraji Allah na Siku ya Mwisho na akamtaja Allah sana» [Al-Ahzaab: 21].

3 – Kuhifadhi swala za faradhi kwa jamaa katika nyumba za Allah, kama alivyosema Allah Mtukufu:

﴿وَأَقِيمُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتُواْ ٱلزَّكَوٰةَ وَٱرۡكَعُواْ مَعَ ٱلرَّٰكِعِينَ﴾

«Na simamisheni swala na toeni zaka na mrukuu pamoja na wanaorukuu» [Al-Baqarah: 43].

4 – Uwe mfano mwema, kwani yeyote aliyefanya Hija ya nyumba ya Allah, au Umra, au aliutembelea Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie anawajibika kuwa mwongofu kwa wengine kila mahali.

5 – Kukithirisha kusoma na kutafakari Kitabu cha Allah kitukufu, kwani ni kinga dhidi ya fitina -kwa idhini ya Allah-, na kinavutia kheri na baraka, kwa hivyo yeyote anayekikaribia (kitabu cha Allah) anapata baraka kubwa kutoka kwake, kama alivyosema Allah Mtukufu:

﴿كِتَٰبٌ أَنزَلۡنَٰهُ إِلَيۡكَ مُبَٰرَكٞ﴾

«Kitabu ambacho tumekuteremshia wewe ni chenye baraka» [Swaad: 29].

Na kusoma herufi moja ya kitabu hiki kuna ujira wa jema moja, na jema moja ni kwa mara kumi yake, hadi mara nyingi sana.

6 – Kusoma vitabu vya Sunna na elimu ya kisheria, kwani vinabainisha na kufafanua Kitabu cha Allah, na mtu hupata kwayo daraja duniani na Akhera, Allah aliyetukuka amesema:

﴿يَرۡفَعِ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ مِنكُمۡ وَٱلَّذِينَ أُوتُواْ ٱلۡعِلۡمَ دَرَجَٰتٖ﴾

«Allah anawainua daraja za juu wale walioamini miongoni mwenu, na wale waliopewa elimu» [Al-Mujaadilah: 11].

Tunamwomba Allah apokee kutoka kwa wote matendo mema, na awaruzuku uthabiti katika dini, na swala na salamu za Allah zimshukie Mtume wetu Muhammad!

***Kimeisha kwa himdi za Allah!***

# FIHRISI YA MAUDHUI

Utangulizi wa Mheshimiwa Sheikh Abdur-Rahman ibnu Abdul-aziz as-Sudais ........ 6
Utangulizi ........ 9
Safari ya Kuelekea al-Madiinatu al-Munawwarah ........ 11
Kuitakasa Nia ........ 12
Hatari ya Riya ........ 14
Ananuwia nini anayetaka kuzuru Al-Madiinatu Al-Munawwarah? ........ 16
Kusafiri Mwanawake bila Mahram ........ 18
Hukumu ya kusema: “Nifikishie salamu zangu kwa Mtume swala na salamu zimshukie” ........ 19
Kuwasili Al-Madiinatu al-Munawwarah ........ 20
Neema ya kufika Al-Madiinatu al-Munawwarah ........ 21
Madina Kabla ya Uislamu ........ 22
Majina ya Madina ........ 24
Jina ambalo Mtume swala na salamu zimshukie alichukia iitwe kwalo Madina ........ 26
Kwa nini Mtume swala na salamu zimshukie aliondoka Makkah na kuhamia Madina? ........ 27
Je kuna dua maalumu ya kuingia Madina? ........ 28
Adabu za mwenye kuzuru Madina ........ 29
Ratiba ya Aliyezuru Madina ........ 30
Fadhila za Mji wa Mtume ........ 32
Fadhila za Madina ........ 33

❈ Kwanza: Fadhila za kiimani:.....33

❈ Pili: Kuwa ni mji mzuri:.....36

❈ Tatu: Kuwepo amani ndani yake:.....38

❈ Nne: Utukufu wa kuishi Madina.....44

❈ Tano: Baraka zake:.....47

❈ Sita: Tende zake:.....49

❈ Saba: Sehemu mashuhuri zilizoko ndani yake:.....51

❈ Fadhila ya kufa katika Madina:.....53

❈ Madina utakuwa mji wa mwisho kuharibika:.....54

Msikiti wa Mtume.....55

(Al-Masjidun-Nabawi).....55

Fadhila ya Msikiti wa Mtume.....56

Ujenzi wa Msikiti wa Mtume na Upanuzi wake Katika Historia.....57

Rawdha.....60

Mihirabu.....61

Mimbari.....62

Kuchomeka kwa Msikiti wa Mtume.....64

Swala katika Msikiti wa Mtume.....65

Dua ya kuingia Msikiti wa Mtume.....66

Kuongezeka kwa thawabu za swala katika Msikiti wa Mtume.....67

Niswalie sehemu gani swala ya jamaa katika Msikiti wa Mtume?.....68

Ni lipi bora: kuswali katika Rawdha au kuswali nyuma ya imamu?.....69

Kukamilisha safu ni jambo la kisheria....................................................70
Hukumu ya Kupita Mbele ya Mwenye Kuswali....................................71
Hukumu ya kuswali mbele ya Imamu....................................................72
Namna ya Kuswali Swala ya Janaza ......................................................73
Ikiwa kuna jeneza nyingi, Je qiraati zitaongezeka?................................74
Je naweza kuswali swala ya Sunna katika kila wakati?..........................75
Nifanye nini katika Msikiti wa Mtume kando na kuswali?...................76
Je kuswali swala arobaini za faradhi katika Msikiti wa Mtume ina asili yoyote?..........................................................................................77
Kupaza Sauti Katika Msikiti wa Mtume ................................................78
Dua ya Kutoka Msikiti wa Mtume ..........................................................79
Mtu aliyehiji lakini hakuzuru Msikiti wa Mtume, Je Hija yake ni pungufu? ..................................................................................................80
Nyumba za Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.......... 81
Nyumba za Mtume swala na salamu za Allah zimshukie .....................82
❈ Vipengele vya Nyumba: .....................................................................82
❈ Maandiko yaliokuja kuhusu "Bayt" (chumba) na Hujra (uani).........82
❈ Aina ya jengo lake: ...........................................................................85
❈ Mahali pake:.......................................................................................85
Wake za Mtume swala na salamu za Allah zimshukie. ..........................88
1. Khadija binti Khuwaylid, Allah amridhie: ..........................................88
2. Sauda binti Zama'a Allah amridhie.....................................................89
3. Aisha binti Abu Bakr as-Swiddiiq Allah amridhie .............................89
4. Hafswa binti Umar ibnu Al-Khattwaab Allah amridhie ....................90
5. Zainab binti Khuzaimah Al-Hilaaliyyah Allah amridhie...................90

6. Ummu Habiiba Ramla bint Abu Sufyan Allah amridhie....................90
7. Ummu Salamah Hind binti Abi Umayyah Allah amridhie...............90
8. Zainab binti Jahsh Allah amridhie......................................................91
9. Juwayriyya binti Al-Haarith Allah amridhie......................................92
10. Swafiyya binti Huyay Allah amridhie.............................................93
11. Maimuna binti Al-Haarith Al-Hilaliyya Allah amridhie..................93
Maisha yao pamoja na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie. .93
Al-Hujratun-Nabawiyyah ......................................................... 95
Al-Hujratun-Nabawiyyah ......................................................................96
❈ Maelezo ya Al-Hujratun-Nabawiyyah.................................................96
❈ Hatua ya kwanza..................................................................................96
❈ Hatua ya pili: ................................................................................... 101
❈ Hatua ya tatu: ................................................................................... 103
❈ Hatua ya nne: ................................................................................... 104
❈ Hatua ya tano: ................................................................................... 106
❈ Hatua ya sita:..................................................................................... 107
❈ Hatua ya saba: ................................................................................... 108
❈ Hatua ya nane:....................................................................................113
❈ Hatua ya tisa:......................................................................................114
❈ Hatua ya kumi:....................................................................................115
❈ Hatua ya kumi na moja: .................................................................... 122

Urefu wa kuta za chumba cha mtume sasa hivi .................................. 123

Uzio wa nje ........................................................................................ 125

Uzio wa Shaba na sehemu ilioko chumba cha Mtume ndani yake ... 128

Masafa yalioko kati ya mtu anayemsalimia Mtume swala na salamu zimshukie na kaburi lake .................................................................... 129

Masafa yalioko baina ya uzio wa shaba wa kushoto na kaburi la Mtume swala na salamu zimshukie .................................................................. 131

Je inawezekana kuingia kwenye chumba cha Mtume? ...................... 133

Hekima ya kuta na vizuizi vya shaba .................................................. 134

Sakafu ya Nyumba na Kuba ................................................................ 135

❈ Sakafu ya Nyumba: ........................................................................ 135

❈ Kuba Kubwa: .................................................................................. 136

Kaburi la Mtume swala na salamu zimshukie na wenzake wawili Allah awaridhie hayajaonekana isipokuwa mara mbili ................................ 139

Je inafaa kujipangusa na ukuta wa chumba cha Mtume? ................... 141

Kutabaruku ......................................................................................... 142

❈ Kigawanyo cha kwanza: Kutabaruku kwa njia ya kisheria, ........... 142

❈ Kigawanyo cha pili: Kutabaruku kulikokatazwa, ............................ 143

Kuzuru Kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie na wenzake wawili Allah awaridhie ............................................ 146

Mtume wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie........ 147

Abu Bakr As-Swiddiiq Allah amridhie ............................................... 149

Umar ibnu Al-Khattwaab Allah amridhie ........................................... 151

Kuelezea kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie na wenzake wawili Allah awaridhie ......................................................... 153

Je Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alizikwa msikitini? . 154

Namna ya kuzuru kaburi la mtume swala na salamu za Allah zimshukie na rafiki zake wawili Allah awaridhie ............................................. 158
Je Allah anaombwa kaburini kwa Mtume swala na salamu zimshukie? ............................................................................................................. 160
Hukumu ya kuomba kwa cheo cha Mtume swala na salamu za Allah zimshukie ............................................................................................ 161
Je yafaa kutaka kitu kutoka kwa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie baada ya kufa kwake? ........................................................ 162
Hukumu ya kusoma al-Faatiha kwenye kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie ................................................................ 164
Hukumu ya kurefusha kusimama kwenye kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie ................................................................ 165
Hukumu ya kurudiarudia kwenye kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie kwa ajili ya kumsalimia ......................................... 166
Hukumu ya kuelekea kaburi kwa mbali ............................................ 167
Hadithi ambazo hazikusihi kuhusu ziara ya kaburi la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie ................................................................ 168
Masjid Qubaa ................................................................................ 169
Masjid Qubaa ................................................................................ 170
Ubora wa kuswali katika msikiti wa Qubaa ...................................... 171
Kuzuru Makaburi ........................................................................... 172
Hikma ya Kuzuru Makaburi ............................................................ 173
Aina za Kuzuru Makaburi ............................................................... 174
❈ Kigawanyo cha kwanza: Kuzuru kwa kisheria: ............................. 174
❈ Kigawanyo cha pili: Kuzuru kusokua kisheria: .............................. 174
Hukumu ya wanawake kuzuru makaburi .......................................... 177
Kurusha mbegu na kutia marashi juu ya makaburi ........................... 178
Al-Baqi'i ........................................................................................ 179

Al-Baqi'i .......... 180
❈ Kuzuru makaburi ya Al-Baqi'i .......... 180
❈ Je kuna kaburi la yeyote katika masahaba linalojulikana ndani ya Al-Baqi'i? .......... 180
Je kuzikwa Al-Baqi'i kuna ubora wowote? .......... 181
Je kuzikwa Madina kuna ubora wowote? .......... 189
Eneo la Makaburi ya Mashahidi wa Uhud .......... 190
Eneo la Makaburi ya Mashahidi wa Uhud .......... 191
Masahaba, Allah awaridhie .......... 192
Fadhila za Masahaba Allah awaridhie .......... 193
Haki za Masahaba Allah awaridhie .......... 195
Sehemu ambazo haijuzu kisheria kuzizuru .......... 197
Hakufanywi ziara katika Madina isipokuwa misikiti miwili na makaburi mawili .......... 198
Je Msikiti wa Qiblatain una fadhila yoyote? .......... 200
Je «Al-Masajid as-Sab'a» kunatembelewa? .......... 201
Vita vya Mtume swala na salamu zimshukie vilivyokuwa Madina .......... 202
Vita vya Uhud .......... 203
Vita vya Al-Ahzaab (makundi) .......... 205
Maji ya Zamzam .......... 207
Fadhila za Maji ya Zamzam .......... 208
Je yajuzu kutawadha kwa maji ya Zamzam? .......... 210
Je manufaa ya maji ya Zamzam yanapotea yakitolewa nje ya Makkah? .......... 211
Safari ya kwenda Makkah Al-Mukarramah .......... 212

Nitaweka nia ya Ihram wapi nikiwa natoka Madina?.......................... 213
Je yajuzu kuweka nia ya Ihram kutoka nyumbani Madina? .............. 214
Je mwanamke aliye kwenye hedhi atahirimia anapofika Miiqaat? ... 215
Ikiwa safari imekaribia na mwanamke ana hedhi, je atafanya Twawaaf? ........................................................................................................ 216
Mwenye Kuzuru Al-Madiinatu Al-Munawwarah.................... 217
Ujumbe unaoubeba kutoka Madina..................................................... 218
FIHRISI YA MAUDHUI......................................................... 220

TAASISI YA TWALIBUL ILM YA KUNUSHURU NA KUGAWA
00966506090448

Na katika zama hizi angavu, al-Madiinatu al-Munawwarah ilipata uangalizi mzuri wa viongozi wa nchi hii iliyobarikiwa – Mamlaka ya Kiarabu ya Saudia - kwa kusimamia kwao na kupatia kipaumbele kila jambo ambalo linauhudumikia Uislamu na Waislamu, pamoja na kuyatukuza maeneo yao matakatifu. Jambo ambalo limefanya wanaotembelea na wenye kufanya Hija na Umra kuona athari yake. Na Sisi katika uongozi mkuu wa mambo ya msikiti mtakatifu (wa Makkah) na msikiti wa Mtume tunashughulikia kila jambo linalodhihirisha cheo cha Misikiti Miwili Mitukufu, na kuwaelimisha wageni wanaoyatembelea, wenye kufanya Umra na mahujaji kuhusu adabu na hukumu za Msikiti mtakatifu na Msikiti wa Mtume, kupitia mwanga wa Qurani na Sunnah kwa njia itakayopelekea kufikia matarajio ya uongozi .wa busara

Na hakika sheikh alinidhania vyema na kunipa fursa ya kuandika baadhi ya mistari mwanzo wa kitabu chake, basi natarajia Allah atawanufaisha watu na mtunzi na kitabu chake, na atuzidishie ujira mimi, yeye na wasomaji watukufu, na atuhifadhie itikadi yetu, uongozi wetu, nchi yetu na neema zetu, amani, usalama na utulivu wetu; kwani Yeye ndiye .mbora anayeombwa na kutarajiwa

محبكم الداعي لكم

Ameandika, anayewapenda na anayewaombea -
Abdur-Rahman ibnu Abdul-aziz as-Sudais -
Raisi mkuu wa usimamizi wa mambo ya Msikiti
Mtakatifu na Msikiti wa Mtume,
Imamu na Hatibu wa Msikiti Mtakatifu.

ردمك: ٩٧٨-٦٠٣-٠٢-٥٦٠٥-١